

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Aprili, 2020

D U A

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASISHWA MEZANI:-

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

WAZIRI WA MAJI:

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2019 [

].

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. SULEIMAN AHMED SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. TUNZA I. MALAPO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

Mtaa wa Maili Kumi na Nane

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa mgogoro kati ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Mvomero juu ya Mtaa wa Maili Kumi na Nane ambao kimsingi upo Mjini.

Je, ni lini Serikali itamaliza Mgogoro huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utatuzi wa mgogoro kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kuhusu Mtaa wa Maili Kumi na Nane ulifanyika ambapo uongozi wa Mkoa wa Morogoro ulifanya kikao cha pamoja tarehe 2/10/2018 kilichohusisha halmashauri zote mbili na kukubaliana kufuta Mtaa wa Kumi na Nane ili eneo hilo liunganishwe katika Kijiji cha Wami Sokoine kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho hayo yameshafanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 536 la tarehe 19/07/2019 la Mamlaka za Miji na Tangazo la Serikali Na. 537 la tarehe 19/07/2019 la Mamlaka za Wilaya kwa kuufuta Mtaa wa Maili Kumi na Nane uliokuwa katika Kata ya Mkundi iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ili kuwa sehemu ya eneo la Kijiji cha Wami Sokoine kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.

Na. 85

Kutoa Elimu Bure Kwa Watu Wenye Ulemavu

MHE. AMINA S. MOLLEL aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu bure kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao wanapata fursa ya

kuendelea na kidato cha tano na sita kwani wanafunzi hao pia wanatoka kwenye mazingira magumu?

WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza azma yake ya kutoa fursa ya elimu kwa watu wote ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi mwenye sifa za kuendelea na kidato cha Tano anapata nafasi na kumaliza mzunguko wa elimu katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya kidato cha Tano na Sita nchini hutolewa kwa ushiriano kati ya wazazi/walezi na Serikali. Wazazi/walezi hupaswa kulipa ada ya shilingi elfu sabini (70,000) tu kwa mwaka kwa ajili ya kuchangia gharama za utoaji wa elimu ambapo Serikali hubeba gharama zingine.

Aidha, upo mwongozo ambapo halmashauri hubaini wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato duni ili waweze kulipiwa ada. Hivyo, Serikali itaendelea kushirikiana na wazazi/walezi katika utoaji wa Elimu katika ngazi hii ya kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vifaa maalumu vya kielimu na saidizi vinapatikana ili kukidhi mahitaji yao ili kupata Elimu iliyo bora.

Na. 86

Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufaa Tanzania

MHE. USSI S. PONDEZA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mahakama ya Rufaa ni suala la Muungano.

Je, kwa nini Wanasheria waliopo Zanzibar katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahakama Kuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar hawateuliwi kufanya kazi katika Mahakama ya Rufaa Tanzania?

Je, Zanzibar kuwa na Jaji mmoja katika Mahakama ya Rufaa kunaleta sura gani katika kuendeleza misingi ya Muungano?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza Mbunge Chumbuni lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 118 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inatoa utaratibu na sifa za watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani. Sifa hizo ni "sifa ya kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyoielezwa katika ibara ya 109 ya Katiba hii au kutoka miongoni mwa watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria zinazotumika Zanzibar na wamekuwa na sifa hizo kwa miaka isiyopungua kumi na tano."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sifa hizo zipo sifa nyingine za kiutawala ambazo huzingatiwa kabla ya uteuzi. Majaji wa Mahakama ya Rufani huteuliwa kwa sifa zilizoainishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo, suala la sehemu anapotoka Jaji husika siyo mojawapo ya kigezo cha uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu itaendelea kuheshimu na kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania ambayo imeweka misingi kwa Serikali zote mbili ya namna ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Na. 87

Hitaji la Nyumba za Polisi Nchini

MHE. ANNA J. GIDARYA aliuliza:-

Jeshi la Polisi katika nchi yetu ni muhimili unaolinda amani pamoja na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeanzisha vituo vya Polisi katika Tarafa na kata mbalimbali bila kuwa na nyumba za kuishi, Je serikali ina mkakati gani wa kuwajengea nyumba za kuishi na vituo ili waondokane na kero na hofu kulingana na uhalisia wa mazingira yao ya kazi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhaba wa nyumba za makazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi nchini, hata hivyo zipo juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo la makazi ya Askari kwa nchi nzima. Mathalani, ujenzi wa jumla ya nyumba 450 katika mikoa Tanzania bara na Zanzibar ambapo baadaye nyumba zitajengwa katika wilaya na hatimaye kwenye Tarafa na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linao utaratibu wa kulipa fedha za makazi kwa Askari ambaye atakuwa anaishi nje ya kambi ya Jeshi la Polisi na hivyo kumuwezesha kumudu gharama za pango.

Kuboresha Makazi Duni ya Wananchi – Manyara

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vigezo vya kupima umaskini wa Wananchi ni pamoja na hali duni ya makazi na maskani ya Watu wake; katika Mkoa wa Manyara bado wapo Wananchi wenye makazi duni ya udongo na nyasi pamoja na vibanda vya kuishi visivyokidhi haja.

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuboresha makazi duni ya Wananchi ikiwemo Mkoa wa Manyara?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbula Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mikakati ya kuboresha makazi duni nchini Serikali ilianzisha Wakala wa Utafiti wa Vifaa vya Ujenzi na Nyumba Bora () kwa ajili ya kufanya utafiti wa vifaa vya ujenzi vinavyopatikana hapa nchini na kuviboresha ili viweze kutumika kujenga nyumba imara na bora. Mfano matumizi ya tofali za udongo kwa kutumia saruji kidogo (), ujenzi kwa kufungamanisha tofali () bila saruji, vigae vinavyotengenezwa kwa mchanganyiko wa mchanga, saruji na nyuzi za katani na mashine za kuzalisha vifaa hivyo. Aidha, elimu ya matumizi ya teknolojia hiyo imetolewa kwa halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa limekuwa likitoa ushauri na mafunzo kwa vikundi vya ushirika wa nyumba juu ya namna ya kujenga nyumba za gharama nafuu. Hivyo, Serikali inashauri wananchi kujiunga na kuanzisha vikundi vya ushirika wa nyumba ili waweze

kupatiwa elimu ya matumizi ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu vilivyofanyiwa na wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali kupitia Wizara yangu ilizikopesha halmashauri 24 jumla ya shilingi bilioni 6.28 kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ambapo jumla ya viwanja 40,651 vimepimwa na umilikishaji unaendelea. Aidha, kwa sasa Serikali inakamilisha mradi mkubwa wa kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini kama sehemu ya mkakati wa kuboresha makazi duni mijini na vijijini.

Na.89

Hitaji la Maji Kata za Masaka na Kalenga Jimbo na Kalenga

MHE. GODFREY W. MGIMWA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko kubwa la watu pamoja na miundombinu ya zamani imesababisha upungufu wa upatikanaji wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya Jimbo la Kalenga hususan Kata za Masaka na Kalenga.

Je, Serikali ni lini itafanya utafiti wa kina na kuanza ujenzi wa miradi ya maji kwenye Kata hizo?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya Jimbo la Kalenga hususan kata za Masaka na Kalenga. Kata ya Masaka ina jumla ya vijiji vitatu (3) ambavyo ni Kaning'ombe, Sadani, Makota na Kata ya Kalenga ina jumla ya vijiji vitatu (3) ambavyo ni Tosamaganga, Kalenga na Isakalilo. Katika kutatua tatizo hilo, Serikali ilikamilisha mradi wa bomba

ambapo vijiji viwili (2) vya Kaning'ombe na Sadani vya Kata ya Masaka vinapata huduma ya maji. Kwa upande wa kijiji cha Makota huduma ya maji inapatikana katika baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji 3 vya kata ya Kalenga vinapata huduma ya maji kupitia mradi wa pamoja wa Tanangozi – Kalanga ambao una jumla ya vijiji 11 kutoka kata za Mseke, Masaka, Kalenga na Ulanda. Mradi huu ulijengwa na DANIDA miaka ya 1980 ambapo kwa sasa hali ya huduma yake haitoshelezi mahitaji kutokana na ongezeko la watu pamoja na miundombinu kuwa ya muda mrefu. Katika kuhakikisha kuwa changamoto ya maji katika Kata za Kalenga inapatiwa ufumbuzi, Serikali kupitia ufadhili wa WARIDI/ ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha upanuzi wa maji ya Iringa () ambapo utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo itaendelea kufanya usanifu wa miradi mipya katika Jimbo la Kalenga pamoja na ukarabati wa miradi ya zamani ili kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo.

Na. 90

Mradi wa Umwagiliaji – Kijiji cha Mangwila

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilitumia takribani shilingi Bilioni moja kutekeleza ujenzi wa mradi wa umwagiliaji katika kijiji cha Mangwila Kata ya Mwanyakina iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Lakini Mradi huo ulijengwa chini ya kiwango ikilinganishwa na thamani ya matumizi ya fedha.

Je, ni lini mradi huo ulikabidhiwa kwa wananchi na ni wakulima wangapi walinufaika nao?

Je, Serikali ipo tayari kwenda kukagua mradi huo na kufanya uchunguzi ili kubaini kasoro za mradi na kuwawajibisha wale watakaobainika kuuhujumu?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa Kijiji cha Mangwila haujawahi kukabidhiwa kwa wananchi kwa kuwa haukukamilika. Miundombinu iliyojengwa ni Banio pamoja na Mfereji mkuu ambao kwa sasa umefukiwa na mchanga kwa sababu ya mvua. Aidha, ni kweli mradi huo ulijengwa chini ya kiwango ukilinganisha na fedha iliyotumika kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia hujuma katika mradi huo, Wizara ilishalifikisha suala hilo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambayo inaendelea na uchunguzi ili kubaini kasoro za utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyotekelezwa kupitia Mradi wa DASIP ukiwemo mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Mangwila uliopo Wilaya ya Meatu. Baada ya kukamilika kwa uchunguzi huo, Serikali itachukua hatua stahiki kwa watumishi na wakandarasi wote watakaobainika kuhusika katika kuhujumu miradi hiyo. Vilevile, katika kuimarisha utendaji wa Tume ya Umwagiliaji Serikali imechukua hatua ya kuwasimamisha baadhi ya watumishi wa Tume ya Umwagiliaji ili kupisha uchunguzi wa tuhuma mbalimbali zinazowakabili. Aidha, Serikali ipo tayari kwenda tena kukagua vitendo vya hujuma vya mradi huo na kuchukua hatua stahiki.

Na. 91

Kupandishwa Hadhi Barabara

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mtiri – Ifwagi – Mdaburo – Ihanu – Isipi – Mpangatazara hadi Mlimba inaunganisha Wilaya mbili, Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Kilolo. Pia inaunganisha mikoa miwili, Iringa na Morogoro; Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa Ujenzi aliahidi kuipandisha hadhi kuwa barabara ya T

Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa kuipandisha hadhi barabara hii?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mngimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mnamo mwezi Julai 2017 Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza mtandao wa barabara za vijijini na mijini yaani barabara za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuanzishwa kwa Wakala huu ni kuhakikisha kuwa barabara za wilaya zinapata msukumo wa kutosha kuliko hapo awali ikiwemo barabara ya Mtiri – Ifwagi – Mdaburo – Ihanu – Isipi – Mpangatazara hadi Mlimba. Kwa kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulianzishwa na kupewa jukumu la kusimamia na kuendeleza barabara za Wilaya nchini, nashauri tuendeleze kuipa ushirikiano ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi na kukidhi maratajio ya kuundwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kupandisha hadhi barabara kutoka barabara ya Wilaya kuwa barabara ya Mkoa zimeainishwa katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, kama barabara hiyo imekidhi vigezo vya kupandishwa hadhi maombi yawasilishwe kufuata taratibu hizo.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali langu halijajibiwa, tayari taratibu zote zilishafuatwa ikiwemo vikao vyote vya Bodi ya Barabara ya Mkoa na Waziri mwenye dhamana wakati huo aliandikiwa barua na Mkuu wa Mkoa wa Iringa, lini Serikali itaanza huo mchakato wa kupandisha hadhi hiyo barabara.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mwaka 2016, Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mheshimiwa Amina Juma Masenza, aliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri maombi ya Bodi ya Mkoa ya Barabara ya kupandisha hadhi barabara hii. Wakati uchambuzi wa maombi hayo na mengine ukiendelea, Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini na hivyo kusitisha maombi yote ili barabara hizo zishughulikiwe na chombo hicho ambacho kilipewa jukumu mahususi la kusimamia na kuendeleza barabara za wilaya.

Mheshimiwa Spika, iwapo Mheshimiwa Mbunge anaona bado ipo haja hiyo tunaomba awasilishe upya maombi hayo kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa ili yafikiriwe upya.

Na. 92

Barabara ya Kutoka Dumila-Rudewa-Kilosa-Mikumi

MHE. JOSEPH L. HAULE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kipande cha barabara muhimu kutoka Dumila -Rudewa-Kilosa-Mikumi yenye urefu wa Kilometa 142 kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO atajibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Dumila – Rudewa – Kilosa – Mikumi yenye urefu wa kilometa 142 ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini ().

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali kupitia Wakala wa Barabara nchini, imeendelea kuimarisha na kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kama ifuatavyo: -

Sehemu ya Dumila – Rudewa yenye urefu wa kilometa 45 imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2014 kwa gharama ya Shilingi bilioni 43.62;

Sehemu ya Rudewa – Kilosa yenye urefu wa kilometa 24, ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea na hadi kufikia Machi 2020 ulikuwa umefikia asilimia 18; na

Sehemu ya Kilosa – Mikumi yenye urefu wa kilometa 73, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa hatua hizi zinazoendelea, miaka si mingi barabara hii itakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizi, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Nchini itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara yote kuhakikisha kuwa inapitika majira yote.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nianze kwa kumwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza hotuba ya Wizara yetu naomba taarifa yote hii iingie kwenye ikiwa kama ni kumbukumbu sahihi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mwaka 2019/2020 na Malengo ya Ofisi ya Mwaka 2020/2021, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na baraka kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2020/2021 mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuiteua kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa kitaifa ya maendeleo, mafanikio haya ni dalili tosha kwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo tuliyoyaweka katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano 2016-2021 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kuifanya nchi yetu kuwa ni kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo aliyotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na kudumisha Muungano wetu pamoja na kuhifadhi na kusimamia mazingira nchini. Vilevile, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi cha uongozi wako. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. Vilevile, nampongeza Katibu wa Bunge na watumishi wa Bunge kwa namna wanavyoliendesha Bunge kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naomba nikupongeze wewe na Bunge lako Tukufu kwa uamuzi wa kuendesha shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA. Hali ambayo imepunguza matumizi ya karatasi katika kuandaa taarifa za Bunge zinazowasilishwa na Serikali hapa Bungeni. Hatua hii, inachangia katika juhudi za uhifadhi wa mazingira nchini na kupunguza gharama kwa Serikali za kuandaa na kudurufu taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq na Makamu wake Mheshimiwa Kanali (Mst.) Masoud Ali Khamis; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa; na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kwa kifo cha Mheshimiwa Rashid Akbar aliyekuwa Mbunge wao kilichotokea mwezi Januari, 2020. Vilevile, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, kwa kifo cha Ndugu Ali Abdulrazack Mfuruki aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira kilichotokea mwezi Desemba, 2019. Aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kupoteza ndugu zao na mali kutokana na

ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo hapo juu ya utangulizi sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Kipindi cha Mwaka 2019/2020 na Malengo ya Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020; Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2019/2020; Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia Mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020 jumla ya Sh.7,855,093,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo Sh.6,734,965,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.1,120,128,000.00 zilikuwa za Mishahara. Kwa upande wa Fungu 31 Sh.29,066,289.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 9.84 ni Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 19.21 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa kutumika hadi Machi, 2019; Hadi kufikia Aprili, 2020, jumla ya shilingi bilioni 7.5 zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, s Sh.5,051,000,000 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na asilimia ya 74.99 ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na Sh.696,636,000.00 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 62.19 ya fedha za Mishahara zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 2 Aprili, 2020 Fungu 31 lilipokea jumla ya Sh.3,057,945,693.00 fedha za matumizi mengineyo sawa na asilimia 71.4 ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa. Aidha, kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 1.7 ni fedha za Ruzuku kwa Baraza la Taifa la

Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 60.6 ya fedha zilizoidhinishwa. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 1.9 zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi sawa na asilimia 70 ya fedha za mishahara zilizoidhinishwa. Aidha, shilingi bilioni 2.92 zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 15.2 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Muungano; katika mwaka 2019/2020 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuratibu kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ; kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii pamoja na kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ya pande mbili za Muungano; na Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudumisha Muungano na Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zenye majukumu yanayoshabihiana. Nikuhakikishie na kulihakikishia Bunge zima hali ya Muungano Tanzania katika mahusiano yetu ni mazuri na sasa hivi kuna nchi zinatoka nchi nyingine kuja kujifunza Tanzania ni namna gani Muungano wetu umeweza kudumu kwa amani na kwa furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi na Usimamizi Endelevu wa Mazingira; katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya usimamizi wa mazingira kupitia vyombo vya habari; na Kuandaa, kukamilisha na kuanza kutekeleza mikakati. Kazi nyingine zilizofanyika katika kipindi hiki ni kutoa mafunzo ya mwongozo wa tathmini ya mazingira kimkakati nchini kwa Maafisa Mazingira wa Mikoa na Wilaya nchi nzima; Kufanya mapitio ya Kanuni za Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka 2009; Kuandaa Kanuni na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2020; Kukamilisha taarifa tatu za Hali ya Mazingira nchini ya Mwaka 2019 na kuanza kusambaza kwa wadau; Kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti; na Kukamilisha na kuridhiwa kuendelea kutekeleza mikataba na itafaki za kimataifa za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti udanganyifu katika usafirishaji wa taka hatarishi, tutaimarisha utaratibu ambao Afisa Mkaguzi atasaini kwenye taarifa yake na kuweka idadi ya namba ya kasha pamoja na kuwa na fomu ya uhalali wa mzigo kabla ya kutolewa kwa kibali ambacho kitasainiwa na waziri mwenye dhamana ya masuala ya mazingira. Tumegundua kuna watu wakipewa vibali hivi badala ya kupeleka mizigo waliyokaguliwa wanapeleka mizigo mbadala, kwa hiyo sasa tunadhhibiti kwa kila kibali kitatoka na kudhibiti uchafuzi na wizi wa miundombinu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020, Baraza limetekeleza kazi zifuatazo: Kufanya ukaguzi katika miradi 1,132; Katika jitihada za kuongeza ufanisi katika masuala ya tathmini ya athari za mazingira Baraza liko katika hatua ya mwisho kukamilisha mfumo wa kielektroniki kwa kusajili miradi kwa njia ya mtandao . Mfumo huu utawezesha wawekezaji kusajili na kufuatilia hatua zilizofikiwa kuhusu miradi yao bila kulazimika kufika kwenye Ofisi za Baraza, hivyo kupunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa usajili wa miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2020 nilifanya ziara katika Mgodini wa tulikwenda Buhemba, Silosimba, Nyarugusu na Mgusu iliyopo Mkoani Mara kwa lengo la ufuatiliaji, usikilizaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika shughuli za uchimbaji wa madini. Aidha, tulipata fursa ya kutoa elimu kuhusu madhara na matumizi ya kemikali ya zebaki katika shughuli za uchenjuaaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilipata fursa kutembelea viwanda vinavyozalisha mifuko mbadala ya () ya ambacho kiko Mwanza pamoja na Serikali inataka urafiki na wawekezaji pamoja na viwanda kuwa vinachangia pato la ndani na kuchangia ajira, lakini viwanda hivyo havina budi kutimiza masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kina ya fedha zilizopokelewa na shughuli zilizofanyika zimefafanuliwa kwenye ukurasa wa 10 hadi ukurasa wa 71 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Maombi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2020/2021. Katika kuimarisha Muungano kwa mwaka 2020/2021, ofisi imepanga kutekeleza majukumu na malengo yafuatayo: Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMT na SMZ; Kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufuatilia utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano; Kuhakikisha gawio la asilimia 4.5 ya fedha za misaada ya kibajeti, faida Benki Kuu, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na inapelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii; na kuratibu masuala yasiyo ya muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara, Taasisi za SMT, SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi na Usimamizi Endelevu wa Mazingira; katika jitihada za kuhakikisha kuna hifadhi endelevu ya mazingira ya mwaka 2020/2021 ofisi imepanga kutekeleza yafuatayo: Kuendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira; Kuandaa na kukamilisha na kuanza kutekeleza mikakati mpango na miongozo ya uhifadhi ya usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kukamilisha kufanya mapitio ya Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2019/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwa mamlaka husika kuhakikisha kuwa nyaya za umeme zinazokuwa na ubora ili kuzuia kuvuja kwa kemikali ya na kusababisha uchafuzi wa mazingira na hasara kiuchumi kwa Taifa. Aidha, uwepo wa mabomba ya gesi, mabomba ya maji machafu na vifaa vingine vinavyoingizwa nchini vikiwa chini ya viwango husababisha uchafuzi wa mazingira. Hivyo natoa rai kwa mamlaka husika

kudhibiti viwango vya ubora na ikibidi kuweka viwango vya juu zaidi ili kulinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nashauri mamlaka husika kuangalia upya usafirishaji wa vyuma chakavu ambavyo vingetumika kama malighafi katika viwanda vya ndani na kulinda miundombinu yetu kama reli, nyaya za umeme na mifumo ya maji taka. Nashauri malighafi hizi zitumike na viwanda vya ndani vinavyotoa ajira kwa Watanzania na kulipa kodi ya Serikali na hivyo kuboresha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la uchafuzi wa mazingira unaotokana na moshi unaotolewa na vyombo vya moto. Ni wakati muafaka sasa kuona utaratibu wa vyombo vyote vya moto kupimwa viwango vya moshi unaotoka kwenye vyombo hivyo (ili kudhibiti tatizo hili. Ofisi yangu kwa kushirikiana na mamlaka zingine itaandaa utaratibu wa kupima moshi unaotolewa na vyombo vya moto kwa utaratibu kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira. Baraza limepanga pamoja na mambo mengine kuendelea na kampeni ya elimu ya mazingira kwa umma na kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi na shughuli mbalimbali zikiwemo kuimarisha usimamizi wa taka ngumu. Taarifa ya kina ya malengo na shughuli zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka 2020/2021 zimeonyeshwa kwenye ibara ya 71 - 84 wa kitabu changu cha hotuba kilichowasilishwa mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho na shukrani. Jana kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika alisema maneno kidogo ya sintofahamu. Unapona mtu anatoka droo anafurahi ujue huyo amekwisha. Ni kama vile mtu anachekelea ndizi mkungu si wake

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni ya Muungano ambao una umuhimu wa pekee wa Taifa na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika

kudumisha amani, mshikamano na usalama wa nchi yetu. Mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 56 tangu kuasisiwa kwake. Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri na hakuna changamoto yoyote inaweza kutufarakanisha, kututenganisha, wala kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Dkt. Shein, kwa pamoja kuondoa suala la kwenye umeme na kuonesha kuwa dhahiri Muungano huu ni wa undungu, upenzi na wa maelewano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu na Serikali kwa ujumla itaendelea kufanyia kazi mambo yote yanayoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala yanayohusu Muungano na kutoa elimu kuhusu Muungano ili uendeleo kuimarika. Hivyo, nawapongeza viongozi wetu Mheshimiwa viongozi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uongozi wao mahiri na maelekezo wanayotupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo endelevu na uchumi wa viwanda hayawezi kupatikana bila kutunza na kuhifadhi mazingira. Kutokana na umuhimu huu ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu yanalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuisitiza kuwa Serikali inathamini wawekezaji kwa kuwa wana mchango

mkubwa katika pato la taifa kwa kutoa ajira na kupunguza umaskini nchini. Hivyo, natoa rai kwa wawekezaji kutunza mazingira kwa kuzingatia sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ili kuwa na maendeleo endelevu nchini

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2020/2021, Ofisi itaendelea kutoa miongozo katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira kwa kuangalia mifumo ya ikolojia, uzalishaji mali na uchumi na matumizi ya rasilimali asili. Vilevile, Ofisi imejipanga kuipa elimu ya mazingira kipaumbele kwa jamii ili kuhakikisha mazingira yanalindwa na kutunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo aliyotupatia kuhusu majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake makini unaotuwezesha kutelekeza majukumu yetu. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mhandisi Joseph K. Malongo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; Balozi Joseph E. Sokoine, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira, Prof. Mhandisi Esnati Chagguna na wajumbe wa Bodi; Dkt. Samuel Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi la Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara, Vitengo na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na Baraza. Pia nawashukuru wale wote waliotuwezesha

kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani za dhati kwa washirika wetu wote wa maendeleo kwa namna tunavyoshirikiana nao katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Aidha, nawashukuru kwa mchango na misaada yao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolenga kuhifadhi na kulinda mazingira yetu. Washirika wote wa maendeleo namewatambua kwa majina yao katika kitabu changu cha hotuba cha bajeti katika ukurasa wa 87 hadi 88.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha. Ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha jumla ya Sh.27,990,155,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 26 - Makamu wa Rais. Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Sh.8,759,191,000 ikiwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2020/2021. Kati ya fedha hizi, Sh.1,024,226,000 ni fedha za Mishahara ya Watumishi na Sh.7,734,965,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(ii) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika fungu hili, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe jumla ya Sh.19,230,964,000. Kati ya fedha hizo, jumla ya Sh.11,581,534,000 ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Sh.7,649,430,000 fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Sh. 6,634,482,000 fedha za Mishahara na Sh. 4,947,052,000 fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Mishahara zinajumuisha kiasi cha Sh.3,083,994,000 Mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kiasi cha Sh.3,550,488,000.00 ni Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha fedha za Ndani Sh.1,000,000,000 na Sh.6,649,430,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya
Makamu wa Rais Muungano na Mazingira*

DIRA

DHIMA

MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS

(i)

(iii)

(iv)

(v)


(vi)

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2019/20; na Malengo ya Ofisi ya mwaka 2020/21, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2020/21.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na baraka kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2020/21 mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee ninamshukuru kwa dhati **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniadini na kunitaua kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira.

Pia, ninapenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya maendeleo. Mafanikio hayo ni dalili tosha kuwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo tuliyojiwekea katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuifanya nchi yetu kuwa ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.



3. Mheshimiwa Spika, kwa dhati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi Mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa ya kuudumisha Muungano wetu pamoja na kuhifadhi na kusimamia Mazingira nchini. Vilevile, ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuenzi na kuudumisha Muungano wetu.



4. Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kiseru katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2020/21. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira.

5. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya katika kipindi cha uongozi wako. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Wenyevitani wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu.

6. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nikupongeze wewe na Bunge lako Tukufu kwa uamuzi wa kuendesha shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA. Hali hii imepunguza matumizi ya karatasi katika kuandaa taarifa za Bunge zinazowasilishwa na Serikali hapa Bungeni. Hatua hii, inachangia katika juhudi za uhifadhi wa mazingira nchini na kupunguza gharama kwa Serikali za kudurufu taarifa hizo.

7. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq (Mb.), Makamu wake Mhe. Kanali (Mst.) Masoud Ali Khamis (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb.), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/20 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2020/21.

8. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa marafiki na wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini, kwa kifo cha Mheshimiwa Rashid Akibar aliyekuwa Mbunge wao kilichotokea mwezi Januari 2020. Vilevile, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, kwa kifo cha Ndugu Ali Abdulrazack Mufuruki aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira, kilichotokea mwezi Desemba, 2019. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutokana na ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini.

Ninaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

9. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi

ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2019/20 na malengo ya mwaka 2020/21.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20

Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2019/20

10. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Fungu 26

11. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, jumla ya Shilingi **7,855,093,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Shilingi **6,734,965,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **1,120,128,000.00** zilikuwa za Mishahara.

Fungu 31

12. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 31, Shilingi **29,066,289,442.00** ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi **9,847,374,000.00** zilikuwa za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **19,218,915,442.00** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha Shilingi **2,808,957,000.00** Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Fedha Zilizopokelewa Hadi Aprili, 2020 Fungu 26

13. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia 02 Aprili, 2020, jumla ya Shilingi **7,533,225,153.00** zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya **Fungu**

26. Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,051,222,999.00** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia ya **74.99** ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na Shilingi **696,636,000.00** kwa ajili ya Mishahara, sawa na asilimia **62.19** ya fedha za Mishahara zilizoidhinishwa.

Fungu 31

14. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia 02 Aprili, 2020 Fungu 31 lilipokea jumla ya Shilingi **3,057,945,693.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na asilimia **71.4** ya fedha za matumizi ya mengineyo zilizoidhinishwa. Aidha, jumla ya Shilingi **1,704,523,905.00** ni Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zilizopokelewa ambazo ni sawa na asilimia **60.6** ya fedha zilizoidhinishwa. Vilevile, kiasi cha Shilingi **1,966,966,000.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, sawa na asilimia **70** ya fedha za mishahara zilizoidhinishwa. Aidha, Shilingi **2,929,865,814.00** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia **15.2** ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

15. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17– 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (2015– 2020); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063

Malengo ya Maendeleo Endelevu ()
) ; na Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

MASUALA YA MUUNGANO

16. Mheshimiwa Spika, mwaka huu, Muungano wetu unatimiza miaka 56. Muungano huu umeendelea kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na kisiasa yanayonufaisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Ni dhahiri kuwa Muungano wetu umeendelea kuimarika na umekuwa nyenzo na utambulisho muhimu wa Taifa letu. Ili kudumisha na kuulinda Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekeleza majukumu ya msingi ya kuratibu utekelezaji wa masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

17. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, kazi zilizotekelezwa ni:- Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii pamoja na kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ya pande mbili za Muungano; Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudumisha Muungano; na Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zenye majukumu yanayoshabihiana.

Utatuzi wa changamoto katika utekelezaji wa Masuala ya Muungano

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 Ofisi iliratibu kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kilichofanyika tarehe 2 Desemba, 2019 - Zanzibar. Kikao hiki kilitanguliwa na vikao vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ vya tarehe 20 Septemba, 2019, tarehe 25 Novemba, 2019 na tarehe 13 Februari, 2020. Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na: Uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu; Hoja za Fedha; na Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Lengo la Vikao hivi ni kukuza mashirikiano ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu ili kuboresha ufanisi.



Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii

I. Miradi ya Maendeleo

19. Mheshimiwa Spika, Ofisi ilifanya ufuatiliaji wa Miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Ufuatiliaji huo ulihusisha kutembelea miradi minne (4) iliyopo katika Wilaya za Chakechake na Wete Kisiwani Pemba – mwezi Desemba, 2019. Miradi iliyotembelewa katika Wilaya ya Wete ni Mradi wa Ujenzi wa vyumba vinne (4) vya madarasa katika Skuli ya Maandalizi Kangagani na Mradi wa Ujenzi wa Kisima Wingwi Mjananza. Miradi iliyotembelewa katika Wilaya ya Chakechake ni Mradi wa Matengenezo ya vyumba vitano (5) vya madarasa katika Skuli ya Msingi ya Vikunguni na Mradi wa Kufikisha Umeme katika Kijiji cha Pujini (Tondooni).

Aidha, Ofisi imefuatilia utekelezaji wa miradi na programu za pamoja zinazotekelezwa pande mbili za Muungano. Programu na Miradi hiyo ni pamoja na:- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (MIVARF) na Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi

20. Mheshimiwa Spika, Ofisi iliratibu na kufanya kikao kazi cha Waratibu wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano tarehe 31 Oktoba, 2019. Lengo la kikao ni kujenga uelewa wa pamoja wa utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji.



Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

21. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeratibu gawio la Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Zanzibar na

- Hadi kufikia Februari, 2020, jumla ya Shilingi bilioni 15.40 zimepelekwa SMZ na mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: - Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo – Shilingi bilioni 1.40; na PAYE – Shilingi bilioni 14.00.

Kuimarisha Ushirikiano wa Masuala yasiyo ya Muungano

22. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuhamasisha sekta zisizo za Muungano za SMT na SMZ kukutana na kujadili masuala yanayohusu sekta zao na kubadilishana uzoefu, utaalum na wataalam ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano. Hadi kufikia tarehe 5 Machi, 2020, vikao kumi na tatu (13) vya Ushirikiano vya kissekta vilifanyika, Wizara zilizofanya vikao ni:- Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT) na Habari, Utalii na Mambo ya Kale (SMZ) tarehe 8 Oktoba, 2019; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (SMT) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (SMZ)

vikao viwili (2) tarehe 29 Julai, 2019 na tarehe 29 Agosti, 2019; Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT) na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (SMZ) tarehe 16 Septemba, 2019; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (SMT) na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (SMZ) vikao vinne (4) tarehe 26 – 27 Novemba, 2019, tarehe 16 Septemba, 2019, tarehe 6 Desemba, 2019 na tarehe 4 Februari, 2020.

23. Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine zilizofanya vikao ni:- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (SMT) na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) tarehe 18 Novemba, 2019; Wizara ya Katiba na Sheria (SMT) na Wizara ya Katiba na Sheria (SMZ) vikao viwili (2) tarehe 8 Julai, 2019 na tarehe 29 Julai, 2019; na Wizara ya Viwanda na Biashara (SMT) na Wizara ya Viwanda na Biashara (SMZ) tarehe 17 Julai, 2019; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (SMT) na Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale (SMZ) tarehe 2 – 4 Machi, 2020; na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (SMZ) na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati (SMZ) tarehe 27 Januari, 2020.

Kutoa Elimu ya Muungano kwa Umma

24. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendee kutoa elimu ya Muungano kupitia redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii. Ofisi iliandaa na kufanya kikao kazi cha Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara zote za SMT tarehe 17 Septemba, 2019 kwa lengo la kujadili uratibu wa Masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano na upatikanaji wa taarifa za utekelezaji kutoka katika Wizara zao. Aidha, Ofisi iliandaa na kushiriki katika ziara ya mafunzo iliyohusisha wanafunzi kutoka Mwanza katika shule inayoitwa ambapo walipata elimu ya Muungano pamoja na kutembelea maeneo ya kihistoria na vivutio vya kiutalii Zanzibar. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 17 - 20 Septemba, 2019 kwa lengo la wanafunzi kujifunza Muungano kwa vitendo, kufahamu faida za Muungano ili kuendelea kuulinda, kuutetea na kuenzi. Aidha, kuelekea miaka 56 ya Muungano wa

Tanganyika na Zanzibar, Ofisi imetoa elimu kwa umma kupitia vipindi vinne (4) vya redio na vipindi vinne (4) vya runinga.



HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEU WA MAZINGIRA

25. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yetu kwa kiasi kikubwa yanategemea matumizi endelevu ya maliasili zilizopo nchini. Kuendelea kuwepo kwa rasilimali hizi ni muhimu kwa ajili ya mahitaji ya sasa na ya vizazi vijavyo. Hata hivyo, Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini ya mwaka 2019 imebainisha kuwepo kwa shughuli za kiuchumi na kijamii zisizo endelevu ambazo zimeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira nchini.

26. Mheshimiwa Spika, uharibifu huu ni pamoja na uharibifu wa ardhi; ukataji wa miti hovyoyote na uharibifu wa misitu, upotevu wa bioanuai, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa mifumo ikolojia ya maji, kupungua kwa ubora na upatikanaji wa maji na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la viumbe vamizi; taka za kielektroniki; taka za kemikali; uchafuzi utokanao na shughuli

za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi; na matumizi ya teknolojia ya uhandisi jeni ambavyo kwa kiasi kikubwa vimechangia uharibifu wa mazingira na kuhatarisha afya ya binadamu na ikolojia kwa ujumla.

27. Mheshimiwa Spika, katika kulinda, kuhifadhi na kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka 2019/20, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo; -

Elimu kwa Umma Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira

28. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti na pia kwa kutumia maadhimisho ya kitaifa na kimataifa. Elimu hii imetolewa katika mikoa ya Simiyu, Geita, Mwanza, Shinyanga, Singida, Dodoma, Morogoro, Tabora, Pwani, Tanga na Dar es Salaam. Aidha, wadau mbalimbali wakiwemo wabunge wameelimishwa kuhusu hifadhi ya mazingira kupitia semina, warsha, mikutano ya hadhara na mitandao ya kijamii.

29. Mheshimiwa Spika, elimu iliyotolewa ilihusu masuala yafuatayo: Katazo la matumizi ya mifuko ya Plastiki; Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa; Usimamizi wa Kemikali na Taka; Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame; Mabadiliko ya Tabianchi; Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu; Mkatiba wa Minamata kuhusu Zebaki; Itifaki ya SADC ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu; Marekebisho ya Kigali katika Itifaki ya Montreal kuhusu Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki hii; na Itifaki ya Ziada ya Nagoya-Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madharayanayoweza kutokea kutokana na Matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.



Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji

30. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi inaendelea na mapitio ya Sera ya Mazingira ya Taifa ya Mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeandaa rasimu ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Mkakati wake wa utekelezaji. Rasimu hiyo inatarajiwa kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi stahiki.

Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira na Mikakati ya Kuhifadhi Mazingira

31. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, Ofisi ina jukumu la kuandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira kila baada ya miaka mitano ambao utatumiwa na Serikali za Mitaa katika kuandaa Mipango ya Mazingira katika maeneo yao. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imepitia na kuandaa

Rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2019 – 2023 kufuatia kuisha muda wa Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2013 - 2018. Mpango Kazi huu unatarajiwa kukamilika mara baada ya Sera ya Taifa ya Mazingira kupitishwa.

Vilevile katika kipindi hiki, Ofisi imekamilisha mapitio ya Mkakati wa Hatua za Haraka za Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2019; na Mkakati wa Hatua za Haraka za Hifadhi ya Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2019.

Mkakati na Mpango-Kazi wa Taifa wa Kukabiliana na Viumbe Vamizi (Invasive Species)

32. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua zinazochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa Mkakati na Mpango-Kazi wa Taifa wa kukabiliana na changamoto ya Viumbe Vamizi nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imekamilisha maandalizi ya Mkakati na Mpango-Kazi huu ambao pamoja na mambo mengine umeainisha hatua za kuchukua na majukumu ya kila mdau katika kukabiliana na changamoto hii.

Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)

33. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kutoa mafunzo ya Mwongozo wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati nchini kwa Maafisa Mazingira wa Mikoa na Wilaya Nchi Nzima. Hadi sasa, mafunzo hayo yamefanyika katika Kanda nne (4) ambazo ni: Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam, Morogoro, Pwani); Kanda ya Kati (Dodoma, Singida); Kanda ya Ziwa (Mwanza, Mara, Simiyu, Geita, Shinyanga, Kagera); na Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga). Mafunzo haya yanahusu dhana na muktadha wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati; mchakato wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati; ushirikishwaji wa wadau katika tathmini; na mchakato wa kuidhinisha Ripoti ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, mafunzo yametolewa kwa Maafisa Mazingira wapatao 150. Aidha, mafunzo haya yaliendeshwa sambamba na kusambaza nakala 450 za mwongozo kwa wadau katika Kanda husika. Katika kipindi hiki, pia Ofisi imefanya mapitio

ya Taarifa tatu (3) za Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) ikijumuisha Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Mwalimu Nyerere katika Bonde la Mto Rufiji, Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Jiji la Dodoma na Sera na Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini ya Mwaka 2019

34. Mheshimiwa Spika, mwaka jana pia nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuandaa rasimu ya Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imewasilisha Taarifa hii Bungeni kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. Taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, imeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini licha ya juhudi zinazofanywa na Serikali na wadau mbalimbali. Hii inatokana na: kutozingatiwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake katika ngazi mbalimbali; Uelewa mdogo wa wananchi; matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali; na kuibuka kwa changamoto mpya za kimazingira. Ofisi imechapisha taarifa hiyo na kuisambaza kwa wadau.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

35. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea na Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 5 Juni ya kila mwaka. Maadhimisho ya siku hii ni kutoa fursa ya kukuza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya mazingira na kuhamasisha jamii kuchukua hatua za makusudi za kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa maisha ya sasa na baadae. Kwa mwaka 2019/20, maadhimisho hayo kitaifa yatafanyika mkoani Lindi na Kauli Mbiu ya Kitaifa ya Maadhimisho hayo itakuwa ***Tutunze Mazingira: Tukabiliane na Mabadiliko ya Tabianchi***". Aidha, katika maadhimisho ya mwaka huu, shughuli mbalimbali za kuhamasisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira zitafanyika ikiwa ni pamoja na: kuendesha Kongamano la Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi; kufanya maonesho ya shughuli za uhifadhi na utunzaji wa mazingira kutoka kwa wadau; na utoaji wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi Mazingira.

Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira

36. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi inaendelea na uratibu wa mchakato wa upatikanaji wa washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ambao kwa mwaka huu ushiriki wa wadau katika mashindano hayo umeongezeka kwa kuweka tuzo katika masuala ya uzalishaji endelevu viwandani; matumizi ya nishati mbadala ya kupikia; uchimbaji endelevu wa madini; kilimo endelevu; usimamizi wa taka; ufugaji endelevu, na Afya na Usafi wa Mazingira. Aidha, Tuzo hii inategemewa kutolewa katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani inayotarajiwa kufanyika tarehe 05 Juni, 2020 mkoani Lindi.

Mwongozo wa Matumizi ya Eneo la Hifadhi la Mita 60 kutoka kwenye Vyanzo vya Maji

37. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inazuia shughuli za kudumu katika eneo la hifadhi ya mita 60 kutoka vyanzo vya maji na inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mazingira kuandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa eneo hilo. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Mita 60 wa Kuhifadhi Vyanzo vya Maji. Rasimu hii inaainisha matumizi mbalimbali endelevu ya eneo la mita 60 kutoka vyanzo vya maji. Ofisi inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuboresha Rasimu ya Mwongozo.

Kampeni ya Upandaji Miti

38. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayoelekeza kila Halmashauri ya Wilaya kutenga maeneo na kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Ofisi imefuatilia utekelezaji wa kampeni hii na kubaini kuwa jumla ya miti milioni **209.7** ilipandwa na miti iliyostawi ni milioni **153.2**, sawa na asilimia **72.6** ya miti iliyopandwa. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimebainisha changamoto zinazo kwamisha kufikiwa kwa malengo. Changamoto hizo ni pamoja na: upandaji wa miti isiyo rafiki katika baadhi ya maeneo na utunzaji hafifu wa miti iliyopandwa na uhaba

wa upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo. Katika kukabiliana na changamoto hizi, pamoja na mambo mengine Ofisi imefanya mapitio ya Mkakati wa kuhifadhi vyanzo vya maji na kupanda miti ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza kampeni hii.



39. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kufuatilia na kuhamasisha utekelezaji wa kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. Kampeni hiyo inatekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC). Katika kutekeleza kampeni hii, miti ipatayo 40,547 imepandwa na kuendelea kutunzwa katika kipindi hiki. Aidha, wadau kutoka Shirika la Hifadhi ya Mazingira Duniani

) pamoja na wameunga mkono juhudi hizi za Serikali kwa kuwezesha na kushiriki katika utekelezaji wa Kampeni hiyo. Ninatoa wito kwa wadau wengine wa sekta binafsi na mashirika mengine kuiga mfano huo na kuwezesha utekelezaji endelevu wa kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Matumizi ya Mifuko ya Plastiki

40. Mheshimiwa Spika, kufuatia Tamko la Serikali la Kupiga Marufuku Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki nchini kuanzia tarehe 1 Juni, 2019, kupitia Gazeti la Serikali Na.394 la tarehe 17 Mei, 2019, Ofisi imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa katazo hilo katika ngazi ya Kitaifa na Serikali za Mitaa.

41. Mheshimiwa Spika, vilevile katika kutekeleza katazo hilo, Ofisi ilitoa elimu kwa umma kupitia vipindi 113 vya redio na runinga; makala 20 kwenye magazeti; mabango 50; video fupi 30; na mitandao ya kijamii. Vilevile, semina mbili (2) kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na semina moja (1) kwa wana habari ziliendeshwa Sanjari na kutoa semina, warsha mbili (2) ziliandaliwa kwa maafisa mazingira wa mikoa 25 ya Tanzania Bara kwa lengo la kusimamia na kuhamasisha umma kuhusu utekelezaji wa katazo.

42. Mheshimiwa Spika, Ofisi imehamasisha wazalishaji wa mifuko mbadala kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya watumiaji ambapo hadi sasa kuna jumla ya viwanda 26 nchini ambavyo vinazalisha jumla ya tani 742.5 kwa mwezi. Aidha, jumla ya ajira za kudumu 365 na ajira za muda 983 zimezalishwa katika viwanda hivyo. Vilevile, takriban watu 50,000 wanajihusisha katika usambazaji wa mifuko hiyo.

43. Mheshimiwa Spika, katika ufuatiliaji wa Katazo hili, jumla ya tani 259.2 za mifuko ya plastiki zilikusanywa, kati ya hizo tani 86.7 zilirejelezwa kwenye viwanda mbalimbali, na tani 172.5 zilliteketezwa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto wakati wa utekelezaji wa katazo hilo ikiwemo kubadilisha matumizi ya vifungashio vya plastiki kuwa vibebeo vya bidhaa na uingizaji na uzalishaji wa mifuko mbadala isiyokidhi viwango (70GSM) vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania. Katika kukabiliana na changamoto hizi, jumla ya viwanda vitatu (3) vilibainika kuzalisha mifuko mbadala isiyokidhi viwango, hivyo kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kutozwa faini na kuzuiwa kuendelea na uzalishaji

hadi watakapokidhi viwango vinavyotakiwa. Aidha, jumla ya maduka Saba (7) yalikutwa na mifuko isiyokidhi viwango na kuchukuliwa hatua za kisheria. Maduka hayo yalipatika katika mikoa ya Dodoma matano (5), Arusha moja (1) na Kigoma moja (1). Vilevile, wauzaji wadogo 10 katika mkoa wa Kagera walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuzuiwa kuendelea na uuzaji wa mifuko hiyo.

Usimamizi wa Taka Hatarishi

44. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa taka hatarishi nchini umekuwa unaongezeka mwaka hadi mwaka. Taka hizi zinajumuisha mafuta machafu kutoka kwenye mitambo na vyombo vya moto, betri chakavu, chuma chakavu, matairi yaliyotumika, taka za kemikali na taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki na umeme. Ili kudhibiti taka hizi na kulinda afya ya binadamu na mazingira, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imekuwa inatoa vibali kwa makampuni na watu binafsi wanaojihusisha na kukusanya, kurejeleza na kusafirisha taka hatarishi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni za Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka 2019. Aidha, kutokana na kasi kubwa ya kuongezeka kwa taka za kielektroniki, Ofisi imeandaa Kanuni mahsusi za Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2020 ili kuimarisha usimamizi wa taka hizo hapa nchini.

45. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imefanya mapitio ya Kanuni za Usimamizi za Taka Hatarishi za Mwaka 2009 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taka hatarishi nchini ambao pamoja na mambo mengine vibali vya taka hatarishi vitatolewa kwa njia ya kielektroniki. Kufuatia maboresho hayo, vibali 25 vya taka hatarishi vimetolewa. Kati ya vibali hivyo 20 ni vya kukusanya, kusafirisha na kurejeleza hapa nchini na vibali vitano (5) ni vya kuingiza na kusafirisha nje ya nchi. Katika kipindi hiki, takribani tani 233,810 za taka hatarishi zimekusanywa na kurejelezwa.

Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility – GEF)

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa nchini. Kwa mujibu wa taratibu za GEF, nchi zinazoendelea ambazo ni wanachama wa mikataba ya kimataifa ya hifadhi ya mazingira hutengewa fedha kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza miradi ya mazingira. Utaratibu hufanyika kwa kila kipindi cha miaka minne (GEF- Katika Awamu ya Saba (7) ya GEF (2019 – 2023) nchi yetu imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 24 ambapo asilimia 2 ya fedha hizo zitatumika kufadhili programu ya miradi midogo inayoandaliwa na asasi za kiraia. Aidha, upatikanaji wa fedha hizi, unategemea ubora wa maandiko ya miradi.

47. Mheshimiwa Spika, kipindi hiki, Ofisi kwa kushirikiana na wadau inaandaa maandiko ya miradi mitano (5) kwa ajili ya ufadhili wa GEF, ikiwa ni pamoja na:

i.

Mradi huu una thamani ya dola za Marekani milioni **5.5** na utatekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii katika wilaya za Kilombero (Morogoro), na Kaskazini A na Kaskazini B (Zanzibar);

Mradi huu una thamani ya dola za Marekani **7.0** na utatekelezwa na Jiji la Dodoma;

Mradi huu una thamani ya dola Marekani milioni **5.5** na utatekelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika wilaya za Kaliua (Tabora) na Mlele (Katavi);

Mradi huu una thamani ya dola za Marekani milioni **4.0** na utatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi; na

v. Programu ya Ufadhili wa Miradi Midogo yenye thamani ya dola za Marekani milioni **2.0**

Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund – GCF)

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuhamasisha Taasisi za Umma na Sekta Binafsi hapa nchini kuomba ithibati () ya kusimamia fedha za miradi ya mabadiliko ya tabianchi zinazotolewa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi. Kupitia uhamasishaji huo Benki ya CRDB imepata ithibati mwezi Novemba, 2019, hivyo kuwa na uwezo kusimamia fedha za miradi kwa ufadhili wa Mfuko huo. Hatua hii itasaidia kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapa nchini.

49. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Benki ya CRDB kwa mafanikio haya ambayo yatasaidia upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa miradi inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapa nchini. Natoa wito kwa wadau kutumia fursa hii kushirikiana na Benki ya CRDB kuandaa na kutekeleza miradi itakayosaidia kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Uratibu na Utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Mazingira

50. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Washirika wa Maendeleo, imeratibu na kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya mazingira ifuatavyo: -

i) Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu
51. Mheshimiwa spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ilikuwa inaratibu mchakato wa kuridhia Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu. Napenda kukutaarifu kuwa Ofisi ilikamilisha mchakato huo na Bunge lako Tukufu liliridhia Itifaki hiyo tarehe 13 Novemba, 2019. Kwa kuridhia Itifaki hii, nchi yetu itanufaika na usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka baina ya nchi wanachama.



Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na Makubaliano ya Paris

52. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, na Makubaliano ya Paris nchini. Katika kipindi hiki, Ofisi imeandaa Mchango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

) na Mpango wake wa Utekelezaji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Makubaliano ya Paris. Vilevile,

katika kipindi hiki, Ofisi inafanya mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2012 – 2018) na Mpango wa Taifa wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi. Sambamba na mapitio hayo, Ofisi kwa kushirikiana na wadau inaandaa Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.



53. Mheshimiwa Spika, chini ya Mkataba huu, Ofisi inaendelea kutekeleza miradi miwili (2) ya kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi. Miradi hiyo ni: -

a) Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Hifadhi ya Ikolojia. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A, (Kaskazini Unguja) kwa gharama ya Shilingi **bilioni 17.4** kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2017 chini ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni: kufanya utafiti na tathmini ya athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya mradi; Kuandaa Mfumo wa Kusimamia na Kueneza Maarifa ya Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi; kutoa mafunzo kwa Viongozi na

Wataalam 76 kutoka Wizara za Kisekta, Taasisi za Elimu ya juu, Asasi za Kiraia na Sekta binafsi kuhusu namna ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya Ikolojia; na kuandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini shirikishi kuhusu huduma za mifumo ikolojia; na kutoa mafunzo ya utengenezaji na matumizi ya Majiko banifu kwa wananchi kutoka Wilaya za Kishapu (40) na Simanjiro (42).

b) Mradi wa Kusaidia Kujenga Uwezo wa Taasisi na J a m i i Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Maeneo ya Kaskazini mwa Nchi Unaotekelezwa katika wilaya za Mwangi na Same (Kilimanjaro). Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya shilingi **bilioni 1.2** chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) katika kipindi cha miaka miwili kuanzia 2018. Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni: ukarabati wa mita 350 kati ya 1,800 za mfereji wa umwagiliaji katika Kijiji cha Mabilioni (Same); kutoa mafunzo kwa wanakijiji 30 kuhusu kilimo endelevu cha umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni (Same); na kutoa mafunzo kwa wanakijiji 30 kuhusu matumizi endelevu ya maji katika Vijiji vya Jipe, Makuyuni na Kambi ya Simba; na kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa mradi.

54. Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi inayoendelea kutekelezwa chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, maandiko ya miradi mitatu Mabadiliko ya Tabianchi, maandiko ya miradi mitatu (3) yapo katika hatua mbalimbali ya kukamilishwa. Maandiko haya ni: Mradi wa Utayari wa Nchi Kuimarisha Uwezo wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Uandaaji Wa Programu za Nchi Kuhusu Masuala ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi

Mradi wa Kuhuisha Masuala ya
Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango ya
Maendeleo ya Nchi

Mradi wa Kupunguza
Uzalishaji wa Gesijoto katika Sekta ya Misititu (

REDD+) unaolenga kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali katika kusimamia masuala ya hewa ukaa.

ii) Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Shughuli zilizofanyika katika kipindi hiki ni: Kuweka malengo ya kupunguza uharibifu wa ardhi

ifikapo mwaka 2030. Ili kufikia malengo hayo, kazi zilizoanza kufanyika ni pamoja na: Kubainisha Ukanda wa Maeneo Kame nchini; kufanya mapitio ya Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame; na Kuandaa maandiko mawili (2) ya miradi na kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Mkataba. Maandiko hayo ni: - Programu ya Utekelezaji wa Malengo ya Kupunguza Uharibifu wa Ardhi Nchini; na Mradi wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame Chini ya SADC. Vilevile, Ofisi inaratibu mapitio ya Mpango wa Taifa wa Kuhimili Hali ya Jangwa na Ukame kwa ufadhili wa Sekretarieti ya Mkataba.

iii) Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Hifadhi wa Bioanuai. Katika kipindi hiki, Ofisi imeratibu mchakato wa kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya-Kuala Lumpur Kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara Yanayoweza Kutokea Kutokana na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa. Itifaki hii iliridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 16 Septemba, 2019. Kwa kuridhia Itifaki hii, nchi yetu inaungana na Jumuiya ya Kimataifa katika kusimamia uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

57. Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kutumia wakaguzi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa imeendelea kusimamia na kukagua shughuli za utafiti wa zao la mahindi

lililofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki katika kituo cha utafiti wa kilimo Makutupora, Dodoma. Aidha, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Sambamba na hili, Ofisi imetoa elimu kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa kwa wananchi takriban 1,500 wakati wa maadhimisho ya siku ya wakulima (Nane Nane) katika Kanda za Mashariki, Kati na Ziwa.

58. Mheshimiwa spika, chini ya Mkataba huu, Ofisi inatekeleza mradi wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa unaofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia

) kwa gharama ya Shilingi bilioni

2.9. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na unatarajiwa kukamilika mwaka 2021. Lengo la Mradi ni kuhifadhi mazingira katika Bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya jamii inayozunguka eneo hilo. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Ludewa na Makete (Mkoani Njombe), Kyela (Mkoani Mbeya), Nyasa na Mbinga (Mkoani Ruvuma).

59. Mheshimiwa spika, katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zimetokelezwa: Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika vijiji vitatu (3) katika Halmashauri tano (5) zinazotekeleza mradi; Warsha ya kukuza uelewa wa usimamizi endelevu wa ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa wataalamu 20 kwa Wilaya zote zinazotekeleza Mradi; kuendesha mafunzo kwa vikundi 15 vya wakulima katika maeneo ya mradi kwa lengo la kufikisha elimu kwa jamii inayozunguka eneo la Bonde la Ziwa Nyasa ambapo jumla ya wakulima 200 walielimishwa kuhusu uandaaji wa bustani za miche ya miti; kutengeneza mizinga ya nyuki; na kilimo bora cha ngano, mpunga na korosho. Aidha, jumla ya miti 9,540 ilipandwa kwenye maeneo yaliyoharibiwa.



iv) Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi

60. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi na Itifaki zake. Katika kipindi hiki, Ofisi imeratibu na kusimamia shughuli za awali za utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani Magharibi ya Bahari ya Hindi. Kupitia mpango huu, Tanzania imefanikiwa kupata ufadhili wa miradi ya mfano mitatu (3) kati ya maandiko manne (4) yaliyowasilishwa Sekretarieti ya Mkataba. Miradi iliyopata ufadhili ni kama ifuatavyo:

. Mradi huu unatekelezwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na kutekelezwa katika maeneo ya vyanzo vya maji vya Wilaya ya Mbarali - Bonde la Mto Rufiji. Gharama za Mradi huu ni Dola za Marekani **190,000**.

ii.

. Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na unasimamiwa na Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Gharama za Mradi huu ni Dola za Marekani **102,650**; na

iii.

Mradi huu unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar na unatekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Chakechake – Pemba. Gharama za Mradi huu ni Dola za Marekani **298,500**.

Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

61. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Katika kipindi hiki, Ofisi iliratibu mchakato wakuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal Kuhusu Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Marekebisho haya yaliridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 13 Novemba, 2019. Vilevile, Nchi yetu iliungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Ozoni Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 16 Septemba kila mwaka. Kwa upande wa nchi yetu, maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika Jijini Dar es Salaam kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi Tabaka la Ozoni na udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka hilo.

62. Mheshimiwa Spika, chini ya Itifaki ya Montreal, Ofisi imetekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi katika Kutekeleza Itifaki ya Montreal. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal (

kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) kwa gharama ya Shilingi milioni **213.9** katika kipindi cha miaka miwili (2017 hadi 2019) na umekamilika. Katika kipindi hiki, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendesha mafunzo kwa

maafisa forodha 31 kutoka katika vituo vya mipakani; na maafisa sheria kutoka taasisi tano (5) zinazosimamia Sheria katika kudhibiti uingizwaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba wa Montreal; Kuendesha mafunzo kwa mafundi mchundo 80 kuhusu teknolojia mpya na njia sahihi za kuhudumia vifaa vinavyotumia kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni.

v) Mkataba wa Basel kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka Hatarishi Kati ya Nchi na Nchi

63. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Basel Kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Kati ya Nchi na Nchi. Katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu taratibu za udhibiti wa taka hatarishi na taratibu zinazotakiwa kisheria ili kusafirisha taka nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali ambapo, jumla ya tani 182 zimesafirishwa nje ya nchi.

vi) Mkataba wa Stockholm kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu

64. Mheshimiwa Spika katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeendelea kutekeleza Mkataba wa Stockholm Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu. Chini ya Mkataba huu, Ofisi imeandaa na kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm wa Mwaka 2018 – 2023 unaohusu Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu. Mpango huu unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) kwa gharama ya Shilingi bilioni **1.8** chini ya usimamizi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP).

65. Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu, Ofisi iliratibu zoezi la ukusanyaji wa jumla ya sampuli 553 za mafuta ya transfoma zinazokisiwa kuwa na kemikali ya

ambazo zinadumu katika mazingira kwa muda mrefu na hivyo kuhatarisha afya ya binadamu na mazingira. Sampuli hizi zilikusanywa kutoka katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Pwani, Dar es Salaam

na Morogoro na kwa pande wa Zanzibar, katika Mikoa ya Mjini Magharibi - Unguja na Kaskazini Pemba. Kati ya sampuli zilizokusanywa, sampuli 22 zilibainika kuwa na kemikali ya PCBs. Kemikali hii ni mojawapo ya kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba wa Stockholm ambazo zinapaswa kuondoshwa kwenye matumizi ifikapo mwaka 2025.

66. Mheshimiwa Spika, sanjari na zoezi hili, Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imeendelea kuelimisha jamii kuhusu madhara yatokanayo na kemikali ya PCBs ambapo elimu ilitolewa kwa wananchi takriban 810. Vilevile, wafanyakazi 45 wa TANESCO walipewa mafunzo mahsusi ya namna bora ya kudhibiti kemikali hii. Mafunzo hayo yalitolewa katika mikoa 9 ambayo ilionekana kuwa na kiwango kikubwa cha Transfoma zenye mafuta yenye kemikali aina ya PCBs.



67. Mheshimiwa Spika, Ofisi imekamilisha na kuanza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Kemikali na Taka Hatarishi wa mwaka 2020 – 2025; na kukamilisha Mfumo wa Kieletroniki wa Upatikanaji wa Taarifa za Kemikali na Taka Nchini

Hatua inayoendelea kwa sasa ni kutoa mafunzo kwa wataalam watakaokuwa wanatumia mfumo huo.

68. Mheshimiwa Spika, Ofisi inatekeleza Mpango wa Kimataifa wa Ufuatiliaji wa Madhara ya Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira Kwa Muda Mrefu (2017 – 2020). Kupitia Mpango huu, Ofisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu ilikusanya sampuli 55 za maziwa ya wamama wanaonyonyesha na kutumwa nchini Ujerumani kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu. Sampuli hizi zilichukuliwa katika mikoa ya Mbeya, Pwani, Arusha, Mwanza na Dodoma. Vilevile, sampuli 44 za hewa zilichukuliwa katika Mkoa wa Pwani na kutumwa nchini Uholanzi na Sweden kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kiwango cha kemikali hizi katika hewa. Matokeo ya uchunguzi yatachangia katika uandaaji wa mipango na mikakati ya kukabiliana na athari za kemikali hizi kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kulinda afya ya binadamu.

vii) Mkataba wa Minamata Kuhusu Usimamizi wa Zebaki

69. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Ofisi imeratibu mchakato wa kuridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Usimamizi wa Zebaki. Mkataba huu umeridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 16 Septemba, 2019. Aidha, katika kipindi hiki, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango-Kazi wa Kitaifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu (2020 – 2025). Mpango-Kazi huu unalenga kupunguza matumizi ya Zebaki kwa asilimia 30 ifikapo 2025. Katika kipindi hiki, Ofisi ilitoa elimu kwa umma kuhusu madhara yatokanayo na Zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira katika mikoa ya Mara, Geita, Shinyanga na Singida hususan katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu. Vilevile, Ofisi imeandaa Kanuni za Udhhibiti na Usimamizi wa Zebaki za Mwaka 2020 za Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Zebaki na Viambata Vyake.

70. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2020 nilifanya ziara katika maeneo ya uchimbaji wa madini ya dhahabu katika migodi mikubwa ya Geita na Buhemba, Mara na maeneo ya wachimbaji wadogo ya Sirorisimba, Nyarugusu na Mgusu iliyopo mkoani Mara kwa

lengo la ufuatiliaji wa utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika shughuli za uchimbaji wa madini. Aidha, nilipata fursa ya kutoa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya kemikali ya Zebaki katika shughuli za uchenjuaji wa dhahabu.

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira Sura ya 191

71. Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, kama msimamizi mkuu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, limeendelea kutekeleza majukumu yake ili kuhakikisha sheria hii inazingatiwa ipasavyo katika kutekeleza shughuli za maendeleo hapa nchini.

Ukaguzi wa Maeneo ya Uwekezaji na Mazingira

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Baraza limefanya ukaguzi katika miradi 1,132 ili kutathmini uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira nchini. Kaguzi hizo zilifanyika katika shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo zinaweza kuwa na athari kwa mazingira. Aidha, katika kipindi hiki, Baraza limepokea malalamiko 257 kuhusu uchafuzi wa Mazingira na kufanya ufuatiliaji kuhusu malalamiko hayo.

73. Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanyika ulibaini changamoto za kimazingira zifuatazo: kutiririsha majitaka kwenye vyanzo vya maji na makazi ya watu; Matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali kama misitu ya asili kwa ajili ya kuni na ujenzi; Ukosefu wa mifumo ya kuhifadhi taka ngumu; Uzalishaji wa hewa chafu; Uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala isiyokidhi viwango; Upigaji wa kelele na mitetemo zaidi ya viwango vinavyoruhusiwa kimazingira; na mazingira yasiyo salama katika baadhi ya machinjio mfano ukosefu wa maji safi, vyoo, kuzagaa kwa takangumu na maji taka. Sababu zilizoainishwa na Baraza ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa chanzo cha matatizo haya ni pamoja na kutokuzingatiwa kwa taratibu za Mipango Miji.

74. Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Jeshi la Polisi limetoa maagizo na maelekezo katika kukabiliana na changamoto hizo. Vile vile, Baraza limechukua hatua mbalimbali zikiwemo kufungua mashitaka ya uchafuzi wamazingira, kuelimisha wahusika, kutoa amri za kurekebisha, amri za katazo na kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Amri na makatazo 79 kwa wavunja sheria ya mazingira zimetolewa na kufuatiliwa. Aidha, Baraza linaendelea kusimamia kesi 12 zinazohusu makosa mbalimbali ya kimazingira.

Udhibiti wa Mifuko ya Plastiki

75. Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Jeshi la Polisi na Serikali za Mitaa pamoja na taasisi limeendelea kutekeleza Kanuni za Usimamizi wa Mazingira zilizopiga Marufuku Uingizaji, Uzalishaji, Usafirishaji na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2019. Katika kipindi hiki, Baraza limeendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa katazo hilo kwa kutoa elimu na kusimamia uteketezaji na urejelezaji wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na mifuko mbadala ambayo haijakidhi viwango. Baraza lilikumbana na changamoto ya kuendelea kwa uzalishaji wa vifungashio laini vya plastiki ambavyo hutumika kama mifuko mbadala.



76. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020, Baraza liliendelea na udhibiti wa uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala aina ya isiyokidhi viwango. Jumla ya watu 268 walikamatwa wakihusishwa na makosa mbalimbali yaliyoainishwa katika Kanuni za Usimamizi wa Mazingira ikiwa ni pamoja na Kanuni ya Marufuku ya Uingizaji, Uzalishaji, Usafirishaji na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2019.

77. Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na Idara ya Kemia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, linafanya utafiti kuhusu ubora na viwango vinavyotakiwa kuzingatwa katika utengenezaji wa mifuko mbadala ya ili kujua uwezo wa mifuko hiyo kuoza

Shughuli za Wachimbaji Wadogo

78. Mheshimiwa Spika, shughuli za wachimbaji wadogo wa madini zina changamoto kwa afya ya jamii hususan, madhara yatokanayo na matumizi ya Zebaki na udhibiti duni wa taka ngumu na taka za sumu katika mazingira. Katika hatua za awali, Baraza limeshirikisha wadau muhimu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Madini, Tume ya Madini, Wizara ya Maji, Wataalam wa Mazingira wa Mikoa, na Maafisa Mazingira wa Halmashauri ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto za uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za wachimbaji wadogo. Vile vile, Baraza limeendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maeneo ya wachimbaji wadogo katika mikoa ya Singida, Geita, Mwanza na Mara ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria ya mazingira na Kanuni zake.

Udhibiti wa Taka Hatarishi

79. Mheshimiwa Spika, ili kuzuia na kupunguza athari zitokanazo na taka zenye madhara, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Dawa na Vifaa Tiba limeratibu na kusimamia uteketezaji wa madawa na kemikali zilizokwisha muda wake wa matumizi. Katika zoezi hilo, jumla ya Tani 464, Lita 219,740.5 na Katoni 320,444 za madawa na kemikali zilizokwisha muda wake ziliteketezwa katika Mitambo ya uteketezaji iliyopo

, Mgodini wa dhahabu wa Bulyang'ulu
- Kahama na Chisai - Kibaha katika kipindi hicho.

80. Mheshimiwa Spika, Baraza lilishiriki katika zoezi la ukaguzi wa makasha 148 ya vyuma chakavu yaliyokuwa yanatakiwa kusafirishwa nje ya nchi. Ukaguzi wa makasha hayo ulifanyika kati ya tarehe 11 Septemba na 12 Oktoba, 2019. Lengo la zoezi hili ni kuhakiki uwiano wa taarifa zilizo wasilishwa na aina na kiwango cha vyuma chakavu vilivyo kwenye makasha hayo. Aidha, katika zoezi hilo, makasha 127 yalikutwa na makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na tofauti kati ya mzigo halisi na maelezo yaliyo katika nyaraka. Kufuatia makosa hayo, hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ikiwemo kutozwa faini, zilichuliwa dhidi ya Makampuni sita 6 yaliyokaguliwa na kukutwa na makosa. Aidha, katika kipindi hiki, Baraza lilipokea maombi 120 ya vibali vya kusafirisha taka zenye madhara na kuyachambua na kufanya ukaguzi kwa wale waliokidhi vigezo vibali 57 vilitolewa.



Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)

Usajili wa Miradi na Utoaji wa Vyeti vya Mazingira

81. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza limesajili jumla ya Miradi 887 (Miradi 556 ya Tathmini za Athari kwa Mazingira

na Miradi 331 ya kufanyiwa Ukaguzi wa Athari za Mazingira

. Idadi hii ni asilimia 74 ya miradi ambayo

imekusudiwa kufanyiwa mapitio kwa kipindi cha mwaka wa

fedha 2019/20. Kwa kipindi hicho, miradi ipatayo 375 imepata

vyeti vya mazingira, ambapo miradi 225 ni ya Tathmini za

Athari kwa Mazingira na Miradi 150 ya Ukaguzi wa Athari za

Mazingira. Aidha, miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali

za upembuzi.

82. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza ufanisi

katika masuala ya TAM, Baraza liko katika hatua za mwisho

kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa kusajili miradi kwa njia

ya mtandao . Mfumo huu utawawezesha

wawekezaji kusajili na kufuatilia hatua zilizofikiwa kuhusu

miradi yao bila kulazimika kufika kwenye ofisi za Baraza.



83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza limechukua hatua madhubuti za kuhuisha daftari () la wataalam elekezi. Wataalam husika walitakiwa kuwasilisha taarifa zao ili kuboresha kumbukumbu zilizopo na kuhakikisha TAM inafanywa na wataalam wenye weledi. Katika zoezi hilo, Baraza limepokea taarifa na kuwatambua wataalam elekezi **104** na Kampuni za Ushauri **60** ambazo zimehakikiwa na kukidhi vigezo vilivyowekwa ili kuendelea kutoa huduma ya utalaam elekezi katika shughuli za usimamizi wa mazingira. Aidha, Baraza limeendelea kufuatilia utendaji na ufanisi wa wataalam elekezi () pamoja na Kampuni za ushauri (). Hadi kufikia Mwaka 2019, Baraza limesajili wataalam elekezi wa Tathmini za Athari kwa Mazingira (TAM) **846**, Wakaguzi wa Mazingira **391**, Kampuni za Ushauri wa TAM **162** na za Wakaguzi wa Mazingira **89**.

84. Mheshimiwa Spika, Baraza linatekeleza mpango wa kuhakikisha kuwa Wataalam elekezi wanapewa mafunzo maalum kuhusu Tathmini za Athari kwa Mazingira ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Hivyo, Baraza lina makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Jiografia katika kutoa mafunzo kwa wataalam elekezi ili kukuza weledi katika masuala ya TAM. Awamu ya kwanza ya mafunzo hayo iliyofanyika mwezi Septemba 2019, ilijumuisha wataalam **20**. Baraza litaendelea kutoa mafunzo hayo ili kuwajengea uwezo wataalam elekezi katika shughuli za TAM. Vilevile, Baraza limeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati kama vile

na kutoa maoni na ushauri ili kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu kwa kufuata masharti yaliyoambatishwa na hati za TAM kuhusu usimamizi wa mazingira.

Miongozo na Mafunzo kuhusu TAM

85. Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na kituo cha Sayansi na Mazingira cha India

limeendelea kuandaa miongozo ya TAM kwenye sekta mbalimbali (). Katika zoezi hilo, miongozo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa shughuli za ujenzi wa majengo

imeandaliwa na ipo katika hatua za mwisho za mapitio kabla ya kuidhinishwa na kuanza kutumika. Miongozo mingine inayoandaliwa ni ya sekta za madini, viwanda na njia za umeme. Pia, rasimu za Hadidu za Rejea

kwa miradi ya Madini na Viwanda zimeandaliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa tathmini zinafanyika kwa uhakika na ukamilifu kwa kuzingatia vipengele muhimu kwenye miradi ya aina hiyo. Vilevile Baraza limeshiriki katika warsha na makongamano katika mikoa ya Mtwara, Geita, Pwani, Morogoro na Dar es Salaam na kutoa mada kuhusu umuhimu na taratibu za Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa wadau ikiwa ni pamoja na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi ya Mazingira

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza limetoa mafunzo ya elimu kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia vyombo vya habari kama magazeti, vipeperushi, runinga; na mitandao ya kijamii ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu masuala ya mazingira. Vipindi 30 vimerekodiwa na kurushwa kupitia vyombo mbalimbali vya Habari nchini. Aidha, Baraza lilishiriki katika maadhimisho ya kitaifa na kimataifa kuhusu mazingira kwa lengo la kukuza uelewa kuhusu mazingira ili kuboresha uwajibikaji katika kutunza mazingira.

87. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Baraza kwa kushirikiana na Mradi wa

unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini limefanya mafunzo kwa watendaji wa mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wataalam wa Mazingira wa Mikoa na Maafisa Mazingira wa Halmashauri ili kuwajengea uwezo katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Sura ya 191 katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa lengo la kukuza uelewa wa masuala ya mazingira hususan matumizi ya nishati mbadala. Mafunzo hayo yalifanyika katika kanda tatu za Baraza ambazo ni Kanda ya Mashariki inayohusisha mikoa Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro (maafisa 40), Kanda ya

Magharibi inayohusisha mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi (maafisa 31) na Kanda ya Kaskazini yaani mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara (maafisa 51).

88. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia Baraza limetoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira

33 kutoka Halmashauri za Kanda ya Kusini inayojumuisha mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi; 40 kutoka Kanda ya Ziwa yenye Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita, Simiyu, Kagera, na Mara; na 15 kutoka Wizara ya Maji. Mafunzo hayo yamewezesha wakaguzi kusimamia sheria ya mazingira katika maeneo yao ya utendaji.

Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (National Environmental Research Agenda- NERA)

89. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira, Baraza liliendesha Kongamano la Tano la Kisayansi kuhusu Binadamu na Hifadhi Hai

lililofanyika mwezi Agosti, 2019, Jijini Arusha. Madhumuni ya Kongamano hilo yalikuwa ni kujadili tafiti mbalimbali, matokeo yake na kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na athari za kimazingira zinazojitokeza hasa kwenye maeneo ya hifadhi hai. Kongamano hilo lilijumuisha wadau **150** wakiwemo watafiti, wanasayansi na wahifadhi kutoka ndani na nje ya Tanzania. Mada **20** kuhusu uharibifu wa mazingira, viumbe vamizi na matumizi yasiyokuwa endelevu ya maji ziliwasilishwa.

Uratibu wa Miradi Inayotekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo Nchini

90. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Baraza limekamilisha utekelezaji wa mradi wa Kuhifadhi Lindimaji la Bonde la Kihansi pamoja na Dakio lake

uliofikia ukomo tarehe 31 Desemba 2019. Mradi huo uligharimu Dola za Marekani milioni **5.98** kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) kupitia Benki ya Dunia. Lengo la mradi huo lilikuwa ni kuhifadhi bioanuai katika bonde

la Mto Kihansi hususan viumbe adimu na walio hatarini kutoweka. Baada ya mradi huo kufikia ukomo, shughuli zote zimehuishwa kwenye mipango ya Halmashauri za Kilolo, Mufindi na Kilombelo, Baraza la Taifa la Hifadhi na usimamizi wa Mazingira, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliohusika katika utekelezaji wake.

91. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto za mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi, Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Bunda na Kongwa, na Asasi Zisizo za Kiserikali limeandaa na kuwasilisha maandiko manne (4) ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi () kwa ajili ya kupatiwa ufadhili. Miradi hiyo ni: Mradi wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi miongoni mwa jamii za Pwani kutoka Zanzibar (

) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **1**; Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi Bunda (

) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **1.4**; Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye jamii za wafugaji na wakulima wilaya ya Kongwa (

) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **1.2**; na Mradi wa kimkakati wa uvunaji maji katika maeneo kame ya ukanda wa kati (

)) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **1.28**.

92. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Baraza limeendelea na jitihada za kusogeza huduma kwa wananchi kwa kufungua Ofisi ya Kanda ya Magharibi mkoani Kigoma, na kufanya idadi ya ofisi za kanda za Baraza kufikia 7. Aidha, ili kuongeza ufanisi, Baraza limefanikiwa kuziongezea vitendea kazi na kuongeza watumishi 20 ambao baadhi wamepangiwa kazi katika Ofisi za Kanda ili kuzijengea uwezo. Vile vile, muundo wa Baraza umehuishwa na kuanza kutumika.

93. Mheshimiwa Spika, Baraza pia limetoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi katika fani mbalimbali ili kukuza weledi. Jumla ya watumishi (4) wanahudhuria mafunzo ya Muda Mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na watumishi (6) wanahudhuria mafunzo katika ngazi ya Uzamili. Vile vile, watumishi wa Baraza wameendelea kushiriki mikutano na warsha zinazohusu masuala ya mazingira ndani na nje ya nchi.

94. Mheshimiwa Spika, sheria ya mazingira imelipa Baraza mamlaka ya kukusanya ada na tozo mbalimbali za mazingira ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake. Baraza limeendelea kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 hususan Kanuni ya Ada na Tozo za Mazingira ya Mwaka za mwaka 2018 zilizofanyiwa maboresho mwaka 2019 kwa kupunguza viwango vya tozo hususan katika kufanya tathmini ya Athari kwa Mazingira. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza limeweza kuwafikia wadau 6,000 wa mazingira ambao wamefahamishwa wajibu wa kulipa ada na tozo za mazingira. Zoezi hili limehusisha maafisa wa Baraza kutoka katika Ofisi zote za Kanda.

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI BARAZA NA MIKAKATI ILIYOPO

95. Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Baraza katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira, bado kumekuwa na changamoto zifuatazo: Uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa wawekezaji, wataalam elekezi na jamii kwa ujumla; Uhaba wa watumishi wa fani ya mazingira; Uwekezaji katika maeneo ambayo hayakufanyiwa Tathmini ya Athari ya Mazingira Kimkakati; Sekta kutokuwa na miongozo husika ya tathmini za Athari kwa Mazingira na Uwasilishaji wa Taarifa zenye upungufu katika TAM.

96. Mheshimiwa Spika, Baraza limekuwa likichukua hatua kadhaa ili kukabiliana na changamoto hizi zikiwemo kuendelea kujengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa vibali vya ujenzi vinatolewa katika maeneo yaliyotengwa maalum kwa aina hiyo ya miradi; Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kupitia

vyombo vya habari na maadhimisho; kuwajengea uwezo wataalam elekezi wa maswala ya mazingira na makampuni ili kuongeza ufanisi katika zoezi la TAM; Kutumia wahitimu wa vyuo vikuu () katika shughuli zake hasa ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi pamoja na ukusanyaji wa tozo za mazingira ili kukabiliana na changamoto ya idadi ndogo ya wafanyakazi; na kuhamasisha Sekta Binafsi na Serikali za Mitaa kushiriki katika shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi imeendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili ya Utumishi wa Umma na imewezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, utendaji kazi wa watumishi umeendelea kupimwa kwa kutumia mfumo wa wazi wa Tathmini na Mapitio ya Utendaji Kazi

98. Mheshimiwa Spika katika kipindi hiki, jumla ya watumishi **46** wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo na kuongeza ujuzi na maendeleo kulingana na kada zao (). Katika kipindi hiki, watumishi sita (**6**) wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi **11** wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi kwa kugharamiwa na Serikali na Wafadhili. Aidha, watumishi **29** wamepatiwa mafunzo ya awali kwa mujibu wa Sheria.

99. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kusafisha taarifa za watumishi kwa kuhakiki kumbukumbu zao na kuziboresha kupitia mfumo Taarifa za Kiutumishi na mishahara (). Aidha, watumishi wote wamesajiliwa kwenye Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na taarifa zao zimeingizwa kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi.

100. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/20, Ofisi imendelea kuimarisha maadili, Utawala Bora, Demokrasia na dhana ya ushirikishwaji na uwajibikaji wa watumishi mahala pa kazi, kupitia vikao vya Idara na Vitengo, Vikao vya kamati za Maadili na Uadilifu, vikao vya menejimenti na vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Aidha, sekta binafsi imeshirikishwa katika utoaji wa huduma na bidhaa katika Ofisi ili kuendeleza dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi.

101. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa kadiri fedha zilivyopatikana. Aidha, majengo ya Ofisi na mazingira ya kazi yameboreshwa kwa kufanya ukarabati wa majengo yaliyopo, kulingana na fedha zilivyopatikana.

CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

102. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yetu, Ofisi ilikumbana na changamoto kadhaa zikiwemo;- Upungufu wa idadi inayostahili ya watumishi katika kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira; Kukosekana kwa Mfumo Thabiti wa Mashirikiano baina ya Taasisi za Serikali kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Uelewa Mdogo wa Jamii kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Uzingatiaji mdogo wa jamii kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

103. Mheshimiwa Spika, katika kukabilina na changamoto hizi, Ofisi ilichukua hatua zifuatazo:- Kuendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora kwa ajili ya kuongezewa rasilimali watu; Kufanya vikao vya ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na OR-TAMISEMI kubaini aina ya mfumo utakaotumika kuimarisha mashirikiano katika kutekeleza kazi za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Uhifadhi na Usimamizi wa mazingira na umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali.

MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/21

MASUALA YA MUUNGANO

104. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Muungano kwa Mwaka 2020/21, Ofisi imepanga kutekeleza majukumu na malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Vikao hivi vitafanyika katika ngazi zifuatazo:- Kikao kimoja (1) cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ; Kikao kimoja (1) cha Mawaziri wa SMT na SMZ; Vikao viwili (2) vya Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ; Vikao vinne (4) vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ; na Vikao vya Kamati Ndogo za Fedha, Uchumi na Baishara na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala pindi itakapohitajika.

ii. Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano, kuhakikisha gawio la asilimia 4.5 ya Fedha za Misaada ya Kibajeti (GBS), faida ya Benki Kuu, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na PAYE linapelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

iii. Kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii kupitia redio, runinga, makala za magazeti, Kongamano la Muungano na mitandao ya kijamii. Elimu sahihi ya Muungano itasaidia kuamsha ari ya wananchi wa Tanzania kuenzi, kuulinda na kuimarisha Muungano wetu.

iv. Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana. Ofisi itaendelea kuzihimiza Taasisi zisizo za Muungano kuendelea kushirikiana katika masuala ya Sera, kubadilishana utalam na wataalam, kushirikiana katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo. Ushirikiano huu ni

muhimu kwa kuwa unasaidia kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza.

HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEU WA MAZINGIRA

105. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuna hifadhi endelevu ya mazingira mwaka 2020/21, Ofisi imepanga kutekeleza yafuatayo: -

Elimu kwa Umma Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira

106. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa jamii na uchumi. Katika kipindi hiki, juhudi zaidi zitaelekezwa katika kuendelea kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki na kuhamasisha matumizi ya mifuko mbadala inayokidhi viwango. Aidha, Ofisi itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambayo yana athari kubwa kwenye mazingira.

Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Kukabiliana na Viumbe Vamizi (Invasive Species)

107. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati huu kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na tathmini ya utekelezaji wake.

Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)

108. Mheshimiwa Spika, Ofisi iteandeshwa mafunzo ya TMK kwa Maafisa Mazingira kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kanda zilizobaki za Magharibi, Kusini na Nyanda za Juu Kusini zinazojumuisha mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Iringa, Njombe, Katavi, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Aidha, Ofisi itaendelea kuratibu mapitio ya Taarifa za TMK.

Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)

109. Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana Baraza itaandaa mfumo wa kieletroniki wa ufuatiliaji mchakato wa utoaji wa

vyeti vya TAM. Mfumo huu utasaidia kuongeza ufanisi, na uwajibikaji katika taratibu za Tathmini ya Athari Kwa Mazingira.

Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini ya Mwaka 2019

110. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuzitatua changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini kupitia uandaaji na utekelezaji wa Mikakati, Mipango na Miradi ya kuhifadhi na kulinda mazingira nchini.

Mwongozo wa Matumizi ya Eneo la Hifadhi ya Mita 60 kutoka kwenye Vyanzo vya Maji

111. Mheshimiwa Spika Ofisi itakamilisha Mwongozo wa Matumizi ya Eneo la Hifadhi ya Mita 60 kutoka kwenye Vyanzo vya Maji kuanza utekelezaji wake. Inatarajiwa Mwongozo huu utakamilika Mei, 2020.

Usimamizi wa Taka Hatarishi

112. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2020/21, Ofisi itaendelea kusimamia taka hatarishi nchini ili kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla. Aidha, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhhibiti wa Taka Hatarishi za Mwaka 2019 pamoja na kutoa mafunzo kwa taasisi za udhibiti, watu binafsi na makampuni yanayojihusisha na taka hatarishi. Mafunzo hayo yatahusu matumizi ya mfumo wa kieletroniki wa kuomba vibali vya taka hatarishi ambao utarahisisha utaratibu wa utoaji vibali husika.

Matumizi ya Mifuko ya Plastiki

113. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa kanuni za kupiga marufuku mifuko ya plastiki za Mwaka 2019 na kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya mifuko mbadala inayokidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania. Aidha, Ofisi itaendelea kushirikiana na wadau katika kutekeleza katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki ikiwemo kutoa elimu kwa Umma.



Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility – GEF)

114. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi itaendelea kuratibu mfuko ya GEF ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za utekelezaji miradi mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira nchini. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (Zanzibar); Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Ofisi itaendelea kukamilisha maandiko ya miradi mitano na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mkatoba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Makubaliano ya Paris

115. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkatoba wa Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mkatoba huu, kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mpango wa Taifa wa

Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame

116. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame, kukamilisha maandiko mawili (2) ya miradi na kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Mkataba. Maandiko hayo ya kutekeleza Mkataba huo ikiwa ni pamoja na kuendelea kuratibu mapitio ya Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame.

Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai

117. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi itaendelea kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika maandalizi ya Mkakati wa Kimataifa wa Kuhifadhi Bioanuai Baada ya Mwaka 2020 -

. Aidha, Ofisi itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa katika Wilaya za Mbinga, Nyasa, Makete na Ludewa.

Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

118. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Montreal na Itifaki yake ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Kanuni za Udhhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; kudhibiti uingizaji na matumizi ya kemikali jamii ya _____ na _____ na kuendelea kuelimisha umma umuhimu wa hifadhi ya tabaka la Ozoni.

Mkataba wa Basel kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka Hatarishi Kati ya Nchi na Nchi

119. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Basel ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa

vibali vya ukusanyaji, usafirishaji na utupaji wa taka hatarishi kwa mfumo wa kieletroniki. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu udhibiti wa taka hatarishi, madhara na fursa zilizopo katika kutekeleza Mkataba huu.

Mkataba wa Stockholm kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu

120. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm na kufuatilia utekelezaji wake. Aidha, katika kutekeleza Mkataba huu, Ofisi itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Shirika la Viwango Tanzania kukusanya sampuli za maji na udongo kwa Mikoa ya Pwani na Singida kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kiwango cha uchafuzi katika maeneo hayo utokanao na kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu.

Vilevile, Ofisi kwa kushirikiana na TANESCO itakusanya na kuteketeza mafuta ya transform ya yaliyobainika kuwa na kemikali jamii ya PCBs na Kuandaa Kanuni Mahsuszi za Udhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira Kwa Muda Mrefu. Aidha, katika kupunguza uzalishaji wa kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu zitokanazo na uchomaji holela wa taka ngumu, Ofisi kwa kushirikiana na Manispaa za Ubungo na Kigamboni itaanzisha vituo vya mfano vya ukusanyaji na urejelezaji wa taka ngumu katika Manispaa hizo.

Mkataba wa Minamata Kuhusu Usimamizi wa Zebaki

121. Mheshimiwa Spika Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Minamata kuhusu Usimamizi wa Zebaki ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu (2020 – 2025); kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Zebaki za Mwaka 2020; na kuendelea kuelimisha Umma kuhusu madhara ya Zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira.

MALENGO YA BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

122. Mheshimiwa Spika, Baraza katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 limepanga pamoja na mambo mengine kutekeleza yafuatayo katika mwaka 2020/21: -

i) Kuendelea na kampeni za elimu ya mazingira kwa umma na kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi/shughuli mbalimbali zikiwemo kufuatilia malalamiko yanayowasilishwa na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake;

ii) Kushiriki katika kuandaa na kufanya mapitio ya nyenzo na miongozo miwili (2) inayohusu uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake;

iii) Kuimarisha Usimamizi wa taka ngumu kwa kushirikiana na wadau na kuimarisha uhibitaji wa utupaji wa taka hatarishi kwa kufanya kaguzi kila mwezi;

iv) Kuimarisha ofisi za kanda 7 zilizoanzishwa kwa kuongeza watumishi na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi;

v) Kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Baraza ili kuwezesha upatikanaji wa vyeti kwa haraka zaidi;

vi) Kufanya mapitio ya TAM kwa miradi 1300 itakayosajwa kwa ajili ya kupata vyeti vya TAM/ ukaguzi;

vii) Kufanya usajili wa Wataalam elekezi (80) na kampuni za TAM (20) na kufanya vikao 4 vya kinidhamu ili kufuatilia mienendo yao katika kutoa ushauri kwenye masuala ya Mazingira;

viii) Kuanza ujenzi wa ofisi za kudumu katika kiwanja cha Baraza kilichopo eneo la Njendengwa, Dodoma;

ix) Kujenga uwezo wa watumishi wa Baraza kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi ili kuboresha utendaji wa kazi;

x) Kuratibu na kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira;

xi) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kujenga uwezo katika rasilimali fedha kwa kuongeza wigo wa mapato kwa kuwafikia wadau 2000 zaidi wanaoguswa na utekelezaji wa Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira (Ada na Tozo) ya mwaka 2019;

xii) Kuwezesha wadau kuandaa miradi 4 ya Mabadiliko ya Tabianchi itakayowasilishwa katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia; na

xiii) Kufuatilia shughuli za kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na kufanya mapitio ya miradi yote itakayowasilishwa na wadau na kuiwasilisha kwenye Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi iweze kupata ufadhili.

MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

123. Mheshimiwa Spika, Ofisi imepanga kuwawezesha watumishi **36** kuhudhuria mafunzo kwa kuzingatia mpango wa mafunzo. Watumishi **74** watapandishwa vyeo kwa kuzingatia utendaji wao wa kazi na miundo inayotawala kada zao na watumishi **3** watahibitishwa kazini na watumishi **25** wataajiriwa.



124. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu na kuimarisha Maadili na Utawala bora katika Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, ushauri nasaha, na kupima afya kwa hiari na kutoa huduma stahiki kwa watakaojitokeza na kuthibitika kuwa na maambukizi ya VVU. Vilevile, Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi, samani za Ofisi na stahili za watumishi.

HITIMISHO NA SHUKRANI

125. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya Muungano ambao una umuhimu wa pekee kwa Taifa na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha Amani, Mshikamano na Usalama wa nchi yetu. Mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 56 tangu kuasisiwa kwake. Ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa faida za pande zote mbili za Muungano.

126. Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri. Chini ya uongozi wao mahiri, hakuna changamoto yoyote inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. Katika mwaka 2020/21, Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi mambo yote yanayoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala yanayohusu Muungano na kutoa elimu kuhusu Muungano ili uendelee kuimarika.

127. Mheshimiwa Spika, maendeleo endelevu na uchumi wa viwanda haviwezi kupatikana bila kutunza na kuhifadhi mazingira. Kutokana na umuhimu huu, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi

yetu zinalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo. Ninapenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

128. Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Serikali inathamini wawekezaji kwa kuwa wana mchango mkubwa katika pato la Taifa, kutoa ajira na kupunguza umaskini nchini. Hivyo, natoa rai kwa wawekezaji kutunza mazingira kwa kuzingatia sharia za nchi ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ili kuwa na maendeleo endelevu nchini.

129. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Ofisi itaendelea kutoa miongozo katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira kwa kuangalia mifumo ikolojia, mifumo ya uzalishaji mali, na mifumo ya uchumi ya matumizi ya rasilimali asili. Vilevile Ofisi, imejipanga kuipa elimu ya mazingira kipaumbele kwa jamii ili kuhakikisha mazingira yanalindwa na kutunzwa.

SHUKRANI

130. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake makini unaotuwzesha kutekeleza majukumu yetu. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji majukumu ya kila siku.

131. Mheshimiwa Spika, Vilevile, ninapenda kuwashukuru Joseph K. Malongo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; Joseph E. Sokoine, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya

Makamu wa Rais, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira, Prof. Esnati O. Chagguna, wajumbe wa Bodi, Dkt. Samuel Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na Baraza. Pia ninawashukuru wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21.

132. Mheshimiwa Spika, Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway; Serikali ya Canada; Serikali ya Sweden; Serikali ya Italia; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (); Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (); Mfuko wa Mazingira wa Dunia () Benki ya Maendeleo ya Afrika
Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda

Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani ()
Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo
Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ()
Shirika la Kilimo na Chakula Duniani
Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani () Kikundi cha Washirika wa Maendeleo kinachoshughulikia Mazingira ()
; Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); na Sekta Binafsi. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo kuendelea kutoa ushirikiano katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi

katika kulinda na kuimarisha Muungano wetu na kulinda na kuhifadhi mazingira yetu.

MAOMBI YA FEDHA

133. Mheshimiwa Spika, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha jumla ya Shilingi **27,990,155,000.00** kama ifuatavyo:

Fungu 26: Makamu wa Rais

134. Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Shilingi **8,759,191,000.00** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2020/21. Kati ya fedha hizi, Shilingi **1,024,226,000.00** ni fedha za Mishahara ya watumishi na Shilingi **7,734,965,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

135. Mheshimiwa Spika, katika fungu hili ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe jumla ya Shilingi **19,230,964,000.00**. Kati ya fedha hizi, Shilingi **11,581,534,000.00** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,649,430,000.00** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Shilingi **6,634,482,000.00** fedha za Mishahara na Shilingi **4,947,052,000.00** fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Mishahara zinajumuisha kiasi cha Shilingi **3,083,994,000.00** Mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kiasi cha Shilingi **3,550,488,000.00** ni Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha fedha za Ndani Shilingi **1,000,000,000.00** na Shilingi **6,649,430,000.00** ni fedha za nje.

136. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria atakayesoma taarifa yake kutokea Msekwa. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6(2) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria ya jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. Aidha, Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kinatoa jukumu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazosisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa Bajeti linaenda sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ina Mafungu 2 ya Bajeti ambayo ni Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Kwa kuzingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano), hakukuwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Fungu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano. Katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, ambapo taarifa hiyo iliainisha kwamba Sh.1,000,000,000 zilizotengwa kutoka fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usalama na ukarabati wa makazi ya Makamu wa Rais – Tunguu Zanzibar, zipo tayari kutolewa na Hazina kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi saba (7) ambao wameingia mkataba na Ofisi hiyo na kazi zinaendelea. Hivyo, hatua inayofuata ni uwasilishaji wa hati za madai ambao utawezesha kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango maombi ya fedha hizo ili zilipwe kwa wazabuni hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, tarehe 24 Machi, 2020. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili, 2019 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Februari, 2020 katika robo ya tatu ya mwaka huu wa Fedha 2019/2020. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 ili kujua vipaumbele vya kibajeti na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina. Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu 26 la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais lilitengewa Sh.7,855,093,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh.6,734,965,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.1,120,128,000 ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020, jumla ya Sh.4,901,091,590.45 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kiasi hicho cha Fedha kilichopokelewa ni sawa na asilimia 62.4% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika Fungu 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati, hatua ambayo imesaidia Ofisi Binafsi ya Makamu Rais -Muungano kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu la 31 la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa Sh.6,352,734,454 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ambapo Sh.5,352,734,454 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.1,000,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Ofisi hiyo ilipokea Sh.2,721,837,543.14 sawa na 50.8% ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za bajeti ya Matumizi ya Kawaida, kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mafungu yote yaani Fungu 26 na Fungu 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza sana Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kutoa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 - Fungu 31. Kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Sh.1,000,000,000 zilizokuwa zimetengwa hazijatumika na tayari wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi husika, maoni ya Kamati ni kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ikamilishe taratibu za Hati ili Hazina iwalipe kwa wakati wakandarasi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi Wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa mwaka wa fedha 2020/2021 tarehe 24 Machi 2020, ambayo imelenga

kutekeleza masuala ya Muungano kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano vya kushughulikia masuala ya Muungano;

(iii) Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii pamoja na kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa pande mbili zote za Muungano kila robo mwaka;

(iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii; na nne

(iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao 15 vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye majukumu yanayoshabihiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha udugu, umoja na mshikamano wa Watanzania kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendeleza jitihada katika kutatua changamoto mbalimbali za Muungano, hususan, kuendelea kurahisisha mwingiliano wa kibiashara baina ya pande mbili za Muungano kwa kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali za kikodi na kisheria kwa manufaa ya pande zote mbili na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.8,759,191,000 kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, Sh.1,024,226,000 ni kwa ajili ya Mishahara, na Sh.7,734,965,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Bajeti ya Fungu 26 imeongezeka kwa kiasi cha Sh.804,098,000 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ongezeko hilo ni sawa na 10.24% ya bajeti ya Fungu 26 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo hususan gharama za utoaji huduma kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31 inaomba kuidhinishwa jumla ya Sh.6,903,111,560 kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh.6,303,111,560 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.600,000,000 ni kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha shilingi 2,038,371,560/= ambapo ni fedha za Mishahara na Shilingi 4,038,371,560/= ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya Fungu 31 imeongezeka kwa shilingi 550,377,106/=: sawa na asilimia 8.7 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya fungu hili kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Fungu 31, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi milioni 600 kutoka fedha za ndani kwa ajili Ujenzi wa (mageti mawili ya kutokea na kuingilia, , mgahawa na ofisi ya madereva) katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Mtumba; ukarabati wa paa kuta, sakafu na dari; matengenezo ya milango,

madirisha na samani za jikoni; ufungaji wa mabomba (maji safi na taka) na vyoo; ufungaji wa mfumo wa hewa na matengenezo ya jenereta katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete, Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza fedha hizo zitolewe kwa wakati kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 ili kurahisisha ukamilishaji wa shughuli hizo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hivyo, inashauri Ofisi hiyo iendelee na utekelezaji huo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kushirikiana na Mamlaka husika za pande mbili zote za Muungano katika kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Biashara baina ya Pande mbili za Muungano, hatua ambayo itachochea ukuaji Uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Serikali iendelee na juhudi hizo katika kubaini changamoto mpya zinazoweza kuibuka na kuzitatua kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo na kwa wakati na pia kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuliendesha vizuri Bunge hili letu la Kumi na Moja na kuishauri vyema Serikali kwa manufaa haya ya wananchi wa Tanzania, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mfumo wa Bunge Mtandao kwa ufanisi wa Bunge lako Tukufu.

Aidha, nakushukuru pia na wewe na kukupongeza kwa kazi kubwa na weledi mkubwa na umahiri wako unaoufanya katika kulisaidia kuongoza Bunge na kumsaidia Mheshimiwa Spika. Pia nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwashauri na kusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja. Wote kwa pamoja tunawaombea afya njema na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa pamoja na Bunge Zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Naibu Waziri; Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Naibu Waziri, ambaye pia na Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitisha na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. Naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kuwashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg. Gerald S. Magili, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rahel Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii pamoja na Watendaji Wote wa Idara husika za Bunge kwa kuhakikisha Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA
MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA
2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA
MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (2) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rias - Muungano.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kinatoa Jukumu

kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ina Mafungu 2 ya Bajeti ambayo ni:-

- i) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na
- ii) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais,

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

2.1 Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano), hakukuwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Fungu hili.

2.2 Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano;

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, ambapo taarifa hiyo iliainisha kwamba, **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000.00)** zilizotengwa kutoka fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usalama na ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais – Tunguu Zanzibar, zipo tayari kutolewa na Hazina kwa ajili ya kuwalipa Kandarasi saba (7) ambazo zimeingia mkataba na Ofisi hiyo na kazi zinaendelea. Hivyo, hatua inayofuata ni Uwasilishaji wa hati za madai ambao utawezesha kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango maombi ya fedha hizo ili fedha zilipwe kwa wazabuni hao.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 24 Machi, 2020. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2019 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Februari, 2020 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa Fedha 2019/2020. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kujua vipaumbele vya kibajeti, ili kuishauri Serikali ipasavyo.

3.2 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina;

3.2.1 FUNGU 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais;
Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 **Fungu 26** la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais **ilitengewa Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Hamsini na Tano na Tisini na Tatu Eflu (7,855,093,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Thelathini na Nne, Laki Tisa Sitini na Tano Eflu (6,734,965,000/=)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Ishirini, Laki Moja Ishirini na Nane Eflu (1,120,128,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2019 hadi mwezi Februari, 2020, **Jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa na Moja, Tisini na Moja Eflu, Mia Tano Tisini na Senti Arobaini na Tano (4,901,091,590.45)**, zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kiasi hicho cha Fedha kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 62.4%** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika **Fungu 26**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati, hatua ambayo imesaidia Ofisi Binafsi ya Makamu Rais-Muungano kutekeleza Majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

3.2.2 FUNGU 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 **Fungu 31** la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu Hamsini na Mbili, Laki Saba Thelathini na Nne Eflu, Mia Nne Hamsini na Nne (6,352,734,454/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo, ambapo, **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Hamsini na Mbili, Laki Saba Thelathini na Nne Eflu, Mia Nne Hamsini na Nne (5,352,734,454/=)** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Ishirini na Moja, Laki Nane Thelathini na Saba Eflu, Mia Tano Arobaini na Tatu na Senti Kumi na Nne (2,721,837,543.14/=)** sawa na asilimia 50.8% ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, kwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mafungu yote **(Fungu 26 na Fungu 31)**.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa wakati.

3.2.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - FUNGU 31

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, **Jumla ya Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000.00)** zilizokuwa zimetengwa hazijatumika, na tayari Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa Miradi husika, **maoni ya Kamati ni kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais ikamilishe taratibu za Hati ili Hazina iwalipe kwa wakati Wakandarasi hao.**

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 tarehe 24 Machi 2020, ambayo imelenga kutekeleza masuala ya Muungano kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

- i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ vya Kushughulikia Masuala ya Muungano;
- ii) Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii pamoja na kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa pande mbili za Muungano kila robo mwaka;
- iii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii, na
- iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao 15 vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zenye majukumu yanayoshabihiana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha Udugu, Umoja na Mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendeleza jitihada katika kutatua changamoto mbalimbali za Muungano, hususan, kuendelea kurahisisha mwingiliano wa kibiashara baina ya Pande mbili za Muungano kwa kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali za kikodi na kisheria kwa manufaa ya pande zote mbili na wananchi wake kwa ujumla.

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

4.1.1 Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (**Fungu 26**) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa na Laki Moja Tisini na Moja Eflu (8,759,191,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Moja Ishirini na Nne, Laki Mbili Ishirini na Sita Eflu (1,024,226,000/=)** ni kwa ajili

ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Thelathini na Nne, Laki Tisa Sitini na Tano Eflu (7,734,965,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Bajeti ya **Fungu 26** imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Milioni Mia Nane na Nne na Tisini na Nane Eflu (804,098,000/=)** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 10.24%** ya Bajeti ya **Fungu 26** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi Ofisi hiyo hususan gharama za utoaji huduma kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

4.1.2 Fungu 31; Ofisi ya Makamu wa Rais

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31**) inaomba kuidhinishwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tisa na Tatu, Laki Moja Kumi na Moja Eflu, Mia Tano Sitini (6,903,111,560/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu na Tatu, Laki Moja Kumi na Moja Eflu, Mia Tano na Sitini (6,303,111,560/=)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi Milioni Mia Sita (600,000,000/=)** ni kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili Sitini na Nne, Laki Saba Arobaini Eflu (2,264,740,000/=)** ni fedha za Mishahara na **Shilingi Bilioni Nne na Milioni Thelathini na Nne, Laki Tatu Sabini na Moja Eflu, Mia Tano Sitini (4,038,371,560/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti ya **Fungu 31** imeongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Tano Hamsini, Laki Tatu Sabini na Saba Eflu, Mia Moja na Sita (550,377,106/=)**, sawa na **asilimia 8.7%** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

4.1.3 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (FUNGU 31).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Milioni Mia Sita Elfu (600,000,000/=)** kutoka Fedha za Ndani kwa ajili Ujenzi wa (Mageti mawili ya kutokea na kuingilia, pavements, mgahawa na ofisi ya madereva) katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Mtumba; ukarabati wa Paa kuta, sakafu na dari; matengenezo ya milango, madirisha na samani za jikoni; Ufungaji wa mabomba (maji safi na taka) na vyoo; ufungaji wa mfumo wa hewa (na matengenezo ya jenereta katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete – Pemba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Fedha hizo zitolewe kwa wakati kwa Mwaka huu wa Fedha 2020/2021 ili kurahisisha ukamilishaji wa shughuli hizo muhimu.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kama ifuatavyo:-

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hivyo, inashauri Ofisi hiyo iendelee na utekelezaji huo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kushirikiana na Mamlaka husika za pande mbili za Muungano katika kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya biashara baina ya Pande mbili za Muungano, hatua ambayo itachochea ukuaji

Uchumi kwa Mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Serikali iendelee na juhudi hizo katika kubaini changamoto mpya zinazoweza kuibuka na kuzitatua kwa haraka.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa lengo kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge la Kumi na Moja (11) katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mfumo wa Bunge Mtandao kwa ufanisi zaidi wa Bunge lako Tukufu. Aidha, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhe. Mussa Azan Zungu, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Mussa Ramadhan Sima, (Mb), Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti

ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI YA BUNGE (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline K. Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Suzan Alphonse Kolimba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg. Gerald S. Magili, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Aidha, Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii pamoja na Watendaji Wote wa Idara husika za Bunge kwa kuhakikisha Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
16 APRILI, 2019

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambaye yeye atasoma kutoka huku Bungeni. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi wa Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Fungu 31 – Idara ya Mazingira kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na maoni kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa mwaka fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Fungu 31 – Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili kwa Mwaka Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilizingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020, ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31 – Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kuchambua Mpango na Bajeti wa Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 98 (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa Maelezo ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Makamu wa Raisi, Mazingira Fungu 31, iliidhinishiwa shilingi bilioni 18.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu la ukaguzi wa miradi, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli za Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira katika maeneo mawili ambayo ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya kiwango cha Dar es Salaam; Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Gesi ya Kinyerezi Dar es Salaam kwa

lengo la kukagua na kuona namna utekelezaji wa mradi unavyoendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira na pia kubaini namna Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wanavyotekeleza jukumu la kusimamia sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuwa miradi hii ilishafanyiwa tathmini ya athari za mazingira na kupatiwa Cheti cha Mazingira. Aidha, miradi yote miwili imekuwa ikitembelewa na Maafisa wa Baraza ili kuweza kujiridhisha kama wamiliki wanazingatia maagizo na maelekezo ya mazingira yaliyopo kwenye cheti. Hali ya miradi hii ni kama inavyoelezwa katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha ziara ya ukaguzi wa Kamati, inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira iweke taratibu wa kuweka Afisa wa katika kila Mradi wa Maendeleo unaotekelezwa kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu wa mazingira wakati wote wa utekelezaji wa mradi. Jambo hili litawezesha hatua zote za mradi kuzingatia masuala ya mazingira;

(ii) Baada ya miradi kukamilika, iwezeshe kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha masuala yanayokubaliana na Cheti cha Mazingira bado yanazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Lengo likiwa ni kujiridhisha kuhusu ukusanyaji wa mapato, utekelezaji wa malengo/kazi na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mapato yanayokusanywa Chini ya Fungu 31 – Idara ya Mazingira, lakini Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambalo lipo chini ya Ofisi hii hufanya makusanyo kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020 lilipanga kukusanya Shilingi bilioni 21.6. Hadi kufikia Machi, 2020 Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi bilioni 9.17 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 42.3 ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kushuka kwa makusanyo kumechangiwa na kushuka kwa ada na tozo za Tathmini ya Athari kwa Mazingira hatua iliyosababishwa na maboresho yaliyofanywa katika kanuni zinazosimamia mchakato wa .

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuliimarisha Baraza kwa kuipatia rasilimali inayohitaji ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Hatua hii itasaidia kuongeza uwezo wa Baraza, kuhudumia wadau wengi zaidi na wapya, jambo ambalo litaongeza mapato ya Baraza lakini pia itasaidia kuongeza kasi katika usimamizi wa uhifadhi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31 – Idara ya Mazingira iliidhinishwa shilingi bilion 22.7 kwa ajili ya matumizi ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Shilingi bilioni 4.49 za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 18.2 za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha shilingi bilioni 5.4 kilikuwa kimepokelewa, sawa na asilimia 23.9 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kiasi kilichopokelewa ni pungufu kwa asilimia 76.1, hadi kufikia kipindi hiki cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha una madhara zaidi kwa upande wa utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo, ambapo shilingi bilioni 2.9 tu sawa na asilimia 16.08 ya fedha za Miradi ya Maendeleo ndiyo zilizotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo ulitokana na kuwa, miradi mitatu kati ya miradi iliyotengewa fedha katika mwaka 2019/2020 fedha zake kutopokelewa kutokana na kutokamilika kwa majadiliano kati ya Serikali na Wafadhili. Kamati inasisitiza Serikali kulipa uzito suala hili na kukamilisha majadiliano hayo ili fedha zipelekwe na miradi husika ianze kutekelezwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi za Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kazi za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, zimetekelwa. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza kuongeza juhudi kadhaa kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kutoa taarifa kwa Serikali, imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza maagizo hayo. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kuyatekeleza maagizo hayo kama ilivyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Uhifadhi na Usimamizi Mazingira, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa lengo la kufuatilia tija iliyoweza kupatikana ikihusishwa na fedha zilizoombwa katika kifungu 5003. Kamati ilibaini kuwa malengo yote yalizingatia hati idhini ya Serikali iliyoidhinisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais,

Mazingira. Kamati imeishauri Serikali kuiwezesha kikamilifu Ofisi hii kutekeleza malengo yake iliyojipangia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato, katika mwaka wa fedha 2020/2021, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanywa chini ya Fungu 31 – Idara ya Mazingira, lakini Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – linalenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 24.09 kutoka katika vyanzo vya ndani vya Baraza ambavyo ni ada na faini zitokanazo na shughuli za usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kinacholengwa kukusanywa kimeongozeka kwa asilimia 9.9 ikilinganishwa na malengo ya makusanyo ya Baraza ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambalo yalitekelezwa kwa asilimia 42.3 tu hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutambua wigo wa mapato yatokanayo na shughuli za Mazingira, lakini pia kuliongezea Baraza uwezo kwa kuwapatia watumishi vitendea kazi ili waweze kuongeza kasi ya ukaguzi, hatua ambayo italeti ufanisi katika kutekeleza majukumu yake lakini pia itaongeza mapato ya Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi. Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi bilioni 12.3 zinaombwa chini ya Fungu 31 – Idara ya Mazingira kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kiasi hicho ni pungufu kwa asilimia 45.7 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, upungufu huu una athari katika fedha za miradi ya maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia 61.3 ukilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilibaini kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na usimamizi wa Mazingira bado hazitoshelezi kukabiliana na changamoto pamoja na uharibifu unaoendelea kujitokeza katika mazingira nchini. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Mazingira na kuupitishia vyanzo vya mapato ili waweze kutekeleza jukumu lao lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira 2019/2020, pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ina Maoni na Ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira ilikuwa ni kuisaidia Serikali katika kuisimamia Sekta Binafsi kuchangia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Mfuko huu umeanzishwa tangu mwaka 2007 lakini ulishindwa kutekeleza majukumu yake mpaka sasa kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya taratibu ikiwepo Sheria ya Mfuko kuhitaji marekebisho pamoja na vyanzo vya mapato ya mfuko. Kamati inaisisitiza Serikali kuharakisha zoezi hili na katika mwaka wa fedha 2020/2021, mfuko uanze kutekeleza majukumu yake. Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi wa ruzuku za Serikali katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazingira ni suala mtambuka na ustawi wake una manufaa kwa sekta mbalimbali. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni Mratibu Mkuu wa masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Katika kutekeleza jukumu hili, husimamia Sheria ya Mazingira, kutunga kanuni pamoja na miongozo mbalimbali ambayo inalenga kuwezesha uratibu huo. Kamati inaendelea kusisitiza Wizara, Mikoa, Halmashauri pamoja na Sekta zote nchini kutoa ushirikiano kwa Ofisi hii. Jambo hili lianze kwa kutenga kifungu katika bajeti zao na kukiwekea fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya 2004 kila Halmashauri inapaswa kuwa na Afisa Mazingira ambaye ana jukumu la kusimamia shughuli za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Halmashauri husika. Changamoto iliyopo ni kuwa Maafisa hawa wapo lakini hawana taaluma ya mazingira, jambo ambalo huwapelekea kutotekeleza majukumu yao kwa weledi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya ajira za Maafisa Mazingira katika Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa lengo la kuhakikisha wana taaluma ya Mazingira. Hatua hizi zitasaidia katika utekelezaji wa masuala yanayohusu mazingira na kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kwa siku za usoni kuangalia namna ya kuwahamisha Maafisa Mazingira wote kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Hatua hii itasaidia uratibu wa shughuli za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambapo kwa sasa Maafisa hao wanaripoti kwa Mkurugenzi wa Halimashauri na siyo kwa Mkurugenzi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado jamii ina uelewa mdogo juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira jambo linalopelekea kuendesha shughuli zao za maendeleo ikiwepo ujenzi, kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na kadhalika, bila kuzingatia Sheria za Usimamizi wa Mazingira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu Rais, Mazingira kirasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia Watanzania wengi zaidi na kuwapatia elimu ya Uhifadhi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imelipa Baraza la Uhifadhi wa Mazingira majukumu ya kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria za Mazingira katika nyanja kuu nne ambazo ni kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa mazingira; kusimamia mchakato wa tathmini ya athari za mazingira; kuwezesha ushiriki wa Umma katika kufanya maamuzi yanayohusu

mazingira; na kusimamia kwa ujumla mambo yote yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Baraza kupewa dhamana hii kubwa lakini kuna baadhi ya maamuzi ni lazima yafanywe na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 yanakayopelekea Baraza kupewa mamlaka kamili, badala ya kuwa Baraza iwe Mamlaka ya Taifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Hatua hii itatoa mamlaka kamili ya kusimamia masuala ya Mazingira na pia tutampunguzia Waziri majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili liende sambamba na kuliwezesha Baraza kupata rasilimali watu, fedha na vitendea haki kwa lengo la kulipa uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa nishati mbadala, imeripotiwa katika taarifa ya tatu ya hali ya mazingira mwaka 2018 kuwa kuna ukataji holela wa misitu ambapo takribani hekta 469,420 zinapotea kila mwaka na kiasi kikubwa cha misitu kinakatwa kwa ajili ya kuni na mkaa. Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu katika kusimamia matumizi, uvunaji endelevu wa misitu yetu. Jambo hili liende sambamba na kuwahamasisha wadau kupanda miti na kusimamia.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uzalishaji wa mkaa mbadala na gesi ili kuongeza nishati mbadala jambo linalopelekea kupunguza ukataji wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuendeleza kuliongoza Bunge letu kwa weledi katika kipindi chote hiki cha uhai wa Bunge hili la 11 kwa dhati na moyo wangu wote na kwa niaba ya Kamati yangu nikupongeze sana wewe mwenyewe Ofisi ya Bunge kupitia Katibu wa Bunge kwa kutuwekea utaratibu wa kutumia Bunge Mtandao

jambo linaloturahisishia utendaji wa kazi katika Kamati na Bunge kwa ujumla tunakupongeza sana

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wamewezesha kutoa maoni, michango na mawazo ya hapa nyumbani wakati wa kupitia na kuchambua bajeti na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii majina yao naomba yaingie kwenye kumbukumbu ya taarifa rasmi za Bunge kama yalivyosomeka kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima Mbunge, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kutoa ufafanunuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kufikia kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira Fungu 31 Idara ya Mazingira kwa mwaka 2020/2021 ambayo ni kiasi cha shilingi bilioni 12,327,852,440 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA
MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)
FUNGU 31 – IDARA YA MAZINGIRA KWA MWAKA 2019/2020
PAMOJA NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA MWAKA 2020/2021 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka **2019/2020** na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili kwa Mwaka Fedha **2020/2021**.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilizingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka wa Fedha **2019/2020** pamoja na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha **2020/2021** kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa maelezo ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha; Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Taarifa hizo.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA 2019/2020.

2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

2.1.1 Mapitio ya Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta, kutumia siku zisizozidi saba kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo, ili kuziwezesha kufanya ulinganisho wa utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na maombi mapya ya wizara husika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, iliidhinishiwa shilingi **18,218,915,442.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la ukaguzi wa miradi, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli za Baraza la taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira () katika maeneo mawili ambayo ni;-

i) Shughuli za Usimamizi wa Mazingira katika Mradi wa Ujenzi wa Reli kwa kiwango cha "**Standard Gauge**" – Dar es Salaam; na

ii) Shughuli za Usimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Uzalishaji wa Umeme wa Gesi – Kinyerezi Dar es Salaam.

a) Shughuli za Usimamizi wa Mazingira katika Mradi wa Ujenzi wa Reli kwa kiwango cha “Standard Gauge” – Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Machi, 2020, Kamati ilitembelea mradi wa Ujenzi wa Reli kwa kiwango cha “Standard Gauge” kutokea Dar es Salaam mpaka Makutopora Wilayani Manyoni, Mkoani Singida. Lengo la Kamati kutembelea mradi huu, ilikuwa ni kukagua na kuona namna utekelezaji wa mradi unavyoendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usimamizi wa Mazingira. Lakini pia kubaini namna Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wanatekeleza jukumu la kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usimamizi wa Mazingira katika miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwemo mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuwa Mradi ulipata Cheti cha Mazingira mwezi Mei, 2019. Mradi huu pia umekwisha tembelewa kwa mara tatu (3) na Maafisa wa Baraza ili kuweza kujiridhisha kama mmiliki wa Mradi ambaye ni Shirika la Reli Tanzania (TRC) anazingatia maagizo/maelekezo ya kimazingira yaliyopo kwenye cheti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa changamoto za kimazingira zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na ukataji wa miti ya asili; mmomonyoko wa ardhi katika ushoroba wa Reli; kuwepo kwa mashimo maeneo mbalimbali yaliyotokana na uchimbaji wa vifaa vya ujenzi kama mawe, kokoto na udongo; na Kukosekana kwa mpango maalum wa kudhibiti taka ngumu na taka maji katika maeneo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zilikuwa zimekwisha bainishwa na Baraza wakati wa kufanya Tathimini ya Athari za Mazingira – TAM katika mradi huu na Cheti cha Mazingira kilichotolewa kilibainisha mambo ya kuzingatia ya Kimazingira

na Kijamii wakati wa uendeshaji wa mradi (Specific Conditions);

Mheshimiwa Spika, Cheti cha Mazingira kilimuagiza TRC kuhakikisha kuwa na mpango wa kupanda miti na kuimarisha kingo za tuta la reli na kingo za milima iliyochoyongwa kwa ajili ya kupitisha njia ya reli; kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kudhibiti taka ngumu na taka maji wakati wa utekelezaji wa mradi; vilevile, kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kukarabati maeneo yaliyochukuliwa vifaa vya ujenzi (Udongo, kokoto na mawe) kabla ya kukabidhi mradi huo kwa serikali;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kutembelea eneo la Mradi kuanzia kituo Posta Stesheni mpaka kituo cha Pugu, hivyo, kushuhudia shughuli mbalimbali za mradi zikiendelea na kuona jitihada wanazozifanya TRC katika kuzingatia maelekezo ya cheti cha mazingira ikiwepo utekelezaji wa kipengele cha kulinda kingo za reli. Kipengele hicho kimezingatiwa kwa kiasi cha kuridhisha ambapo, mkandarasi ametengeneza matuta kwenye kingo za reli na kuyapanda majani kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko.

Mheshimiwa Spika, hali ya mazingira katika eneo la mradi ni yakuridhisha, pamoja na hilo Kamati inalishauri Baraza kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na TRC ili kuwapatia ushauri stahiki na kwa wakati wa kimazingira kwa lengo la kuendelea kulinda mazingira yetu. Mfano kwa sasa TRC imetekeza ushauri wa _____ wa kuweka mitaro pembezoni mwa mradi lakini mitaro hiyo inaonekana kuwa ni midogo na kuwa itashindwa kuhimili endapo itatokea mvua kubwa. Jambo hili lingetatuwa mapema kama NEMC wangekuwa muda wote wa mradi na kuwashauri waendesha mradi juu ya kipimo cha mitaro ya maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukuta hali shwari ya mazingira, Kamati inaomba kuisisitiza TRC kufuata maelekezo/maagizo yaliyopo katika Cheti cha Ukaguzi wa Mazingira kwa lengo la kulinda mazingira yanayozunguka mradi lakini pia kuleta tija ya mradi huo;

b) Shughuli za Usimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Uzalishaji wa Umeme wa Gesi – Kinyerezi Dar es Salaam;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi 1 – Dar es Salaam, kwa lengo la kukagua na kuona namna uendeshajiwa mradi unavyozingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, kuwa Mradi wa Kinyerezi 1 ulipata cheti cha mazingira mwezi Aprili, 2012. Pia umekwisha tembelewa na Maafisa wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) mara tano (5), kwa lengo la kujiridhisha kama utekelezaji wake unazingatia maangalizo/maelekezo ya Mazingira yaliyopo kwenye cheti cha Mazingira walichopewa. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu unajumuisha ujenzi wa kituo cha umeme kwa ajili ya Treni ya Umeme wa SGR na Njia ya umeme wenye msongo wa 220kV kutoka Kinyerezi hadi Morogoro ambao Kamati pia imeutembelea.

Mheshimiwa Spika, Cheti cha Mazingira kilichotolewa na NEMC kilielekeza mambo mbalimbali ya kuzingatia kwenye mradi huo, kwa lengo la kulinda mazingira yetu. Hatua zilizoripotiwa kwa Kamati juu ya utekelezaji wa masharti/maelekezo ya Cheti cha Mazingira ni kuwa Mradi umeandaa Mpango maalum wa kusimamia taka hatarishi, taka ngumu na maji upo na unatekelezwa vizuri; utekelezaji wa Mradi umehakikisha kuwa katika eneo la ushoroba wa msongo wa umeme ni miti pekee ndio inakatwa na kuruhusu majani kuota ili kupunguza athari za mmomonyoko wa ardhi. Mambo haya mawili ndio changamoto kuu zilizosisitizwa katika cheti cha Mazingira cha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauri muendeshaji wa Mradi aendelee kutekeleza masharti yaliyoainishwa katika Cheti cha Mazingira, lakini pia imeisitiza NEMC kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika mradi huo ili kuhakikisha masuala

ya mazingira yanazingatiwa lakini pia kutoa ushauri wa kitaalamu pindi jambo la kimazingira linapotokea.

2.1.2 Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

i) Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira iweke utaratibu wa kuweka Afisa wa NEMC katika kila Mradi wa Maendeleo unaotekelezwa kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu wa Mazingira wakati wote wa utekelezaji wa Mradi. Jambo hili litawezesha hatua zote za mradi kuzingatia masuala ya Mazingira;

ii) Baada ya Mradi kukamilika NEMC iwezeshwe kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha masuala waliyokubaliana katika Cheti cha Mazingira bado yanazingatiwa.

2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika uchambuzi huo, Kamati ilitumia matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Mazingira, taarifa zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati pamoja na mahojiano wakati wa vikao vya Kamati. Lengo likiwa ni kujiridhisha kuhusu ukusanyaji wa mapato, utekelezaji wa malengo/kazi na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

2.2.1 Makusanyo ya Mapato

Mheshimiwa Spika, hakuna mapato yanayokusanywa Chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, lakini Baraza la Taifa la

Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – ambalo lipo chini ya Ofisi hii hufanya makusanyo kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza ambapo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Baraza lilipanga kukusanya Shilingi **21,697,273,657.00**. Hivyo, Kamati imepewa taarifa kuwa, hadi kufikia Machi, 2020, Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi **9,179,894,074.00** kiasi ambacho ni sawa na asilimia **42.3** ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kushuka kwa makusanyo kumechangiwa na kushuka kwa ada na tozo za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) hatua iliyosababishwa na maboresho yaliyofanywa katika kanuni zinazosimamia mchakato wa TAM.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuliimarisha Baraza kwa kuipatia rasilimali inazohitaji ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, hatua hii itasaidia kuongeza uwezo wa Baraza kuhudumia wadau wengi zaidi na wanya, jambo ambalo litaongeza mapato ya Baraza lakini pia itasaidia kuongeza kasi katika usimamizi wa uhifadhi wa mazingira Nchini.

2.2.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **22,713,554,988.00** kwa ajili ya matumizi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kati ya fedha hizo Shilingi **4,494,639,546.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **18,218,915,442.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambazo ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, kiasi cha shilingi **5,441,789,390.79** kilikuwa kimepokelewa, kiasi hiki ni sawa na asilimia **23.9** ya fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-
i) Kiasi kilichopokelewa ni pungufu kwa asilimia **76.1**, kwa kipindi hiki cha robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha ambapo

ilikuwa itarajiwa zaidi ya asilimia **75** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge ziwe zimepokelewa; na

ii) Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha una madhara zaidi kwa upande wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, ambapo Shilingi **2,929,865,814.35** sawa na asilimia **16.08** ya fedha ndio zilizotoka, kati ya fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo ulitokana na kuwa, Miradi mitatu (3) kati ya miradi iliyotengewa fedha katika mwaka 2019/20 fedha zake kutopokelewa kutokana na kutokamilika kwa majadiliano kati ya Serikali na Wafadhili. Kamati inaisisitiza Serikali (Wizara ya Fedha) kulipa uzito suala hili na kukamilisha majadiliano hayo ili fedha zipokelewe na miradi husika ianze kutekelezwa haraka iwezekanavyo.

2.2.3 Utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuhusu utekelezaji wa kazi za Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha **2019/2020**. Jumla ya kazi Kumi na Sita (16) zilipangwa kutekelezwa na taarifa ya Ofisi hii ilibainisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kazi za uhifadhi na usimamizi wa mazingira zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha **2019/2020**, zimetokelezwa. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuongeza juhudi katika majukumu yafuatayo;-

i) Kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira 1997 na mkakati wa utekelezaji wake kwa lengo la kuihuisha iendane na mazingira halisi ya sasa na iweze kuboresha usimamizi wa shughuli za mazingira;

ii) Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa kudhibiti Viumbe vamizi (Invasive Alien Species) kwa lengo la kuokoa maisha ya binadamu, mazingira na bioanuai zote kutokana na athari za viumbe vamizi;

iii) Kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza Mazingira, suala hili liende sambamba na kuuelimisha umma juu ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004; na

iv) Kuongeza jitihada katika kutekeleza kampeni za Upandaji na utunzaji wa miti hiyo, hususani katika maeneo ambayo yameathirika sana na ukame.

2.3 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa mwaka wa fedha **2019/2020** Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo katika maeneo lshirini na Moja (21). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza maagizo hayo, hata hivyo kuna maeneo ambayo Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kuyatekeleza, maagizo hayo ni pamoja na;-

i) Serikali iongeze kasi katika kukamilisha mchakato wa kuliingiza Ziwa Manyara katika maeneo Lindwa kwa lengo la kuliweka katika usimamizi maalum na kulitoa katika hatari ya kupotea. Mchakato huo uhusishe maziwa yote ambayo yapo katika hatari ya namna hii ikiwepo Ziwa Jipe na Chala;

ii) Serikali iongeze kasi ya kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira, pia kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za asili husasani misitu na vyanzo vya maji;

iii) Serikali ihakikishe kuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mfuko wa Mazingira unawezeshwa na kuanza kufanya kazi kikamilifu;

iv) Sheria ya Mazingira imemtambua na kumpa majukumu makubwa Afisa Mazingira ya usimamizi wa Mazingira, lakini Afisa huyo ni muajiriwa wa Halmashauri na anaripoti kwa Mkurugenzi wa Halmashauri badala ya kuripoti kwa Mkurugenzi wa Mazingira. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuona haja ya kupunguza mlolongo uliopo badala yake Afisa Mazingira awe anaripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa masuala yote yanayohusu mazingira.

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

3.1 Uchambuzi wa malengo/mpango

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi mazingira, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha **2020/2021** kwa lengo la kufuatilia tija inayoweza kupatikana ikihusianishwa na fedha zinazoombwa katika kifungu **5003**. Kamati ilibaini kuwa Malengo yote yalizingatia hati idhini ya Serikali iliyoainisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilirizishwa na malengo pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati imeishauri Serikali kuiwezesha kiukamilifu Ofisi hii kutekeleza malengo yake iliyojipangia kiukamilifu.

3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya mapato

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/2021, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanywa Chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, lakini Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – ambalo lipo chini ya Ofisi hii linalenga kukusanya jumla ya Shilingi **24,097,697,647.00** kutoka katika vyanzo vya ndani vya Baraza ambavyo ni ada na faini zitokanazo na shughuli za usimamizi wa mazingira.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kinacholengwa kukusanywa kimeongozeka kwa asilimia **9.9** ukilinganisha na malengo ya makusanyo ya Baraza ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambalo yalitekelezwa kwa asilimia **42.3** tu hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutambua wigo wa mapato yatokanayo na shughuli za Mazingira, lakini pia kulinganisha Baraza uwezo kwa kuwapatia watumishi na vitendea kazi ili waweze kuongeza kasi ya ukaguzi, hatua ambayo italetu ufanisi katika kutekeleza majukumu yake lakini pia itaongeza mapato ya Baraza.

3.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi **12,327,852,440.00** zinaombwa chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira. Mchanganuo wa fedha hizo ni Shilingi **5,278,422,440.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,049,430,000.00** ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa;-

i) Kiasi hicho ni pungufu kwa asilimia **45.7** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020; na

ii) Upungufu wa Bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 unaathari katika fedha za Miradi ya Maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia **61.3** ukilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na usimamizi wa Mazingira bado hazitoshelezi kukabiliana na changamoto pamoja na uharibifu unaoendelea kujitokeza katika mazingira Nchi. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Mazingira na kuupitishia vyanzo vya mapato ili weze kutekeleza jukumu lililokusudiwa.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

4.1 Hali ya Mazingira

Mheshimiwa Spika, hali ya Mazingira nchini iliyoripotiwa ndani ya taarifa ya Tatu ya hali ya Mazingira ya Mwaka 2018 inatia mashaka, imeripotiwa kuwa Asilimia 61 ya ardhi nchini ipo kwenye hatari ya uharibifu mkubwa unaohusisha uharibifu wa udongo na uwepo wa chumvi ardhini vinavyosababishwa na matumizi mabaya ya kemikali; kuna ukataji holela wa misitu unaosababishwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu, ambapo takribani hekta 469,420 zinapotea kila mwaka huku Tanzania imeripotiwa kuwa nchi ya tano Afrika inayoongoza kwa kukata misitu.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyoripotiwa kwenye taarifa hiyo ni kuna ongezeko la viumbe vamizi, ambapo athari zake zimekwishaonekana katika Sekta ya kilimo kwa kuharibu mazao mengi ikiwepo mahindi; pia kuna udhibiti mbovu wa taka ngumu, hivyo kusababisha kuzagaa kwa taka hizo; na Utiririshaji wa majitaka ya viwandani umeendelea na kusababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa uharibifu wa mazingira nchini, Kamati inaona kuna ulazima kwa Serikali kuandaa mipango madhubuti na mahsusni ya kuhifadhi na kuyalinda mazingira yetu.

4.2 Maoni na Ushauri

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira 2019/2020, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ina Maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali;-

i) Mfuko wa Mazingira

Mheshimiwa Spika, dhana ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira ilikuwa ni kuisaidia Serikali katika kuisimamia Sekta

Binafsi kuchangia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Mfuko huu umeanzishwa tangu mwaka 2007 lakini unashindwa tekeleza majukumu yake mpaka sasa kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya taratibu ikiwepo Sheria ya Mfuko kuhitaji marekebisho pamoja na vyanzo vya mapato vya mfuko. Kamati inaisisitiza Serikali kuharakisha zoezi hili na katika mwaka wa fedha 2020/2021, mfuko uanze kutekeleza majukumu yake. Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi wa ruzuku toka Serikalini katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira.

ii) Wajibu wa Wizara na Sekta zote nchini kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mazingira ni suala mtambuka na ustawi wake una manufaa kwa sekta mbalimbali, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ni mratibu mkuu wa masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na katika kutekeleza jukumu hili husimamia Sheria ya Mazingira, kutunga Kanuni pamoja na miongozo mbalimbali ambayo inalengwa kuwezesha uratibu huo. Kamati inaendelea kusisitiza Wizara, Mikoa, Halmashauri pamoja na Sekta zote nchini kutoa ushirikiano kwa Ofisi hii, jambo hili lianze kwa kutenga kifungu katika bajeti zao na kukiwekea fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mazingira ya 2004.

iii) Afisa Mazingira

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya 2004 kila Halmashauri inapaswa kuwa na Afisa Mazingira ambae anajukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa Mazingira katika Halmashauri husika. Changamoto iliyopo ni kuwa maafisa hawa wapo lakini hawana taaluma ya mazingira jambo ambalo huwapelekea kutotekeleza majukumu yao kwa weledi uliokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya ajira za maafisa mazingira katika Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa lengo la kuhakikisha wanataaluma ya mazingira hatua hii itasaidia katika utekelezaji wa masuala yanayohusu mazingira na kuleta tija.

Pia, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kwa siku za usoni kuangalia namna ya kuwahamisha maafisa mazingira wote kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, hatua hii itasaidia uratibu wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira ambapo kwa sasa maafisa hao wanaripoti kwa Mkurugenzi wa Halimashauri na si kwa Mkurugenzi wa Mazingira.

iv) Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

Mheshimiwa Spika, bado jamii inaelewa mdogo juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira jambo linalopelekea kuendesha shughuli zao za maendeleo ikiwepo ujenzi, kilimo, ufugaji, uchimbaji madini n.k, bila kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu Rais-Mazingira kirasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia watanzania wengi na kuwapatia elimu ya Uhifadhi wa Mazingira.

v) Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira- NEMC.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mazingira ya 2004 imelipa Baraza la uhifadhi na usimamizi wa Mazingira majukumu ya kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya mazingira katika nyanja kuu nne ambazo ni kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa mazingira; kusimamia mchakato wa tathimini ya athari za mazingira; kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya maamuzi yanayohusu mazingira; na kusimamia kwa ujumla mambo yote yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Baraza kupewa dhamana hii kubwa lakini kuna baadhi ya maamuzi ni lazima yafanywe na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya Mazingira ya 2004 yatakayopelekea Baraza kupewa mamlaka kamili, badala ya kuwa Baraza iwe Mamlaka ya Taifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, hatua hii itaipaa mamlaka kamili ya

kusimamia masuala ya Mazingira na pia tutampunguzia Waziri majukumu.

Mheshimiwa Spika, Jambo hili liende sambamba na kuliwezesha Baraza kupata rasilimali watu, fedha na vitendea kazi kwa lengo la kulipa uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kwa ufanisi.

vi) Upatikanaji wa Nishati mbadala

Mheshimiwa Spika, imeripotiwa katika Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2018, kuwa kuna ukataji holela wa misitu ambapo takribani hekta 469,420 zinapotea kila mwaka na kiasi kikubwa cha misitu kinakatwa kwa ajili ya KUNI na MCAA. Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kusimamia matumizi/uvunaji endelevu wa misitu yetu, jambo hili liende sambamba na kuhamasisha wadau kupanda miti na kuisimamia. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uzalishaji wa mkaa mbadala na gesi ili kuongeza nishati mbadala jambo litakalopelekea kupunguza ukataji wa mti.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa katika kipindi chote hiki cha uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira nikupongeze sana wewe mwenyewe, Ofisi ya Bunge kupitia Katibu wa Bunge kwa kutuwekea utaratibu wa kutumia Bunge Mtandao jambo lililoturahisishia utendaji kazi katika Kamati na Bunge. Tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyevidi wa Bunge kwa

kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini:-

i. Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	Mwenyekiti
ii. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	M/Mwenyekiti
iii. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
iv. Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb	Mjumbe
v. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
vi. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
vii. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
viii. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
ix. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
x. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
xi. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xii. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xiii. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xiv. Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xv. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xvi. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xvii. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xviii. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xix. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xx. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xxi. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
xxii. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais-Muungano na Mazingira, Mhe. Mussa Azan Zungu, Mb, Naibu Waziri wake Mhe. Mussa Ramadhan Sima, Mb, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhan pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa nallomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka wa Fedha **2019/2020** ambayo ni kiasi cha Shilingi **12,327,852,440.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)

MWENYEKITI

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA
NA MAZINGIRA**

16 Aprili, 2020

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea mambo matatu. La kwanza mnakumbushwa kuendelea kupiga kura kwa sababu Mtandao umeshawezeshwa ili muweze kupiga kura.

Jambo la pili ni taarifa ambayo ilibidi isomwe hapa hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni mtakumbuka siku ya tarehe 01 Mheshimiwa Spika wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akisoma taarifa ya akisoma bajeti kwa maana ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake alitoa maelekezo kuhusu taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani na akaeleza kwamba wakati mwingine pengine atalazimika kutoa maamuzi kwamba isisomwe kabisa kama ikionekana inaenda tofauti na utaratibu wetu wa Bunge.

Sasa taarifa niliyonayo hapa mbele Waheshimiwa Wabunge na mtaona kwenye Mtandao pia haijawekwa kwa sababu ukiitazama kuanzia ukurasa wa pili mambo yaliyoandikwa humo sitayarejea kwa sababu nitakuwa na maimi nayaweka kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge mpaka ukurasa, taarifa yenyewe ina kurasa 19 lakini kurasa 14 kati ya hizo haziwezi kusomwa kwa sababu zinaenda kinyume na utaratibu wetu.

Kwa maana hiyo hata hizo kurasa chache zilizobaki ambazo zingeweza kusomwa zitakosa mukelele wa kuonesha ni kitu gani hasa kilitaka kusemwa. Kwa muktadha huo taarifa hii haitasomwa kwa mujibu wa maelekezo aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 01 mwezi wa 04.

Kwa maana hiyo tumeshamaliza mawasilisho ninayo majina hapa kutoka kwenye vyama vinavyowakilishwa hapa Bungeni kuhusu uchangiaji nitawasoma Waheshimiwa Wabunge ambao wanatakiwa kwenda kuwa Msekwa kwa sababu watachangia kutokea kule na nawaona wako humu ndani, kwa hiyo nitawasoma ili waende huko halafu tutaendelea na uchangiaji.

Mheshimiwa Ibrahimu Raza atachangia kutokea Msekwa, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atachangia kutokea Msekwa, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa atachangia kutokea Msekwa, Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar atachangia kutokea Msekwa, Mheshimiwa Kubenea atachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Ally Saleh yuko tayari Msekwa atachangia kutokea huko, hao ndio Waheshimiwa watachangia kutokea Msekwa wengine ambao orodha yao iko hapa watachangia kutoka hapa Bungeni. Kwa hivyo tutaanza uchangiaji na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwana Mheshimiwa Tauhida Cassian Nyimbo.

Mheshimiwa Fakharia kabla hujaanza kuchangia naona Mheshimiwa Esther Bulaya amesimama. Mheshimiwa Esther Bulaya.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kiti chako kimetoa maamuzi kwamba hotuba yetu isisomwe lakini hukusema hotuba yetu imekiuka Kanuni ipi na ni mambo gani hasa ambayo kiti chako kimeona yamekiuka taratibu za Bunge. Sasa kwa ajili ya kuweka sawa kiti kinapotoa maamuzi kwamba hii hotuba haisomwi kwa maelekezo kadhaa yale maelekezo yalikuwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tulitarajia sasa umetoa maamuzi leo utuambie hotuba hii imekiuka Kanuni moja, mbili, tatu ili sisi pia kama Kambi tujiridhishe sio tu kiti kinatambia hotuba hii haisomwi kwa sababu ya maelekezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Spika, maelekezo yake aliyatoa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hakutoa kwenye hotuba ya Makamu wa Rais. Sasa leo wewe ndio unatoa maelekezo utuambie tumevunja Kanuni gani ili na sisi tupitie hiyo hotuba tujiridhishe ili sasa tusije ikajirudia huko kwingine kwa sababu inawezekana ni tafsiri tu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimelazimika kusimama tena kwa sababu kwa Kambi Rasmi ya Upinzani amesimama kuhusu jambo ambalo nimelisema hapa mbele. kwa taratibu zetu za kikanuni kwa sababu nimeshatoa maamuzi kama kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye hakubaliani nayo Kanuni ya 5 inatoa maelezo ya namna ya kufanya huwezi kukihoji tena kiti baada ya kutoa maelezo, ndio utaratibu uliopo kikanuni kama hujakubaliana na maelezo ama mwongozo uliotolewa unachukua hatua kwa mujibu wa Kanuni ya 5 haukirudii tena kiti kukihoji kuhusu maamuzi ambayo kimetoa.

Hata hivyo Mheshimiwa Spika wakati akitoa maelezo ama wakati akitoa maelekezo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya tarehe 01 alitoa maelezo kuhusu hotuba ile ya Kambi Rasmi ya Upinzani na alitoa maelekezo ya jumla kuhusu hotuba zitakazofuata. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndio maana huwa tunakumbushwa siku zote kuwa wasikivu ili tuwe wote tunaenda kwa pamoja. Kwa hiyo, huo ndio uamuzi wa kiti kuhusu taarifa ya leo ya kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo na huo ndio utakuwa muongozo wa mwisho Waheshimiwa Wabunge.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimekusikiliza vizuri lakini nakumbuka hata siku ambapo Mheshimiwa Spika ametoa hotuba yetu bado alitungeza muda alitupa muda ule ambao tulipaswa kuchangia au kuzungumza. Kwa hiyo, nilikuwa naomba muongozo wako kama kwa muda huu ambao nafasi yetu haitasomwa basi tupewe walau wachangiaji ili tuweze kufidia muda huu ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge huo sidhani kama ni mwongozo ni ombi kwa sababu kikanuni mwongozo ni kama unataka kujua jambo lililofanyika linaruhusiwa au haliruhusiwi ndio Kanuni yetu ya 68 inavyosema. Hili alilolita Mheshimiwa Suzan Lyimo ni ombi ambalo halihitaji nisimame hapa ili niweze kulitolea maelekezo. Kwa hiyo, kama ana ombi ataandika na atatumia utaratibu wa kawaida ambao hauhitaji yeye kusimama. Tutaendelea na wachangiaji Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss, Mheshimiwa Ibrahim Raza kutokea Msekwa ajjandae.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kunipa uzima na afya njema. Sina budi kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuhairisha sherehe ya Muungano na sherehe ya Mei Mosi kutokana na gonjwa hili la Corona. Hili ni jambo kubwa na jambo zuri kwa Mheshimiwa Rais wetu kulifikiria na kuwa na hona nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile sina budi kumshukuru kwa kuchumua milioni 500 za sherehe za

Muungano kuzipeleka Zanzibar kwa ajili ya kuchangia gonjwa la Corona. Mheshimiwa Rais ahsante sana na hongera kwa kutupatia pesa hizo ambazo zitasaidia Zanzibar na tutazidi kudumisha Muungano wa Zanzibar na hilo Wazanzibar hatuna la kukulipa isipokuwa Oktoba 2020 kura zote wa Wazanzibar kwenye sanduku la Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija pia nachangia nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara Zanzibar na ameitembelea Zanzibar ameangalia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ameangalia shughuli za Muungano nakupongeza Mheshimiwa na huo ndio Muungano na hivyo ndivyo inavyotakiwa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu kutembelea Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuwa na ombi dogo tu nilikuwa nataka niliombe wakati anapofanya ziara Zanzibar baadhi ya Waheshimiwa Wabunge anakuwa hatuoni asione kwamba hatuoni hatutaki, tunakuwa taarifa hatuna tunasikia wakati anaondoka au yuko kwenye . Sasa uzuri anapokuwa anakuja Zanzibar angetoa taarifa katika Ofisi yetu ya Zanzibar au Ofisi ya Makamu wa Rais ili yeye angeweza kuratibu tukaweza kupatikana Waheshimiwa Wabunge. Tunapenda tukupokee, tunapenda tuwe na wewe katika ziara, tunapenda ukiondoka tukusindikize na baadhi ya kati tukae tunong'one na wewe wakati sisi tuko Zanzibar. Nafikiri hilo kwetu sisi Wabunge litazidi kutusaidia maana taarifa zikifika SMZ inakuwa sisi Wabunge hatuzipati lakini nilivyokuwa Ofisi za Muungano zipo tungeomba taarifa zetu zifike huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuizungumzia Ofisi ya Makamu wa Rais, ofisi ya Makamu wa Rais inafanya kazi nzuri mwenyewe nilikuwa ni mfanyakazi Ofisi ya Makamu wa Rais na kipindi hicho kilikuwa kigumu hakuna vitendea kazi, hatuna ofisi, hatuna magari kila kitu tukitegemea SMZ. Lakini sasa Ofisi ya Makamu wa Rais ina jengo lake la ofisi, ina nyumba yake anayotumia Mama, ina magari yake, ina ofisi

yake ambayo inajitegemea. Zamani ilikuwa haijitegemei sasa inajitegemea Zanzibar majukumu yao yote wanayafanya kwa weledi, Mama hongera endelea kufanya kazi zako nzuri na nina hakika wafanyakazi uliokuwa nao wazuri nimefanya kazi nao na ninawajua na wana uwezo wa kazi na wataweza kukusaidia hongera Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilita nikupongeze Makamu wa Rais, kwa ziara za mara kwa mara Zanzibar unaitembelea Unguja, unatembelea Pemba, unachangia Unguja unaangalia Ilani ya chama pamoja na Muungano wake vipi unaimarika hongera Mama kwa sababu baadhi ya Majimbo umeyasaidia mfano Jimbo la Jang'ombe, Jimbo la Kikwajuni na Majimbo mengine ya Unguja na Pemba na hilo ndilo tunalolipenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hongera kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakuamini, baadhi ya ziara zake za kikazi anakutuma unakwenda unatekeleza na unarejea unaleta merejesho wenye utekelezaji mahiri Makamu wa Rais hongera kwa kazi na tunakutakia kila lenye kheri na Mwenyezi Mungu atakujalia urejee tena mara ya pili katika nafasi hiyo kwasababu wanawake tuko pamoja na wewe Makamu wa Rais na Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sina budi kumshukuru na Mheshimiwa Waziri wa Muungano Mheshimiwa Zungu ulikuwa Mwenyekiti wangu Kamati ya Mambo ya Nje tumefanya kazi na wewe vizuri umahiri na uwezo wako tunaujua na hapo ulipowekwa ndipo hasa panapokufaa kwa kazi zako na baada ya kufika umekwenda Zanzibar umetembelea Unguja, umetembelea Pemba umeonana na Mheshimiwa Rais na umeweza kuangalia nini kinacholeta maslahi kwa Muungano na nini kinacholeta matatizo na katika hotuba yako umeyazungumza yotekwa sababu hii kazi ulikuwa umeshaifanya, lazima nikupe hongera na uendeleo na ufanye kazi vizuri na wafanyakazi Ofisi ya Makamu wa Rais hawana matatizo watakuwa na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kuzungumzia Corona. Naizungumzia Corona kwa sisi Viongozi. Wizara ya Muungano Afya na Wizara ya SMZ Afya wanafanya kazi nzuri ambapo wanashirikiana na huu ndio Muungano unavyotaka. Sisi Viongozi baada ya kuisaidia Wizara kuisaidia na Serikali kazi yetu sisi kubeza ili kile kinachofanyika kama hatukioni na wakati kizuri, wakati mimi kama Mbunge natakiwa nijiongeze katika wapiga kura wangu jinsi ya kuweza kupokea maagizo ya Serikali, maagizo ya Wizara ya Afya sio kubeza yale yanayotakiwa wakati wewe ndio kiongozi kama ni kioo cha jamii, wewe ndio ufanye kazi kuisaidia Serikali, wewe kama kuna udhaifu uweze kuzungumza onana na viongozi wape taarifa sio tu ukae kwenye mitandao au tukae tunabeza wakati wewe hufanyi chochote na wakati wewe kiongozi unatakiwa wewe usimame imara

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kwa wapiga kura wako kama kuna vitu vingine Serikali imeshindwa wewe saidia kutoa ili hawa watu wetu wapiga kura wetu waweze na wao kujisikia kwamba na Wabunge wao au wawakilishi wao au viongozi wao na wamo katika hili janga kwa sababu hili janaga si la Tanzania janga la dunia na sote tunakiwa kulisimamia imara na sisi viongozi ndio hapo tunakiwa hata humu ndani hatuoni Mheshimiwa Spika alivyotupanga wengine tuko huku wengine ili analianguka janga likoje. Wakati tunaambiwa tusiende kwenye sehemu za starehe utakuta tunaenda, kwenye sehemu za kilevi tunaenda, sasa tuweze kujikataza sisi kwanza viongozi ili baadaye tuweze kusimamia kuwakataza na wapiga kura wetu ili hali halisi...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss atafuatiwa na

Mheshimiwa Ibrahimu Raza atakayechangia kutokea Msekwa, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi ajiandae.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Muungano. Kwanza kabisa ka jinsi ya kipekee nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vilevile nimpongeze Mama yetu Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi ya kipekee niwashukuru kwa muda wa miaka mitano wameiongoza Tanzania wameiongoza vyema wameitendea haki wamewafanyia Watanzania yale mahitaji ambayo wao wanatarajia kuyapata kutoka kwa Viongozi wao, niendeleo kuwashukuru na sisi kama viongozi wenzetu neno kubwa la kuwaambia hatuna neno ahsante hata tulizungumze kwa lugha gani bado litabaki kuwa ahsante lakini kwa jinsi ya kipekee tuwaambie tunawaombea Dua usiku na mchana Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya njema, Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa hekima viongozi wenzetu, viongozi wetu ili muweze kuipeleka Tanzania mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati huu tuliokuwa nao lazima tuzngumzie haya maradhi hayachagui jinsia, nchi wala rangi. Niseme kwamba tuwashukuru viongozi wote kwa pamoja kwanza kabisa Marais wetu, lakini pia kwa jinsi ya kipekee Mawaziri wa Afya wa Serikali zote mbili, Dada yangu Mheshimiwa Umy na Naibu wake lakini vilevile nimshukuru Waziri wa Afya wa Zanzibar na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Jitihada kubwa tumeziona kwa viongozi hao wakichukua jitihada kuhakikisha Tanzania tunaweza kujikinga au kupunguza kasi ya maambukizi ya ndani ya Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hili kwa umuhimu mkubwa, tumshukuru Rais wetu baada ya kuahirisha sherehe zote mbili aliamua kwa makusudi kuchukua kiasi cha fedha milioni 500 kupeleka Zanzibar kwa kuwekeza kwa ajili ya suala la Hili tunasema ahsante na tunaamini kwamba bado liko mikononi mwa viongozi na bado wanaendelea kulifanyia kazi zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee niishukuru Serikali yangu; mambo mengi ambayo tulikuwa tukisimama kama Wabunge tukisema hizi ni changamoto za Muungano. Sisi mtu akizungumza kwamba kero huwa hatumfahamu, kuna tofauti ya kero na tofauti ya changamoto, sasa changamoto huwezi kuziita kero. Zilizopo ni changamoto, hakuna kero ndani ya Muungano, unapozungumza ndani ya Muungano kwamba kuna kero sisi hatuzifahamu tunaelewa changamoto. Ndani ya jambo lolote, mahali popote changamoto ni jambo la kawaida, lakini niseme leo nimesimama hapa, Mwenyezi Mungu kanijaalia kwa kipindi hiki ni miaka minne na nusu sasa niko ndani ya Bunge, kwa asilimia zaidi ya 85 changamoto za Muungano zimepungua na takribani nina uwezo wa kusema kwamba zinakaribia kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya changamoto 12 zimeweza kutatuliwa, lakini baadhi yake tu naweza kuzitaja, sitozitaja zote lakini nitataja baadhi kati ya hizo 12: Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora lakini pale pale kuna utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Vyombo vya Majini, lakini kuna uvuvi wa bahari kuu ambapo kuna masuala mengi ambayo Serikali imekwenda kutatua, pamoja na changamoto ya suala la kodi ya umeme, kuna zaidi ya kero 12. Sasa ukifika muda kwamba sisi tukisimama hapa tukisema tunamshukuru Rais, tukisema tunaishukuru Serikali yetu, kuna watu huwa hawatuelewi; kama unashindwa kushukuru kwa kidogo, utaweza kushukuru kwa kubwa utakalofanyiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya changamoto zilizokuwepo za Muungano, zaidi ya changamoto 12

zimeweza kutatuliwa yaani kwa mimi Tauhida kusimama hapa kwa sasa ninazoziona haraka haraka labda changamoto tatu. Siyo kero kama watu wanavyozungumza, ni changamoto tatu. Sasa kati ya yote yaliyokuwepo tumwambie nini Rais wetu wa Tanzania? Sisi kama Wabunge tukisimama tukisema Rais wetu iko haja ya kuongezwa muda kuna watu nje wanatufikiria tunawaza Wabunge kuongezwa muda, lakini tuseme, Bunge ndiyo lenye kuleta sheria na utaratibu. Tunaweza tukasema Wabunge tunaweza tukabaki na mchakato wa miaka mitano mitano lakini Rais aongezewe muda aifikishe Tanzania kwenye ndoto yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi na yanafanyiwa kazi, lakini nimesema kuna mambo matatu, kati ya matatu, Mheshimiwa Waziri wa Muungano na Naibu wake walichuku moja walitatie kwa haraka; suala la vyombo vya moto; walichukue, walifanyie kazi. Tunatamani sasa kuona kwamba gari yenye _____ ya Zanzibar pia na huku iwe inatembea lakini kwa kuweka utaratibu uliokuwa mzuri. Lichukue hili jambo Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla litawapa faraja zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la afya; suala la afya siwezi kulizungumza siyo la Muungano na kuna mambo wakati ni Muungano hatuwezi kuyakwepesha. Waziri wa Muungano akiwa yupo katikati asimamea vizuri, tunaomba; kuna mambo mengi ya afya kuhusu suala la watoto, lakini takribani suala kubwa Zanzibar ni suala la akinamama hususani kwenye suala la _____ Hospitali yetu ya Muhimbili imepiga hatua kubwa ya kutatua tatizo hili. Tunamwomba Waziri wa Muungano, yeye si Waziri wa Afya afahamu na namwambia kwa sababu yeye ni Waziri wa Muungano, akae kati alisimamie, Dada Ummy nikimwambia hana tatizo. Anaweza akasema atachukua hatua lakini kwake litakwama zaidi, kwamba kuwe na muda kusema kwamba wanapelekwa Madaktari Bingwa kutoka Muhimbili wanakwenda Zanzibar, iwe kwa suala la akinamama, masuala ya uzazi au _____ waende wakaongeze nguvu na ijulikane kwamba kila mwezi Zanzibar inapokea Madaktari Bingwa angalau mara mbili, mara tatu kutoka Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kwamba kila siku tutegemee wageni kwa maana waje na tunawapokea na tunawataka naomba niliweke vizuri, lakini kama kuna Madaktari Bingwa zaidi wako Muhimbili kwa nini tusitumie fursa hiyo Waziri wa Muungano, wakaweka utaratibu wakasema, hawa Madaktari bingwa kwenye eneo liwe la watoto, maradhi ya moyo au masuala ya watoke Muhimbili kwa siku maalum kwa kila mwezi waende Zanzibar. Baadaye kama kuna masuala ya kufanyiwa na mengine ndiyo mtu aandikiwe kuja Muhimbili, lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri sisi viongozi wenziwe ndiyo tunaofua hii shida. Kuna akinamama kila mwezi zaidi ya mara tatu au mara nne anatakiwa kwenda Muhimbili. Anapofika Muhimbili anakwenda kuangaliwa hali yake na kubadilishiwa dawa kitu ambacho tukileta Madaktari watatu au wanne wana uwezo wa kuwahudumia wananchi wa Zanzibar kwa wingi.

Mheshimiwa Waziri...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida kengele ya pili imeshagonga.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ibrahim Raza kutokea Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Emmaculate Sware Semesi na Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum ajiandae.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya kwa kusimama hapa kuchangia hii bajeti ya Muungano na Mazingira

ambayo ni bajeti muhimu sana ambapo kama tunavyojua ni Muungano wa nchi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri Mheshimiwa Azzan Zungu kwa kuwasilisha bajeti nzuri sana na nimpongeze vilevile Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa pia wanayofanya. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza viongozi wakuu wa Nchi, Dkt. John Pombe Magufuli na Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuweza kusimamia Muungano mpaka leo Muungano umekuwa wa kudumu na imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi nyingine kumpongeza Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Balozi Ali Seif kwa kuweza kusimamia changamoto za Muungano. Mimi sitoita kero, nitaita changamoto kwa sababu changamoto ndiyo inatatuliwa na tumeona juhudi kubwa anayofanya Mama yetu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mama Samia kuchukua jitihada pamoja na upande wa pili wa Muungano kutatua changamoto zilizokuwepo na sisi baadhi yetu wote ni mashahidi kwamba changamoto zilikuwa nyingi na nyingi zimetatuliwa na nyingine zipo njiani kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana kwamba hizi changamoto zilizobaki waziharakishe ili wananchi wa pande zote za Muungano waridhike. Vilevile niwaombe sana wananchi wa Tanzania kwa ujumla wa upande wa huku Tanzania Bara na kwa upande wa Tanzania Visiwani kwamba Muungano huu pamoja na changamoto zilizokuwepo lakini bado zimeleta manufaa kwa pande zote mbili.

Mimi kwa upande wangu naweza kusema kwamba Muungano huu umetusaidia vilevile kuweka amani katika nchi yetu, usalama umekuwa mkubwa sana. Vilevile ukiangalia biashara kwa pande zote mbili hizi, pande zote mbili zimenufaika upande wa biashara. Haya yote yanatokana kwa ajili ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tumechanganya damu; leo aliyekuwa Zanzibar kaenda kuoia Tanga, leo Mzanzibari kaenda kuoia Arusha na wa Manyara kaenda kuoia Zanzibar, sasa tumechanganya damu. Mwaka 1964 tulichanganya udongo leo tumechanganya damu, kwa hiyo, naweza kusema ni hatua kubwa sana ambayo sasa hivi wananchi wa pande zote mbili hizi wanapendana na tuombe tuendeleo kupendana kwa sababu ni manufaa ya vizazi vyetu vijavyo na watoto wetu wanaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika suala la Muungano limetuletea faida katika mambo ya utalii. Sasa hivi Zanzibar imepiga hatua kubwa sana katika mambo ya utalii. Kwa kweli utalii huu vilevile kwa sababu watalii wanaokuja Arusha, Ngorongoro, Serengeti, wale wale ndiyo wanakuja Zanzibar na kutuongozea mapato. Kwahiyo, nasema kwamba kazi kubwa imefanywa na viongozi, wakuu wetu wa nchi pamoja na Mawaziri wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zipo, changamoto hata mtu anapokuwa nyumbani kwake ana changamoto yeye na mke na watoto wake sembuse nchi. Mimi hapa pengine nina changamoto zangu nyumbani sasa itakuaje nchi isiwe na changamoto? Kwa hiyo ni jambo la kuomba viongozi wetu Mungu awape busara watatue changamoto zilizokuwepo ili tuendeleo mbele ya safari. Hayo ndiyo nilikuwa nataka niseme kwa hili suala la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuvunja sherehe za Muungano na kupeleka pesa Zanzibar, itatusaidia sana kwenye . Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua yake aliyochukua ya kutueletea pesa Zanzibar ambayo itatupa matumaini kidogo na kutumia pesa vizuri katika corona kwa sababu sasa hivi siyo Bara mpaka Zanzibar inaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika masuala ya mazingira kwa sababu hii ni Wizara ya Muungano na

Mazingira; kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Azzan Zungu kwanza nimpongeze kwa kuteuliwa kwako kuwa Waziri wa Muungano. Mheshimiwa Rais hajakosea, kwa hiyo nina matumaini makubwa sana kwamba atamsaidia Mheshimiwa Rais katika kuweka mambo sawa katika Muungano na katika sekta ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu upo kwenye hili la Hapa Dar es Salaam hata Mheshimiwa Waziri akitaka ushahidi nitamletea, kuna omba omba Dar es Salaam kila pembe au kona kuna omba omba. Tunakwenda katika mazingira ya sasa hatujui wale ombaomba wametoka wapi, wanalala pale Dar es Salaam kwenye maduka nje, asubuhi pale wanachukua ndoo za maji, choo kidogo hapo hapo sasa sijui hicho choo kikubwa wanakwenda kukifanyia wapi, hiyo sijui, sina ushahidi lakini kwa choo kidogo na kuoga hata akitaka ushahidi nitamletea. Ningeomba...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: ...kupita Wizara yako ya Mazingira na watu wako wa Manispaa wafanya jitihada kubwa sana ya kuwaondosha hawa omba omba ambao watatuzidishia hii kwa sababu sasa hivi kila kona Dar es Salaam kuna omba omba ambao wanachukua ile mikono yao, wanakamata...

NAIBU SPIKA: Wataalam wa mitambo nadhani mmelekezwa nini cha kufanya jana...

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: ...pale wanafungua magari na nini. Kwa hiyo, ningeomba sana.

MBUNGE FULANI: Muda wako umekwisha.

Naam!

WABUNGE FULANI: Muda wako umekwisha.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ibrahim Raza.

Mheshimiwa Immaculate Sware Semesi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum na Mheshimiwa Ally Saleh ajjandae.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu

Spika, nashukuru kwa nafasi. Mchango wangu utajikita katika Fungu Namba 31- Idara ya Mazingira na nitakuwa na maeneo manne ya kuyagusia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo nataka nisisitizie na kukumbushana ni umuhimu wa mazingira; kila mtu anaishi katika mazingira na mazingira ni uhai lakini kwa bahati mbaya masuala ya mazingira hayapewi kipaumbele katika nchi yetu na ni jambo la kushangaza sana. Ninaposimama hapa, ningepomba kwa kweli kwa hali tuliyonayo na jinsi ambavyo tunakwenda hata bajeti iliyotengwa haitoshelezi na ningependa kwamba Bunge lako liridhie kutoipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kuna umuhimu sana na kuna kubwa sana ya maendeleo ya jamii, uchumi wa nchi, afya ya wanajamii ambayo ni mazingira na rasilimali sisi tunao uchumi wetu unaendeshwa na mazingira hapa Tanzania kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, ni dhahiri umuhimu wa mazingira haupewi kipaumbele ilihali ni ni tegemezi kwetu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili naomba niongelee kuhusu Sheria ya Mazingira; Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imeandika kwa umahiri mkubwa, lakini imeishia kwenye karatasi. Utekelezaji wake na usimamizi wake haupo sawa kabisa. Mfano; sehemu ya tatu ya sheria hii inaongelea Utawala wa Muundo wa Kiasasi; ni sekta gani zinatakiwa zisimamie, maeneo gani na nani anatakiwa asimamie kuanzia Serikali Kuu mpaka Serikali za Mitaa lakini

hali hiyo haipo nchini. Ndani ya Wizara hii tuna Idara hii ya Mazingira na tuna Baraza la la Mazingira lakini hapa sheria yetu imetutaka tuwe na Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira na tuwe na Mfuko wa Mazingira ambao sasa ndiyo kitendeakazi cha kwenda kutekeleza masuala mbalimbali ya usimamizi, uboreshaji na utunzaji wa mazingira husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maadam sheria tunayo lakini haijapewa meno na nguvu ya kutumika, basi naomba nilishauri Bunge lako mambo ya mazingira kwa unyeti wake na umuhimu wake basi yawekwe katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili mamlaka husika iweze kuona uzito wa mazingira nchini na kuweza kuyapa kipaumbele yale yanayotakiwa kama Nchi jirani zetu za Kenya, na nchi mbalimbali duniani wameweka kwenye Katiba kwa sababu ndiyo roho ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria hii ya Mazingira unasimamiwa katika Wizara hii ya Muungano na Mazingira ambayo inatakiwa iunganishe Wizara na Taasisi zote nchini kuwa na kipengele cha usimamizi wa mazingira kwa sababu mazingira ni suala mtambuka. Bunge lililopita, Bajeti iliyopita nilisema kwamba kila Wizara ilitakiwa ionyeshe kifungu ambacho kitakuwa kinagusa masuala ya mazingira kwa sababu kila Wizara, kila Taasisi kwa njia moja au nyingine kwa unyeti wake inatakiwa i masuala ya mazingira kwa sababu ndiyo ya maendeleo, ndiyo ya kuonyesha kwamba jamii yako ina uwezo na afya ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii kama nilivyosema imetaja wazi lazima kuwe kuna Mfuko wa Mazingira lakini Mfuko huo umeandikwa tu na kumetengenezwa Bodi husika lakini haiwezi kufanyakazi. Mara ya mwisho walisema kwamba vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko huu vina utata, sasa hivi kisingizio ni kwamba sheria haijakaa sawa. Inahitajika miaka mingapi kuhakikisha kwamba tuna mfuko wa mazingira ambao unaweza kufanya kazi na wenye uwezo wa kutuwezesha sisi kusimamia mazingira yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu nataka niigusie kwa haraka lakini kwa unyeti wake ni bajeti na fedha zinazotengwa kwa ajili ya mazingira. Kama nilivyosema naomba niwashawishi Wabunge wenzangu bajeti hii tusiipitishie, tuifanyie mrejesho kwa umuhimu wake tutakapokuwa tunapitisha bajeti kuu tuangalie sasa jinsi ambavyo tunaweza tukaubeba Mfuko wa Mazingira na sekta ya mazingira kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Wizara ya Fedha haitoi kipaumbele katika bajeti ya masuala ya mazingira ingawa uchumi wa Tanzania hutegemea maliasili na hali ya mazingira nchini. Naomba waje wa- hapa, hakuna Wizara ambayo imetenga fedha mahsusi kwa ajili ya masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutoa tu mfano haraka haraka bajeti iliyopita 2019/2020 Wizara hii bajeti ya maendeleo ilitoa 16% tu na fedha zake zilikuwa za nje. Mwaka huu wa fedha 2020/2021 ambayo tunataka tuipitishie hapa imetenga shilingi milioni 400, shilingi bilioni 6 inategemea fedha za nje. Mwaka jana fedha za nje ilikuwa shilingi bilioni 7 ilitoa tu 16% mwaka huu ni hizo hizo shilingi bilioni 6 fedha hizi tunaweza tukazipata kwa sababu kuna baadhi ya hawa wanatufadhili hawakuleta fedha. Sasa hivi na hali hii ya kiuchumi na mlipuko huu wa , sidhani kama wafadhili hao itakuwa kumpa Mtanzania fedha ya kutunza mazingira yake na kuyasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe kwa jicho la ziada. Mazingira ndiyo hii afya tunayoiongelea, ndiyo hii rasilimali ardhi ambayo tunavyoitumia inaweza kutuletea maendeleo au ikatushusha chini kimaendeleo, ndiyo hewa tunayoivuta na ndiyo hayo maji safi na salama tunayoyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Waheshimiwa wajumbe kama hawajapiga kura basi nawaomba wapige kura ya siyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi. Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh Ally nilikuwa nimeshamtaja ambaye atachangia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kamoli na Mheshimiwa Yussuf Hussein ajiandae.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa kazi ambazo amezifanya toka ameteuliwa. Vilevile nimpongeze Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu amekuwa _____ yaani kwa mara ya kwanza nasikia ile _____ ambayo haina ukakasi kwamba pamoja na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini anampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mara nyingi hapa zinachanganywa, anatajwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini ameizungumza _____, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tunampongeza sana kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Corona na Muungano. Tunampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua yake ya kufuta Sherehe za Muungano na kuchukua fedha kupeleka Zanzibar kwa ajili ya kusaidia vita dhidi ya Corona. Ni jambo la kupongezwa na linaakisi ushirikiano mkubwa na udumishaji mkubwa wa Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa hiyo, jambo hili ni lazima tuchukue fursa kulipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri pamoja na mengine wanaendelea kutoa elimu kuhusiana na Muungano, ni jambo nzuri sana. Wametoa

angalau wadau ambao wamewapa hiyo elimu inayohusu Muungano wakiwemo wanafunzi na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri afanye jambo la ziada kuona kwamba elimu hii ya Muungano inatolewa ndani ya Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ingekuwa ni busara tuka- zaidi kwa sababu sisi ndiyo wawakilishi wa hao wananchi ambao wapo nyuma yetu. Kwa hivyo, sisi tunapokuwa hatujui maana halisi ya Muungano na matukio yanayoendelea kutokea baina ya pande mbili za Muungano hata hao ambao sisi tunawakilisha hawapati ile ladha ya elimu yenyewe ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja inawezekana tukaliona siyo lakini limekuwa likitokea. Tarehe 7 Aprili, 2020 ilikuwa ni Karume Day lakini kwa sababu tunajua huu mwaka ni ule ambao lazima ajimwambafai baadhi yetu tukatengeneza vipeperushi Cha kushangaza kwenye hivyo vipeperushi tulikuwa tumeandika ile ilikuwa ni sherehe ambayo inabidi tusherehekee lakini kiukweli siku kama ile ni ya huzuni kwa Zanzibar kwa sababu ni siku ambayo kiongozi wa Zanzibar wa mwanzo ameuwawa, Inaonekana hata katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania elimu ya Muungano haijashiba sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kupitia kwamba, naomba Mheshimiwa Waziri achukue sasa hatua ya kusisitiza elimu ya Muungano kuanzia katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bado Waheshimiwa Wabunge hawajajuwa hususani matukio ambayo yapo upande wa pili au upande wa Zanzibar hayajajulikana sawasawa. Naompongeza kwa hatua ambazo wamezichukua lakini aongeze kasi kutoa hii elimu ya Muungano kwa upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kwamba sasa hivi kuna taarifa zinatolewa kuhusiana na mambo ya Mara nyingi Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatoa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar anatoa taarifa lakini zile taarifa ambazo

zinatolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto zinatoa idadi ya matukio ya walioathirika ama waliofariki kutokana na ugonjwa wa Corona. Inavyoandikwa inakuwa hivi, labda Dar es Salaam wagonjwa 20; Kilimanjaro mgonjwa 1 labda Arusha mgonjwa 1 na Zanzibar wagonjwa kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya Zanzibar inapotoka inaakisiwa kama ni sehemu ya mkoa na wakati athari hasa inayotokea kule Zanzibar ni katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Hili linaonekana katika taarifa hizi lakini linajitokeza pia katika , vyombo vyetu vya habari vikitoa taarifa vina- na yenyewe ni mkoa kama Dar es Salaam, Kilimanjaro au Arusha. Nadhani Mheshimiwa Waziri achukue hili inaonekana labda siyo jambo lakini ni jambo kwa sababu wale ambao hawapendi Muungano wetu wanachukua vitu vidogo vidogo kama hivyo na kuvi- na kuonekana kama hakuna hizo juhudi za kusimamia umarishaji wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusiana masuala ya umeme. Tumeshukuru sana kuondolewa kwa kwenye umeme ambao unauzwa Zanzibar. Mheshimiwa Waziri wa Nishati kama tutakuwa tunahesabu kura za Chama cha Mapinduzi basi ana- ya 50% na kuendelea lakini gharama bado Mheshimiwa Waziri wa Nishati hajazifanyia kazi. Hatujaona au hatujapata taarifa gharama za kuuzwa umeme Zanzibar mbona hatujaona?

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa hivi dakika kumi tayari?

NAIBU SPIKA: Haziwezi kufika kumi ni dakika saba Mheshimiwa kwa sababu Wabunge majina yako mengi sana hapa.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, naomba tu nimalizie hili.

NAIBU SPIKA: Dakika moja.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hiyo taarifa Waziri wa Nishati atatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, sasa unaanzisha jambo jipya tena? Muda umeisha, labda kama dakika moja uliyopewa inakutosha.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hayo yatatosha na ahsante sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ally Saleh ambaye atachangia kutokea Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kamoli atachangia kutoka humu Bungeni halafu Mheshimiwa Yussuf Hussein ajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu katika uhai wetu wa Muungano pamoja na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusiana na hili suala zima la makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kule Zanzibar. Makamu wa Rais anakaa katika eneo la Tunguu kuna ofisi yake ya faragha lakini pia kuna nyumba anayoishi. Walipoanza kujenga pale waliwakuta watu ambao ni mmiliki binafsi wa eneo lile. Yule mmiliki binafsi alikuwa amewakatia vipande watu wengi wanafika 40 mpaka 50 kwa sababu ilikuwa ni eneo kubwa. Wizara ya Muungano ilipotakiwa kuchukua eneo yule mwenye kiwanja akawauliza, je, niwaongezeeni au nisiwaongeze? Wakasema inatosha. Kwa hiyo, yeye

akaendelea kuwauzia watu na wengi wakakatiwa vipande na baadhi wamewekeza na wengine bado wana eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni mwaka watano hakuna suluhu. Kwa ajili ya usalama wa nyumba ile na mimi naweza kukubali jambo hilo ni lazima kuwa na buffer zone na pengine buffer zone yenyewe iwe kubwa kutenganisha baina ya eneo na watu au ile nyumba na watu. Hata hivyo, imechukua miaka mitano na barua kwa malaki zimeandikwa na ofisi zote za nchi hii barua zimeandikwa lakini wale watu hawajapata suluhu mpaka leo. Kwa hivyo, wameshindwa kuendeleza, yule aliyewauzia ana nyumba yake anaambiwa aivunje wakati anajenga walimuona alikuwepo na suluhu haijapatikana. Kwa hiyo, naomba hili lifanyiwe kazi ili watu hawa waweze kufanya kazi zao za maendeleo yao, waweze kujenga au waondoshwe lakini wapewe fidia zao. Walikuja watu wakapima wakawaambia kuna fidia lakini mpaka leo hakuna fidia. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili miaka kadhaa baada ya Muungano naumia sana mtu akisema leo kwamba sisi tumeungana tumechanganya damu, sijui kuuziana vitunguu, sijui kubadilishana watalii, haya mambo tungekuwa majirani hata tusingeungana tungefanya tu. Kwani watu wameoana baada ya Muungano? Watu wameoana kabla hapo, wamechanganyika wanafanya biashara. Kwa hiyo, ni haki ya kila upande upatikane kwa mujibu wa sheria na Katiba siyo kwa sababu tutachanganya damu, tutachanganya damu kwa mapenzi tu na watu wataendelea kuoana na kuachana kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumepewa shilingi milioni 500 tumeambiwa imevunjwa Sherehe ya Muungano zimekwenda Zanzibar kwa ajili ya Corona, kila Mzanzibar atafurahia. Hata hivyo, isionekane kama ni kwa maana nyingine kama kusingevunjwa sherehe Serikali ya Muungano haikuwa na wajibu wa kuwapa fedha Serikali ya Zanzibar kupambana na ? Kwa hiyo, kweli tunafurahia kwamba pesa zimetolewa lakini sisi tunaona

16 APRILI, 2020

tumepewa ni haki yetu ambayo hata isingevunjwa sherehe, kungekuwa sherehe ya Muungano ipo au haipo Serikali ya Muungano ilikuwa na wajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana sisi bado tunashikilia kwamba kuna haja ya kutazama mambo haya ya kikatiba na kisheria. Kwa mfano, tumesema na Rais Magufuli anaondoka madarakani deni la kuunda Mfuko wa Pamoja wa Fedha ameliacha pale pale hata hakuligusa. Leo miaka 40 tangu kuundwa taasisi ile na kumalizia tuna Mfuko mpaka leo haujaundwa. Kwa hiyo, sisi tunataka mambo yaende kikatiba na kisheria, Mfuko ule uundwe ili ijulikane Zanzibar ana ngapi na anatomia ngapi, Tanganyika ana ngapi na anatomia ngapi na Muungano una ngapi na unatumia ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufanye hilo siyo tu kwamba tunapewa fedha kama basi tu, ambayo inaendeshwa kwa Katiba na sheria haiendeshwi kwa utashi wa mtu kwamba ameamua tu fedha hizi nazipeleka huku basi ndiyo ameamua. lazima iende kwa Katiba na sheria, ndiyo maana tunataka kuwe na Mfuko wa Pamoja. Tunataka twende kwenye Katiba ya Tanzania turudi kwa Warioba, turudi kwa Katiba ile au ile Katiba ambayo ilipitishwa Bungeni ijulikane mamlaka ya kila mtu ni yepi na mgao uko vipi na kila kitu kipo vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu labda niende haraka haraka ni kwamba kwa fikra zangu tunajidanganya tu. Corana ni mkusanyiko, ni kujitenga, kusafisha mikono na Tuchukue hali ambayo tumefika sasa, watu 88 maana yake kuna watu zaidi ya 2,000 walioambukizwa ambao wapo mtaani, huo ndiyo ukweli. Ni kwamba kila mtu mmoja anaambukiza si chini watu kumi kwa siku. Fikiri watu hao ambao wameambukizwa na hao walioko ndani nje wapo wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nashauri Zanzibar na Dar es Salaam zifungwe. Meli isitoke Zanzibar, Pemba na Unguja pia watengenishwe, Dar es

Salaam ifungiwe, Dodoma ifungiwe na Dodoma si ajabu kwa sababu hata Wachina waliikinga Beijing na Shanghai, magonjwa yote yaliyotokea kule walikinga vitu vyao. Kwa hiyo, sasa imefika wakati lazima tufanye maamuzi magumu. Tufunge na maduka ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba Watanzania maskini, wanahemeahemea tuwaachie tu, twende hivi hivi, tutakufa. Baadaye Tanzania wameshakufa watu 10,000 au 15,000 viongozi wa kisiasa mtakuja kutuomba radhi. Maamuzi magumu lazima myafanye, Uganda, Kenya na Afrika Kusini kuna maskini na wote wamekwenda katika Hatuwezi nzima basi angalau tufanye ya nusu yaani lazima tunusuru umma wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Bonnah Kamoli atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein na Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi ajiandae.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Zungu kwa kuteuliwa katika Wizara hii ya Mazingira. Pia nimpongeze Naibu wake na mama yetu Mheshimiwa Samia kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuongelea jambo moja ambalo linahusiana na Mto Msimbazi. Mto huu Mheshimiwa Waziri, Naibu na watendaji wote wanaujua. Mto Msimbazi ambao umepita Dar es Salaam umekuwa ni tatizo kubwa hasa kwa sasa hivi mvua inaponyesha. Juzi niliongea hapa nilisema kwamba kumekuwa na mafuriko makubwa, mafuriko mengine yametokea kutokana na uchakavu wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwa sababu mwaka 2017 tuliitwa kwenye

16 APRILI, 2020

kikao tukaambiwa kwamba Mto Msimbazi utaanza kuwekewa kingo ambazo zingeweza kuwasidia wananchi wetu ambao wamejenga karibu na mto huu ili wasiweze kupata mafuriko. Sasa huu ni mwaka 2020, Mheshimiwa Waziri hatujaona hiyo kingo ambayo imejengwa wala maandalizi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulishawahi kuhudhuria kwenye kikao na Mheshimiwa Waziri tuliitwa na Mkuu wa Mkoa wakasema kwamba pesa ni za _____ na mkandarasi alikuwa ameshapatikana. Mpaka sasa hivi sijajua ni kitu gani ambacho kinazuia mto huu usianze kujengwa? Kwa kweli mto huu umekuwa ni tatizo kubwa sana hasa kwa wananchi ambao wanakaa pembezoni ya mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi pia imekuwa ni tatizo kubwa sana, huu mto kutokana na miundombinu mibovu sasa hivi maji hayapiti kwenye mto yameanza kuwafuata wananchi ambao wanakaa jirani na hilo bonde. Siyo kwa sababu wamejenga jirani kama navyosema nafikiri hata wataalam kutoka _____ tulishawahi kufanya ziara wakaona, maji sasa hivi yameacha njia yake yanawafuata wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulishafanya mikutano mbalimbali ya kuwaelezea wananchi kwamba wale ambao wamejenga karibu sana na mto sasa hivi wasihangaikie kuhama kwamba mto unajengewa kingo na wananchi wataendelea kuishi na wengine wataendelea kupita na kufanya mambo mengine na mpaka tukaambiwa pia kutakuwa na utalii ambao utafanyika kwenye mto huo. Mpaka sasa Mheshimiwa Waziri ni 2020 hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea na kuna nyumba nyingi zimezungukwa na maji. Kwa mfano, nikiingelea Kata ya Vingunguti tu ambapo huo mto umepita zimeondoka nyumba karibu 500 lakini Kata ya Kipawa mto umekuwa ni tatizo kubwa na maeneo mengine pia.

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anapofanya
atuambie ni lini mto huu unaanza kujengewa kingo?

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anapofanya atuambie kwamba atuambie kwamba huu mto unaanza kujengewa kingo lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusiana na dampo la Pugu Kinyamwezi ambalo nimeona Mheshimiwa Waziri amelitembelea lakini bado halina hali nzuri na wakazi wa maeneo ya pale wanapata shida sana kutokana kwanza na harufu pia na mazingira. Kwa sababu kama mnavyojua, Dar es Salaam inazalisha taka nyingi sana kwa siku na zile taka haziwezi kutosha kwenye lile dampo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, ni lini tutapata dampo la kisasa kama madampo mengine ambayo tunayaona kwenye sehemu nyingine? Siwezi kusema nchi nyingine; kuna dampo la kisasa ambalo liko Mkoa wa Arusha. Nasi kwa sababu Dar es Salaam kutokana na kubwa, tunahitaji tupate dampo la kisasa ambalo linaweza likawa sehemu watu wakakaa na dampo likaweko lakini kusitokee matatizo au na uchafuzi wa hali ya hewa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo nilikuwa nataka kuchangia katika hii siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Yusuph Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleman Masood Mchambi na Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakari atachangia kutoka Msekwa.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami niungane na wenzangu wote kuwapa pole Watanzania kwa janga kubwa la na niwaombe tuendelee kuchukua tahadhari na kufuata taratibu

16 APRILI, 2020

tunazoelekezwa na wataalamu wetu wa afya na Mwenyezi Mungu atatuepushia balaa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalotaka kuchangia leo katika Wizara hii ya Muungano, zaidi ni suala la mazingira. Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni wataalam nadhani watanisikiliza vizuri. Kuna mchezo wa kitoto tulikuwa tunacheza zamani, sijui sasa hivi; watoto nyoka, watoto nyoka; na apite! Nyoka yuko Dar es Salaam; na apite! Yuko Morogoro na apite! Yuko Kibaigwa na apite! Yuko Ihumwa, ndiyo wanaanza kukimbizana, nyoka nyoka!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna balaa kubwa; janga kubwa linakuja ndani ya nchi yetu na litaua Watanzania wengi kulikoni hii ambayo sasa hivi tunayo, lakini tunalidharau tunalionga kama liko mbali sana. Tanzania inapoteza hekta 470,000 kila mwaka za misitu katika hali mbalimbali. Kilimo cha ufugaji usiokuwa na utaratibu, uvunaji wa misitu, uhomaji wa mkaa, hekta hizo zinapotea katika hali tofauti tofauti na hakuna tahadhari yoyote inayochukuliwa na Serikali yetu mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, likitokea hilo, itanyooshewa kidole Wizara ya Maliasili Idara ya Misitu ambapo wao wanasilimia 33 tu ya misitu iliyopo nchini; nao wanapanda hekta 13, 000 kwa mwaka wanazojua wao. Wao kama Wizara wanapanda 9,000 na jamii inapanda 4,013. Sasa sijui kama Wizara ya Mazingira hii ina takwimu ambazo ni zaidi ya hapo. Sijui kama TAMISEMI wanao-asilimia 66 ya misitu wanapanda au wana takwimu zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunapoteza 407,000 kwa mwaka tunapanda 13, baada ya miaka 10 Tanzania tunategemea nini? Tutakufa kwa njaa, tutakufa kwa maradhi, tutakufa kwa upepo mkali utakaokuja, tutakufa kwa jua, kwa sababu ya joto kali litakalokuja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano hai Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru upo, tuma timu yako iende Kojani tu hapo. Katika miaka mwishoni mwa 1980

walikata msitu ule upande wa Kusini, waliufyeka wakatamia kwa kujenga. Kila mwaka Juni - Julai walikuwa wanakufa watoto kati 150 mpaka 250, ni na . Wenyewe wanasema walikuwa na baridi yabisi, kumbe ni tatizo la upepo wa kusi unapiga, watoto wadogo hawahimili wanakufa kwa idadi hiyo. Mpaka walipokuja kugundua wakahifadhi ule msitu, maradhi yakaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano halisi upo ndani ya nchi yetu. Leo ndani ya nchi yetu tunapoteza hekta 407,000 kwa mwaka, hatuchukui tahadhari yoyote, tunapanda 13. Nini kitatokea baada ya miaka 10? Litatokea jua hapa kulikoni hilo la Arabuni magari yaungue. Utakuja upepo maradhi yote yatakuwa yanakuja Watanzania wanakufa. Sasa ya misitu inachukua muda mrefu kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu upo, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira ni mtaalam, naomba mkae kama Serikali muone tunachukua tahadhari gani? ipo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora ameonyesha njia, anastahili sifa na anastahili apewe tuzo kwa namna ambavyo amejizatiti kuhakikisha kwamba anafanya ya upotevu wa mazingira katika Mkoa wake, lakini ni Mkoa mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii hatari inayokuja, leo hatuioni, tunasema nyoka bado yupo Morogoro au yuko wapi, lakini siku akiingia nyoka huyo hapo sasa tunakimbizana kupanda miti, tutakimbizana kweli. Kwa hiyo, hili niliona niliseme leo ili kama Serikali muone namna gani mtaweza kukaa pamoja kulitatu tatizo hili. Hili ni tatizo kubwa sana, ni janga kubwa sana linakuja kwenye nchi yetu na kuja kulirekebisha linachukua miaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizo 13 zinazopandwa ni hizo zinapandwa tu kwa namba lakini ni ngapi? Pengine 11 au 12 kama zinafika. Kwa hiyo, bado hata 10% ya uharibifu hatujafika. Tunaelekea wapi? Watanzania wanaongezeka, mahitaji yanaongezeka,

16 APRILI, 2020

teknolojia zinaongezeka, ardhi yetu ni ile ile, misitu yetu ni ile ile haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wanadamu labda tutakuja kupata teknolojia nyingine ya kufanya; wanyama je, ambao tumeshawaharibia zile zao, wao wataenda wapi na hawawezi kupanda miti? Hawawezi kuchimba mabwalo na visima wakapata maji ya kunywa, tushaharibu kila kitu, wao watakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutapoteza kila kitu, uchumi wa nchi utakwenda na kila kitu kitakwenda. Naiomba Serikali ikae ilifikirie hili iliandalie mkakati wa kutosha tuone tunapoteza 407,000 tunapanda ngapi, zina-ngapi? Vinginevyo tunaenda katika balaa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka niliseme...

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili ishagonga. Ahsante sana.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Suleiman Masood Nchambi, atafatiwa na Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar na Mheshimiwa Vuai Shamsi Nahodha ajiandae.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, wawheja sana. Kwanza nataka niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya kazi. Kumekuwa na mabadiliko makubwa, kumekuwa na kasi kubwa. Sisi Wasukuma tuna msemu tunasema, yaani macho yanayoona na masikio yanayosikia. Kwa hiyo, tuna hakika kabisa mwenye macho

anaona kile kinachoendelea na mwenye masikio anasikia kile ambacho kinaelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi sana pia kwa Wizara yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Zungu. Nina hakika anayapeleka mambo Kizungu sasa hivi. Nieleze mambo machache ambayo pia yamesemwa hapa na baadhi ya Wabunge kabla sijaweka michango yangu sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ally Saleh ameongea mambo ambayo yamenisikitisha sana. Sisi Waislamu kuna hadithi inasema,

Waislamu ni safi ndani ya mioyo yetu na imani zetu na hatuwezi kwenda katika pepo ambayo Mungu ametuandalia mpaka tuwe wasafi. Sasa ameeleza jambo ambalo kidogo limenisikitisha, anasema, masuala ya kuona siyo ya msingi kabisa; masuala ya kuunganisha udugu wa damu siyo ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua historia ya kuumbwa mwanadamu. Mwanadamu ameumbwa katika pembe nne za dunia; udongo ulichukuliwa sehemu tofauti, siwezi kushangaa sana, lakini ni bora niliseme na niliweke wazi ili hata watu wa Mji Mkongwe zamani ikiitwa Malindi wapate tahadhari juu ya mwakilishi wao na hoja anazozitoa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu tumeumbwa na kuchukuliwa udongo kutoka sehemu mbalimbali. Kuna ambao ulichukuliwa katika sehemu ambazo kuna matope yananuka, kuna sehemu ya bustani na kuna sehemu ya mito. Kwa hiyo, inawezekana udongo uliochukuliwa wa mwenzetu sina takwimu kwa sababu ni historia, lakini nawaomba watu wa Mji Mkongwe wachukue tahadhari kwa sababu mtu anapokataa udugu wa damu anaelekea wapi? Mtu anapokataa dada zangu wa Shinyanga, wameolewa Zanzibar na Wazanzibar na ndugu zangu Shinyanga wameoa Zanzibar wamewaleta pale. tunao Wazanzibar mashemeji. Leo undugu ule siyo wa maana.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi mtu badala ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kupeleka shilingi milioni 500, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kutoa kile kidogo ambacho aliona kingeenda kwenye Sherehe za Mei Mosi na Muungano ziende zikasaidie angalau ziwe pale katika janga hili endapo chochote kitatokea mchango wa Muungano, mchango wa Mheshimiwa Rais, mchango wa nchi nzima kwa maana ya Tanganyika Visiwani na Tanganyika huku kwetu uonekane, lakini anasema hizi shilingi milioni 500 zisiwe ni agenda ya kuonekana kwamba ni jambo la kimuungano linatuunganisha. Ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana Waheshimiwa Wabunge tumwombee mwenzetu tutakaporudi majumbani na katika mioyo yetu ili moyo wake angalau uwe na shukurani. Binadamu asiye na shukurani kwa kweli hana roho ya ubinadamu. Nisingependa kumsema sana, niende katika michango.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo lilikuwa hapa linaongelewa sana kuhusu sukari Zanzibar. Nami namwomba sana Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili tuliangalie kwa mapana. Kumekuwa na tabia sasa hivi, kila kunaposogea mwezi wa Ramadhani katika miaka hii mitano Serikali yetu inaanza kuchonganishwa na Waislamu. Nimeona kuanzia juzi tunakwenda sasa Ramadhani, ajenda kwenye mitandao imekuwa ni bei ya Sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana wamesema sukari kule kwao haijapanda, lakini najiuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi huku mtaani tunayo Serikali nyingine inayotoa maelekezo juu ya bei ya sukari kila inaposogea Ramadhani? Jambo hili ni la hatari sana kwa sababu kila tunaposogea hapa kwenye mfungo wa Ramadhani; sukari ni kiungo muhimu sana wakati wa kufuturu jioni, lakini bei inaanza kupandishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu maelekezo makali yatoke kwa Serikali tunayojua hii ya Awamu ya Tano inayoongozwa na jemadari Magufuli

na wewe ukiwa ni Mtendaji Mkuu wa Serikali. Sipendi nikupe maelekezo, hapana; lakini haka ka Serikali kaliyoko mitaani ka wafanyabiashara wachache ambao wanataka kutuchonganisha sisi na wananchi, lazima tuwashughulikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo kero kubwa sana ya za kimazingira hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam ni- kwamba nina heka moja tu pale Kipawa, lakini gharama ya ile ya inakwenda mpaka shilingi milioni nane. Nami kitu ambacho ningeshauri kwenye hili jambo, gharama inaletwa kubwa kwa sababu ya wale ma- wanaoandaa zile nyaraka. Chukua mfano wa , nami nawapongeza sana wao wenyewe wanakwenda kufanya wanapeleka wataalamu wao, unalipa kwa kila kitu wanakufanyia wao mpaka tuna-

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wanakwenda wataalam wenyewe. Sasa Wizara yako wataalam hawa wa lazima upitie kwa upitie mzunguko mkubwa. Mtu ana nusu heka, robo heka ya biashara yake kwa leo hii anachajiwa zaidi ya shilingi milioni tano mpaka saba mpaka kukamilisha ya kimazingira. Hii ni kero kubwa sana inayoendelea katika Mkoa wako wa Dar es Salaam na ninajua itaendelea kushuka chini taratibu kama Wabunge hatutaisemea vizuri.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja bado. Kwa hiyo, hiyo dakika moja nitaitumia vizuri...

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

16 APRILI, 2020

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, shukurani.

Mheshimiwa Zainab Musa Bakar atachangia kutokea Msekwa, atafatiwa na Mheshimiwa Vuai Shamsi Nahodha na Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa ajiandae.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuongea. Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema nikaweza kusimama katika ukumbi huu na kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili namshukuru Mwenyekiti wangu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kuniamini na kunateua kuwa Naibu Waziri Kivuli wa Ofisi ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunatakiwa tujue nini maana ya Muungano na hili neno Muungano lilitokea wapi? Kwanza tunapozungumza Muungano tunazungumzia nchi mbili ambazo ziliungana; nchi ya Tanganyika na nchi ya Zanzibar. Ina maana hapo ndiyo lilipatikana neno "Tanzania" ambalo lilitujumuisha tukawa na Muungano. Huu Muungano siyo kama umesababisha tusiongee ambayo yanatuathiri katika mioyo yetu. Hilo ni wazi, ni lazima tuliongee kama Watanzania na kama Wazanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kwamba hakuna kero za Muungano lakini kero za Muungano hazijaondoka. Kwa mfano, kuna tatizo hili la muundo wa Muungano. Hapa tunaona kwamba Muungano uliopo Watanzania wengi hawaridhiki nao. Huo ndiyo ukweli na ukweli haufichiki. Hapa ilikuwa tuwe na Serikali tatu; ya Tanganyika, Zanzibar na baadaye kuwe na ya Muungano. Ndipo Muungano huu ungeondoa mazagazaga mengine yote ambayo yanajitokeza leo ambayo tunafungwa mdomo

tusiseme ni kero za Muungano. Tutaendelea kusema kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba ndiyo Mheshimiwa Rais amepeleka shilingi milioni 500 Zanzibar, hiyo ni haki yetu kama Wazanzibar kwa sababu ni kitu cha Muungano. Ni sawasawa na mwaka 2016 Mheshimiwa Rais huyu huyu alipeleka zaidi ya shilingi bilioni mbili kupanua barabara ya Mwanza

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainabu, kuna taarifa inatoka hapa, kwa hiyo, uisikilize. Mheshimiwa Suleiman Nchambi.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la shilingi milioni 500 halikuwepo katika bajeti. Nilitaka nimpe taarifa Mheshimiwa Zainabu kwamba halikuwepo katika bajeti na haikuwa haki kwa sababu halikupitishwa kisheria. Ni Mheshimiwa Rais kwa wema na moyo wake mzuri ameona bora fedha zile zikawasaidie wenzetu kule. Nilitaka nimpe hiyo taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuipokea hiyo taarifa kwa sababu yeye mwenyewe anajikanganya. Kwa sababu hata hapo alipopeleka mwaka 2016 zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa upanuzi wa barabara, haikuwa ndani ya bajeti. Kwa hiyo, hiyo ni haki kwa sehemu zote mbili. Kwa hiyo, hapo haina budi kwamba sisi tumshukuru au tutoe pongezi kwa sababu ya suala hilo, isipokuwa ametimiza wajibu wake kama Rais.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, kuana suala ambalo Mheshimiwa Ally Saleh pia amelizungumza kuhusu mgogoro wa pale katikati ya Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Zanzibar, Tunguu. Ni kwamba ile ofisi kuna watu zaidi ya 50 wengine wamejenga nyumba zao, wengine wamejenga ma lakini wamezuiwa kutokana na sababu za kiusalama zaidi. Sasa huu ni mwaka wa tano tena hawalipwi fidia, hawalipwi viwanja mbadala ambavyo vitawawezesha kwenda kufanya shughuli zao. Wamedunduliza pesa zao mpaka sasa hivi wameshazitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara hii ituambie kwamba ni lini watawalipa fidia, na kama kuna eneo ambalo watalipima wajulikane watu ambao watakuweco ndani ya eneo na waliokuwa hawako ndani ya eneo...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Taarifa.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:...wapewe fidia zao waendeleo kujenga na walioko ndani ya ... waendeleo kupewa fidia zao.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie katika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab, kuna taarifa, halafu kengele ya kwanza ilikuwa imegonga, natumaini uliisikia; Mheshimiwa Mwakajoka.

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa tu Mheshimiwa Zainab kwamba ukweli Serikali Tatu katika nchi hii zinahitajika na Mheshimiwa Prof. Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje, anajua, pamoja na Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi, Polepole, anafahamu vizuri sana...

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: ...kwamba Serikali mbili hazijakidhi haja, zinahitajika Serikali tatu; ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa naipokea kwa mikono miwili kwa sababu ni jambo ambalo ni haki na Muungano ndipo utadumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia pia suala la akaunti ya Zanzibar, Tume ya Pamoja ya Fedha. Hili ni takwa la Kikatiba, mpaka leo tunajiliza hivi pesa zinazokusanywa za Muungano zinapelekwa kwenye akaunti ipi na Zanzibar wanapewa kiviipi? Hii akaunti ni suala la Katiba litatekelezwa lini, nataka Waziri atakapokuja kuhitimisha anjibu hilo swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitazungumzia kuhusu miradi ambayo ilikuwa itekelezwe Zanzibar; mradi wa uwanja wa ndege, mradi wa bandari, mradi wa njia ya kilometa zisizozidi 40 kutoka Chake kwenda Wete. Hili ni suala ambalo tokea mwaka jana tunalipigia kelele hapa; kuna kikwazo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kule tumepata wafadhili, haturuhusiwi kufanya hicho kitu mpaka tupate saine ya Waziri wa Fedha wa Muungano, au Jamhuri ya Muungano itie saine. Kwa nini mnashindwa kutia saine ili tutekeleze hiyo miradi?

MBUNGE FULANI: Mambooo motomoto!

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Kunakuwa na shida gani? Naomba Waziri atakapokuja pia atoe ufafanuzi wa suala hilo kwa sababu ni suala ambalo linatumiza sana Wazanzibari. tunaambiwa sisi ni ndugu wa damu; ndugu wa damu unaweza kumfanyia mambo kama hayo?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab, muda wako umekwisha, ahsante sana.

16 APRILI, 2020

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vuai Shamsi Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Salum Rehani ajjandae.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nipate kutoa mchango wangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1964 wakati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na Mzee wetu Karume walipoasisi Muungano, Zanzibar ilikuwa ina watu wapatao 360,000, lakini leo Zanzibar ina watu wasiopungua 1,300,000. Umuhimu wa Muungano kwa maoni yangu, leo ni muhimu zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1964.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Zanzibar ilikuwa na watu 300,000 lakini mzee Karume, kama ilivyo ya viongozi wa aina yake, wana maono ya mbali sana mambo ambayo watu wa kawaida hawayaoni. Alisema anatambua kwamba Zanzibar ni sehemu ndogo sana na Tanzania Bara ni nchi kubwa lakini akaona Zanzibar ya miaka 100 mbele akasema Zanzibar itakuwa na tatizo kubwa sana la ardhi, jambo ambalo sasa hivi sisi tuliopo hata kabla ya miaka mia hiyo tunaliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ina watu, kama nilivyosema, milioni moja, Mheshimiwa Saada anasema na laki tano, lakini eneo lake ukubwa wa Zanzibar ni kilometa za mraba 2,641, sasa tufanye hesabu, watu hao wanakaaje kwenye eneo hilo. Kuna baadhi ya maeneo kule Zanzibar tunaanza kupata matatizo makubwa sana ya ardhi ya ujenzi wa viwanda, mashamba, kujenga shule, kwa hiyo lile alilolisema marehemu mzee Karume linaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa nasaha Wazanzibari wenzangu waitumie fursa hii ya Muungano vizuri

16 APRILI, 2020

sana. Kwa nini; hivi sasa takwimu zinaonesha Tanzania Bara kuna Wazanzibari au Watanzania kutoka Zanzibar wasiopungua 500,000, ni karibu asilimia 50 ya wale walioko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini; bila ya Muungano wangekuwa Zanzibar, tungevurugana kwelikweli, tungeumizana kwelikweli. Kwa hiyo, sisi Wazanzibari muungano na ardhi ya Tanzania Bara inatupa nafasi ya kupumua. Mzanzibari anayo haki ya kuomba hata ekari 1,000 Bara na wapo Wazanzibari nawafahamu kwa majina.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wapo Watanzania wenzetu wanaliona kama ni la kipuuzi hili, lakini kama ardhi tunaona jambo la kipuuzi naomba tukawaulize Wakenya. Kumekuwa na mjadala wa siku nyingi sana ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya matumizi ya ardhi, hasa ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema tunaweza kuliona hili ni jambo dogo lakini viongozi, na hasa sisi viongozi wa kisiasa, nasema tu tujirudi, maneno huumba. Tukiiona Muungano hauna maana utakuwa hivyo hivyo hauna maana, lakini tukiamini kwamba unayo maana utaendelea kuwa na maana. Kwa hiyo maneo huumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hiyo. Au naomba dakika mbili.

MBUNGE FULANI: Apewe!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuai umeongezwa dakika tatu.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasema maneno huumba na sisi wazazi tunalijua sana jambo hilo, ukisema aah, hili toto la kazi gani? Ataendelea kuwa hivyo hivyo akishakuwa mkubwa; wa kazi gani. Sasa tukiiona Muungano huu hauna maana utakuwa hivyo, lakini

16 APRILI, 2020

tukiamini kwamba Muungano unayo maana utaendelea kuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba huu ni Muungano wa watu, sio wa malaika. Inawezekana ziko kasoro tu lakini hata kwenye familia zetu hatuzivunji, kasoro zipo. Kazi ya viongozi si kuogopa matatizo, kazi ya viongozi ni kuzungumza matatizo na kuyatafutia ufumbuzi. Kazi ya viongozi sio ya kulalama tu. Sisi hapa kama Wabunge hatuwezi kukaa tu hapa tukalalama, hili ni jukumu letu, tutafute njia, kama kuna matatizo tukae.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; uwakilishi wa Wazanzibari katika Bunge la Muungano; wapo wanasiasa na kutoka vyama tofauti na Chama Cha Mapinduzi ndani ya Bunge nimewasikia sio mara moja au mbili wanasema hivi; wanahisi kwamba Zanzibar inapewa isichostahiki. Wanasema Zanzibar kuna watu 1,500,000 lakini wana Wabunge 50 kwa hiyo Zanzibar inapata zaidi. pengine ingekuwa Zanzibar ni majimbo mwili. Sasa nasema Muungano huu unaendeshwa kwa ridhaa, na Muungano ni ridhaa tu; wakati mwingine utapoteza kidogo, wakati mwingine utapoteza kikubwa, lakini jambo la msingi ni umoja na maelewano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudia, nawaambia ndugu zangu Wazanzibari tutumie vizuri fursa za Muungano. Tukizitumia vizuri bila shaka Zanzibar itanufaika kwa kiasi kikubwa sana, lakini hata na Bara inanufaika na umoja na kuwa na Zanzibar kwa hiyo, naomba tuenzi, tuutukuze, tuudumishe na kama kuna matatizo tusiogope matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, atachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hotuba ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakwenda kwenye maeneo matatu; eneo la kwanza ni shukrani, eneo la pili pongezi na eneo la tatu ntachangia kiasi fulani kwenye hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi; naomba niwashukuru viongozi wetu wa Bunge kwa kutuletea fursa ambayo imekuja kwa wakati. Tumepata Janga la Corona na tumejigawanya sasa wengine tuko Msekwa, wengine wako huko, tunatumia _____ nawapongeza sana kwa utaalim mliotuletea wa kutumia vishikwambi katika kuendeleza shughuli zetu za Bunge, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesema nitumie fursa kwa kuwapongeza viongozi wetu wakuu wa nchi. Napenda nimpongeze sana Dkt. John Pombe Magufuli. Sababu za kumpongeza, kama nachangia Wizara ya Muungano, Dkt. Magufuli amechukua fursa kubwa sana ya kuyafuata au kuyatekeleza yale ambayo yalipangwa na viongozi wetu wa asili, Mwalimu Nyerere na Mzee Karume, hiki ni kitu cha mfano. Kuna mambo mengi sana ambayo alikuwa na fikra nayo mzee Nyerere yakashindwa kutekelezeka, na sasa tunashukuru sana mambo mengi yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hilo halitoshi, kwa upande wa Zanzibar napenda nimshukuru sana Dkt. Ali Mohamed Shein. Amefanya vitu ambavyo hatukuvitegemea lakini sasa vitu vinaonekana. Niseme kwa uchache tu; natoka Jimbo la Amani. Kuna eneo pale linaitwa Kwa Wazee au Sebleni, miaka ayami panatuama maji na kila masika watu

wanahama, lakini kuanzia masika hii hakuna mtu aliyeondoka pale, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hilo halitoshi, nizungumzie suala zima la Muungano. Kuna mwenzangu kagusa kidogo sana. Nataka niuseme kwa upana wake; Muungano ni suala la ridhaa la nchi mbili zilizokuwa huru, Nchi ya Tanganyika na Nchi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1964 ilikuwa tarehe 22, Aprili, kuna wakilishi mmoja yuko hapa Dodoma, huyu mzee Lusinde, huyu ndio aliyekuja na waraka akapokea mzee Moyo wakaenda nao kwa mzee Karume wakasema hapa sasa tunataka kufanya muungano. Na dhamira yao ni kubwa sana kwa sababu mtazamo huo ulikuwa kuunganisha Afrika nzima, sio Zanzibar na Tanganyika tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa muungano huu ni wa nchi mbili ambao tumekubaliana wote na manufaa yake tunayaona. Ingingekuwa salama nchi yetu ya Zanzibar ama ya Bara kama kulikuwa hakuna muungano huo. Sasa wale wanaotaka muungano wa Serikali tatu wasubiri, na hilo litachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu walikuwa wanasema kuna changamoto za Muungano, mimi nasema kuna kero za Muungano, zote ndivyo zinavyosema, kwamba kuna kero za Muungano na zilikuwa karibu kero 15, lakini kero 12 zimetatuliwa bado kero kubwa tatu sasa hivi. Na lazima tuzitaje wazi kabisa na imani yangu kabisa ni kwamba Mheshimiwa Zungu, namjua ni mtu mweledi, mwelewa na mtu mwenye bidii sana ya kazi yake, si mtu mwenye tabia ya kushindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hii kero ya usajili wa vyombo vya moto, inanipa shida sana, itachukua muda gani; au Hebu tuambie ya kufanya tathmini. Kwa nini kuna shida leo, chombo ambao kimesajiliwa Bara Zanzibar kinatembea bila shida yoyote lakini chombo ambacho kimesajiliwa Zanzibar ikija hapa Bara

inakuwa ni kero. Tunamuomba sana Waziri anapofanya majumuisho atuambie kero hii itaisha lini, inatusumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lazima niseme ni mwanamuungano kwa sababu mbali ya kuwa Mbunge hapa nimepata uhifadhi, nimepata usajili wa kwamba ni Mwanamsalato, sasa nawashangaa sana wale ambao bado mpaka leo hawajathamini jitihada ambazo zinafanywa na viongozi wetu katika kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kidogo sana, nakitaka hiki kitu kifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo kwa sababu wapinzani wanapozungumza namna ya kuleta maandamano na mambo mengine katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania hoja yao kubwa ni kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na mwelekeo ulivyo, kesho tukienda kwenye uchaguzi hapa na kama kero moja nyingine itapata ufumbuzi basi hawa hatutawaona kwenye Bunge humu, hawatachaguliwa. Wananchi wana imani kabisa na viongozi wetu wa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu wamefanya jitihada ya kuondosha kero na kuleta faraja ndani ya nchi yetu ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho...

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa. Mheshimiwa Salum Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia machache katika Wizara hii ya Makamu wa Rais,

16 APRILI, 2020

Muungano na Mazingira. Nina mambo matatu ambayo niliona niweze ku- na Wabunge na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni suala zima la mazingira, hasa wenzetu wa ambao hawa ndio wenye jukumu la kuhakikisha kwamba, mazingira yetu yanakuwa salama na endelevu, lakini muono wangu naona kama sasa hivi inageuka ni au taasisi ya uzalishaji na utafutaji fedha badala ya kutoa misingi halisi ya vipi tunaweza tukahifadhi mazingira yetu. Kuna maeneo mengi ambayo wanatakiwa wayasimamie, watoe elimu na maelekezo kuliko kupita na kukusanya fedha kwa ajili ya vibali na mambo mengine.

Tuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu, hasa maeneo ya misitu. Wenzetu takwimu wamezitoa hapa baadhi yao za ukataji wa miti, lakini Tanzania vilevile sasa hivi kwa hatua tuliyofikia ya uharibifu wa mazingira tumeingia katika nchi ambazo na sisi tunachangia katika uharibifu ule wa miongoni mwa nchi ambazo zenye uharibifu mkubwa, lakini tulikuwa na mipango mingi na mizuri ya kuweza kuhifadhi na kuweza kuwa na za kutosha kabisa ambazo zingeweza kuchangia kupunguza athari hizo za mazingira, lakini matokeo yake watu wetu wa Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais imeziacha na haikuzishughulikia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Mwongozo na kupitia Mradi wa hakuna kilichokuwa kimeendelea mpaka leo tumeitia kapuni. Mradi ambao ulifanyiwa kazi kwa miaka mitatu; wenzetu wa Norway walipoteza fedha nyingi kuweza kujenga misingi na utaratibu mzuri wa kuweza kuhifadhi mazingira ya nchi kavu pamoja na ya bahari ambayo yangeweza kutunusuru na kutuelekeza sasa tuelekee wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja lilikuwa ni mkakati sasa wa kuhakikisha kwamba, tunapeleka fedha kwa ajili ya kutawanya sasa matumizi ya gesi asilia kwa wananchi wetu ili kupunguza sasa msukumo mkubwa wa ukataji miti kwa ajili ya mkaa, hili limeachwa na watu wamekaa kimya na bado

nguvu ya kulishughulikia hili imekuwa ni ndogo sana. Nimwombe Waziri moja kati ya kazi kubwa ambayo anatakiwa kuifanya ni kuifanya Tanzania iwe ni nchi ambayo inatumia gesi asilia na sio kuendelea kutumia mkaa, hasa katika taasisi mbalimbali za umma na nyingine za watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Kuna uharibifu mkubwa katika bahari zetu, haishughuliki chochote katika suala zima la uhifadhi wa mazingira ya bahari; eneo letu la bahari ni kubwa, lakini limekuwa dampo la kutupia kemikali za vitu mbalimbali. Kuna baadhi ya meli zinakuja zinatupa mafriji mabovu katika bahari, zinatupa mabaki mbalimbali ya kemikali za kilimo na nyinginezo katika bahari, lakini hakuna utafiti, hakuna chochote kinachofanyika na tunafikiri kwamba, yale yatabaki kama yalivyo, lakini ile ni athari kubwa na sisi ndio tunaoelekea sasa kuangamia katika hilo janga.

Mheshimiwa Naibu Spika,

[Maneno Haya Siyo

Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Kuna Taarifa, sijui kama yuko Msekwa au humu ndani?

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, niko Msekwa, Mheshimiwa Ally Salleh.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Salleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimuarifu Msemaji kwamba, katika hadhara kama hii kutaja jina la kampuni na kuitia hila si uzuri katika

hali ya kibiashara. Ningependa nimpe Taarifa hiyo na iondolewe nafikiri.

NAIBU SPIKA: Shukrani. Mheshimiwa Rehani kabla hajasimama Mheshimiwa Ally Salleh nilikusudia kukuuliza kama unazo hizo taarifa za kitaalam kwa sababu, maji yanapimwa kwenye vyombo vyetu ambavyo chombo chenye mamlaka ya kutuambia ni lakini pia inaitwa sasa hivi Sasa hivyo vyombo viwili kama vimeona kuna kitu kimezidi kwa afya yetu vitasema, lakini kama hizo taarifa za hivyo vyombo viwili hazijatoka, nadhani itabidi uondoe huo mchango wako Mheshimiwa Rehani, karibu.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lakini ndio kwanza nilikuwa nikifikisha huu ujumbe kwamba, mimi sina. Taarifa niliyokuwa nayo, yangu mimi mwenyewe ni ku- yale maji nikagundua hicho kitu, lakini za hizo nimeziacha kama zilivyo...

NAIBU SPIKA: Sawa, basi ngoja tuongozane vizuri. Kama taarifa hii ni ya kwako wewe, hiyo tunaondoa kwenye mchango wako kwa sababu moja tu, mimi nitakavyokunywa maji ninavyosikia ladha ni tofauti na wewe, kwa hiyo, hizi ladha za kwetu sisi tukizitumia itatupa mtihani. Kwa maana hiyo, tunasubiri taarifa za wataalam ndio zinazopaswa kusema kitu gani kina shida ipi ama kimeongezeka wapi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rehani, huo mchango kuhusu hayo maji ya hiyo kampuni uliyoitaja unaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimelikubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba, tuwe na uchunguzi wa maji na vitu ambavyo tunavitumia viendane na ubora na mahitaji yetu halisi kwa sababu, sasa hivi hasa kwenye uapnde wa maji kumekuwa na makampuni mengi na kila mmoja anatangaza kwa anavyojua. Sasa nafikiri tungepata uelimishaji halisi kukawa na za viwango ambavyo

vitaweza kutumika kwa ajili ya maji ambayo tunayatumia katika maeneo yetu, sio leo ladha unaikuta hii, kesho ladha unaikuta nyingine ya maji yaleyale ambayo tunayatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, suala la ni janga ambalo udhibiti wake una ugumu wake; mimi nimeona kitu kimoja ambacho pengine na wenzangu hawajaki- hasa suala la kusambaa kwa . Katika maeneo yetu mengi na watu ambao wanatusaidia kuweza kututibu bado naona kama ni sehemu hatarishi, hasa kwa Manesi na Madaktari...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rehani, lakini nadhani angalizo lako ni la muhimu kwa sababu, hospitali tunakwenda, lakini kama yule anayetuhudumia amepata hiyo changamoto, tutazame namna ya kulishughulikia hili upande wa Serikali. Wakati mwingine sisi tunaweza kuwa hatuna barakoa kwa sababu, ndio naenda hospitali, lakini daktari ya kwake angalau wayazuie kuyaleta kwangu, asante sana.

Mheshimiwa Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Ally Hassan King ajiandae.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza niipongeze Serikali kiujumla kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi chini ya Wizara hii akiongozwa na Makamu wa Rais, mama yetu, Waziri mwenyewe pamoja na Manaibu na watendaji wote kwenye hii Wizara.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la Muungano. Kwanza naomba tu niungane na wenzangu kumshukuru Mungu na kusema kwamba, Mungu aendelee kuwarehemu waasisi wetu Marehemu Baba wa Taifa na Mzee wetu Karume kwa namna ambavyo waliweza kuweka Muungano huu ambao una faida 98% na tunaona changamoto ni kama 2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano sisi nchi tu za Afrika ya Mashariki tumeweza kuungana, tunaona faida tuliyonayo, lakini zaidi ya hapo kati ya Zanzibar na Tanganyika zilivyoungana na tuna Tanzania tuna faida kubwa sana, si lazima nikitaje hapa, lakini wengi tunazijua, naomba tuendelee kuzisimamia, ili tuendelee kuwa katika nchi yenye amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala la mazingira naomba nianze na suala la upimaji wa maeneo. Niombe Wizara ya Ardhi inayosimamia masuala mazima ya upimaji na kutengeneza zile basi kwa namna moja au nyingine washirikiane pamoja na Wizara hii yenye dhamana na mazingira, ili kuhakikisha kwamba, changamoto ambazo zinaweza kutokana na mafuriko zinakuwa hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetokea maeneo mengi sana ya nchi upimaji unaenda mpaka kwenye vyanzo ambavyo ni vya maji, upimaji unaenda mpaka kwenye kingo za mito, kwa hiyo, inakuwa inakinzana na sheria inayosimamia mazingira. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwe na ambayo baadaye haiumizi wananchi. Ukiangalia maeneo mengi ya nchi kuna maeneo ambayo ni maji yanajaa na baadaye mpaka viwanja vinapimwa na wananchi wanajenga na maeneo mengine upimaji unaenda unazuia mpaka zile njia za maji kupita. Kwa hiyo, tuombe sana Wizara hizi ziwe na mahusiano ya karibu, ili kuondoa adha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tu, bahati nzuri Waziri mwenyewe anatokea kwenye Mkoa wa Dar-es-Salaam, naomba atembelee eneo la Mbweni, Mtaa wa Teta.

Jana nimeweza kuona kwenye vyombo vya habari Brigedia Mstaafu, Mzee Chacha wiki nzima bado anatumia kuvuta maji kutoka kwenye mji wake, eneo zima limejaa maji, barabara haipitiki, nyumba takribani kaya 50 wananchi wamehama Mbweni wameenda kupanga kwenye mahoteli na kwenye nyumba za Ndugu zao wameenda kukaa. Kwa hiyo, yote hii ni kutokana na kwamba, hakuna miundombinu ya kutoa maji kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba utembelee Mbweni, Mtaa wa Teta, nimeona kwenye vyombo vya habari. Pia, nimeona hata Diwani akilalamikia hilo, Mwenyekiti wa Mtaa na ni tatizo la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kutoa malalamiko bahati nzuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilimfikishia. Basi tunakumbusha tena ili waweze kutatua changamoto hii maana baadaye Mheshimiwa Lukuvi anakuja kwamba, wananchi hawaendelezi viwanja vyao. Sasa hawaendelezi kwa nini, maeneo yao hayo yanajaa maji na gharama yake haizidi bilioni tatu. Kwa hiyo, tuombe waangalie eneo hilo, ili wananchi waende wakaendeleze viwanja vyao na sasa wakazi waondoke kwa kutokana na athari za mvua na maji kujaa mtu anaweza kupata kipindupindu, anashindwa kufanya kazi za kiuchumi na sasa hivi tunambiwa corona kwenye ubaridi vidudu vinaishi sana, kwa hiyo, yote hii ni hatari kwa wananchi kiujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na sera. Imeelezwa vizuri kwamba, sera ya mazingira sasa inasubiri kwenda kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kwenda kupitishwa. Tuombe sasa basi na mabadiliko ya sheria mbalimbali kutokana na sera ambavyo sasa imeboreshwa na yenyewe yaende yakazingatiwe na sheria ziboreshwe kutokana na sera ambavyo imeweza kuboreshwa. Kwa hiyo, mchakato mzima unavyoenda na hili suala linaweza pia likaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na kutunza mazingira kiujumla katika nchi yetu. Naomba tuchukue Dar-es-Salaam kama iwe ni _____ ya kuhusiana

na kuondokana na matumizi ya mkaa. Dar-es-Salaam ina watu takribani milioni tano na wanatumia sana mkaa na wameshaanzisha zoezi la kusambaza gesi asilia. Sasa tuingie kwenye namna ya uwezeshaji ambapo gesi iweze kutumika sana kwenye Jiji la Dar-es-Salaam na tukitoka hapo twende kwenye miji mikubwa, ili tupunguze uvunaji wa miti ambao una athari kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania na sisi ni nchi ambayo inalisha bahari kwa maji mengi na mvua nyingi sana. Kwa mfano Mkoa wa Katavi tumekuwa na mvua nyingi sana mwaka huu na mikoa mingine tofauti na miaka 10 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na hizi nchi duniani ambazo zinatakiwa zichangie kwenye kutunza mazingira. Kumekuwa na habari kwamba, nchi nyingi hazichangii, sasa kama Tanzania je, michango hii tumepata ipasavyo? Kama mtu hachangii, sheria iboreshwe ili kuweza kuwabana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saed Kubenea atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, tutamalizia na Mheshimiwa Hadija Hassan Aboud.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Muungano na Mazingira. Kwanza nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioathirika na janga hili la na nimwombe Mwenyezi Mungu atuepishe na janga hili kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi ni Wabunge, ni Bunge, ni watu ambao tumepewa mamlaka makubwa sana na wananchi, tuache kuzomea Serikali, tuache kuzodoa na tuache kujifanya hamnazo, hii nchi ni yetu sote. Ukiamka asubuhi unakuta kwenye mitandao zinakera kabisa

ambazo haziisaidii Serikali wala hazisaidii wananchi wetu. Nishauri sana kama Mbunge una ushauri mzuri kwa Serikali, peleka kunakohusika unaweza ukasaidia zaidi kuliko kuleta taharuki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niwape hongera sana baadhi ya Watanzania wenzetu, wafanyabiashara wadogowadogo na wakubwa waliojaliwa kutoa kile ambacho Mwenyezi Mungu amewapa katika kusaidia katika mapambano haya. Nimshukuru sana mfanyabiashara, Ndugu yetu Rostam Aziz, ambaye amejitolea pamoja na wafanyabiashara wenzake angalau kuleta mazingira mazuri ya wananchi wetu wa Dar-es-Salaam na maeneo mengine waweze kupambana na janga hili na huu ndio uzalendo kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya, Dada yangu Umy na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mchango mkubwa na kazi kubwa wanayoifanya katika kuelimisha umma na kutoa taarifa juu ya gonjwa hili la . Mwenyezi Mungu awape nguvu, awape uwezo na awape baraka za kuendelea kutusaidia na kuwasaidia Watanzania wenzao katika kipindi hiki kigumu tunachopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika kero za Muungano. Kuna watu wamezungumza wengine wakaita changamoto, lakini nasema hizi ni kero na kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili; neno changamoto mana yake ni hamasa, kutia ari, kuwa na hamu ya kufanya jambo. Kwenye Muungano, kwenye nyaraka zote zilizopo katika Muungano zinazungumzia kero za Muungano. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati akifungua Bunge la 10 alisema kwamba, ataenda kupambana na kero za Muungano, kwa hiyo, hizi ni kero na zimekuwa kero kwelikweli kwa miaka 40 na zaidi sasa ni kero ambazo hazijawahi kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoshangaa ni watu sisi kukataa ukweli kwamba, tuna matatizo makubwa

katika Muungano wetu. Ni kweli kwamba, baadhi ya kero zimeondolewa ikiwemo kero ya umeme ambayo Shirika la Umeme la Zanzibar, lilikuwa linanunua umeme wa na kulipa kama mtumiaji wa kawaida kwa msaada wa Wabunge na mchango wa Wabunge, kero hii iliweza kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo kero ambazo zinatokana na Katiba ya Zanzibar pamoja na Katiba ya Muungano. Kumekuwa na watu ambao wamekuwemo katika Serikali ya Zanzibar kwa miaka kdhhaa na bado mpaka leo hii hawaoni kwamba, Katiba ya Zanzibar ina matatizo makubwa kabisa ambayo yanaifanya ikinzane na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 77.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ibara ya 1 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, naomba niinukuu, inasema: "Zanzibar ni nchi ambayo mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vinayoizunguka bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar". Ibara ya 2 inasema: "Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti haya ni kinyume na Katiba ya Muungano, Ibara ya 1 inayotamka Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukisoma Katiba hii kwenye ibara za mwanzo tu zinapingana na Katiba ya Muungano na Katiba ya Zanzibar. Haya ni matatizo ambayo yamekuwepo kwa zaidi ya miaka 50. Baadhi ya watu wamekuwepo katika Serikali ya Zanzibar wakiwa viongozi wakubwa wameshindwa kuyatatua wanasema, eti tumeungana kwa hiari, kuna matatizo ya msingi yanaletwa na huo Muungano wa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar Ibara ya 26, inatamka kuwa Rais wa Zanzibar ni Mkuu wa nchi ya Zanzibar lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 32(2) inatamka Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Viti vinavyopingana

kabisa na Katiba ya Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Tayari kengele ya pili imegongwa.

WABUNGE FULANI: Aaaa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Mussa Sima ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, nashukuru sana kupata nafasi hii na pia tulishukuru Bunge lako Tukufu hili kwa kuwa na mambo haya ya kimtandao na teknolojia mpya ambayo tunawasiliana sehemu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kama vitu vyote unaweza ukavizungumzia, vingine ukivisema kiufupi vinafahamika. Huyu mzungumzaji aliyepita aliyezungumzia muundo wa Muungano akasome hesabu za atajua. Ni somo la darasa la tisa kwamba katika ukichukua mbili ukaweka pale, ukafanya kile kinachokuwemo katika umbile moja inakuwa ni moja, wa nje anakiona moja lakini ndani itaonekana kama zilikuwa mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tumrejee Mwenyezi Mungu, mtu asiyekuwa na fadhila ni sawasawa na punda/mnyama. Mtu asiye na fadhila ni sawa na mnyama. Kwa hiyo,

16 APRILI, 2020

unapomfanyia mtu harudishi shukrani basi inakuwa ni sawa na mnyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mimi niulize, katika ndoa ya mke na mume, wanapokuwemo ndani wakifanya mambo yao, kila mmoja akitimiza haki na wajibu kwa mwenzake hawaambizani ahsante? Hamna haki na wajibu mle? Basi hata hili mtu linamshinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo moja ambalo limesemwa hapa. Watu wametaja habari ya Serikali tatu. Nchi zetu zimeungana lakini kuna nchi ina uchumi mkubwa na kuna nchi nyingine ina uchumi mdogo. Tuna mambo yetu ya Muungano, yale pale tumeweka tunataka kuyafadhili, kwa hiyo hapa ndipo unapoweza ku-kwamba uwe na Serikali ngapi. Tazama ya Zanzibar na ya Tanzania nzima. Leo tuna shughuli za Muungano, kwa mfano, tumeweka hizo Serikali tatu, Rais wa Tanganyika atakuwepo, akisema sichangii, shughuli zitaenda?

MBUNGE FULANI: Haziendi.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu wanapokaa ni lazima wawe wanaweza kupima na wawe na akili ya kuzungumza jambo.

T A A R I F A

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, taaria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ali King, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Seleh aliyepo Msekwa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Ali Hassan King kwamba tulipokuwa Tume ya Warioba tuliambiwa kwamba kuna imefanywa na ile imeonesha kwamba fedha za Muungano zilizopo zinaweza kuendesha Serikali ya Zanzibar, zikaendesha Serikali ya Tanganyika na zikaendesha

na Serikali ya Muungano na wote wakapata maslahi yao. Kwa hivyo, nataka kumuarifu kwamba ya pesa siyo ikiwa tutakubaliana. Ni kufuata misingi tu kwa sababu pesa Tanzania ziko za kutosha kuendesha Serikali tatu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, nafurahi kusikia kwamba unasema Serikali ina fedha za kutosha. Mheshimiwa Ali King unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ningepokea maana yake ningekuwa na mimi mtu mmoja wa ajabu sana. Kwani hilo walilolisema limekuwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea. Muungano wetu huu ni wa ridhaa na mimi nitumie msemu mmoja niseme kwamba udugu wetu ni hazina. Leo ukitazama katika randama na katika hotuba ya Waziri, kuna mambo ambayo siyo ya Muungano yametajwa na Wizara chungu nzima pale zimeorosheshwa kwamba zimekutana na mambo yamefanyika ambayo sio ya Muungano kwa sababu udugu wetu huu ni hazina. Kwa hiyo, hii hazina sisi hatuwezi kukaa tukasema kwamba tunaitupa ambapo tunaweza tukaja tukaipoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muungano ni wa maridhiano hatusemi kwamba halitoweza kutokezea jambo ambalo likakwaza upande mmoja au mwingine. Kwa hiyo, nami niseme yale mambo ambayo ninayaona kwamba yanakwaza lakini yakafanyiwe kazi na ndipo tunapokutana humo. Ndiyo maana tuna Wizara ya Mambo ya Muungano hapa kwa sababu yakitokezea hayo mambo yataenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda kulizungumzia ni ambalo alilizungumza Waziri wa Fedha katika bajeti kubwa iliyosomwa mwaka jana ambapo alitoa ahadi kwamba kuna mambo matatu yanaenda kujadiliwa katika ofisi ya Makamu wa Rais. Jambo lenyewe

16 APRILI, 2020

ni upatikanaji wa fedha kuhusiana na mkopo wa bandari ya Mpigaduri, uwanja wa ndege na barabara. Aliyasema haya na mimi naamini Serikali yangu ni ya kiungwana na hilo jambo litashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna lingine zuri ambalo amelisema hapa Mheshimiwa Saada, naamini kwamba mtemewa mate na wengi hulowa na mimi nalisema, nalo ni suala la bei ya umeme. Mheshimiwa Waziri wa Nishati alituambia kwamba jambo hili linafanyiwa kazi, kwa hiyo, tuone ile kazi iliyofanywa matokeo yake ni yapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni bidhaa ambazo zinapigwa Kuna watu wananunua bidhaa Bara wanaenda nazo Zanzibar, Bara anachajiwa kwa sababu huku hajatimiza ile kwa hiyo, inakuwa na Kwa hiyo, anaponunua huku pengine ni taasisi ya kijamii, inahudumia mambo ya dini, shule au mambo mengine ya kijamii, sio ya kibiashara lakini anatozwa mara mbili. Nalisema tena, tuliambiwa kwamba litashughulikiwa, naomba lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lingine ambalo ni la muhimu kulizungumza, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kushikamana na wananchi katika kuongoza suala hili. Kuna msemo mmoja wa kiarabu unasema: kuondosha ufidadi kunatangulizwa halafu baadaye ndiyo utatazama maslahi. Janga la ni fidadi kubwa sana, kwa hiyo, ndiyo kwanza tutangulie kulitazama baadaye kama kuna kitu cha maslahi tutakiangalia kitu cha maslahi. Kwa hiyo, Rais wetu amesema hivyo, wananchi wachukue tahadhari kama zinavyosemwa na Serikali katika kufanikisha suala hili ili hili tatizo liondoke.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu amesema kwamba...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ali King, muda wako umekwisha. Kengele mbili zimeshagonga, ahsante.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, nipe dakika moja nimalizie hiki tu.

NAIBU SPIKA: Muda wetu pale kidogo unanibana, shukrani.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Medard Kalemani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Spika wetu, wewe na watendaji wenzako wote kwa kulingoza Bunge letu kwa umahiri hadi kufikia sasa tunamaliza Bunge. Bunge hili ni sehemu moja kubwa ya Muungano wetu. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze na upande wa mazingira. Wizara imetueleza mipango na mikakati mbalimbali ya kutunza na kuhifadhi mazingira. Napenda

16 APRILI, 2020

kusisitiza kwamba mazingira ni muhimu na mazingira ndiyo nchi yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uhifadhi wa misitu na mazingira kwa ujumla wake, pia nguvu kubwa elekezewe katika Ukanda wa Pwani na hasa ukanda wa visiwa. Visiwa vyetu vya Zanzibar, Pemba, Mafia na vingine vidogovidogo, kuna hatari ya kupotea hapo baadaye. Hadithi zinasema kuna baadhi ya visiwa huku duniani vimeshapotea na sasa hivi visiwa vyetu vinakabiliwa na hali mbaya ya maji ya bahari kupanda juu na baadhi ya nyumba zimeshafunikwa. Kwa hiyo, nasisitiza uhifadhi wa mazingira katika Ukanda huu wa Pwani na Ukanda wa Visiwa vyetu ili visiwa hivi viweze kudumisha huo Muungano na nchi hii irithiwe kama ilivyo Bara pamoja na Visiwa vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye upande wa Muungano. Napenda kuwapongeza viongozi wetu wakuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, kwa umahiri na upendo wao na kujitoa kwao kwa dhati kuhakikisha Muungano huu unadumu na unaendelea kuwepo kwa manufaa ya vizazi vya leo na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza viongozi wote wa Awamu zilizopita kutoka waasisi wa Muungano huu, Mwalimu Nyerere na Hayati Baba Abeid Aman Karume kwa kuanzisha jambo hili lenye busara na hatma yetu Watanzania kwa ujumla. Baada ya hapo zikafuata Awamu nyingine ambazo zililiendeleza wazo hili kwa umahiri na kwa upendo kabisa hadi kufikia hapa tuna majemedari wetu hawa wawili, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Dkt. John Pome Magufuli, nawapongeza kwa dhati. Naomba waendeleo na jitihada zao za kuhakikisha wanaulinda Muungano huu, wanautetea kwa amani na kwa vitendo kwa manufaa yetu sote Watanzania na manufaa ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea hapo kwenye Muungano, Muungano wetu ulianza kuwa na siku moja,

tarehe 26 Aprili, 2020, unatimiza miaka 56. Hii inamaanisha kwamba Muungano huu haukusimama, Muungano huu unakua. Kila kinachokua, kinakuwa na tatizo na changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jinsi Muungano unavyoendelea kuwepo, yatajitokeza mambo mbalimbali ambayo naamini kwa viongozi wote watakaokuwepo wataendelea kuyatataua kwa wakati muafaka kwa manufaa yetu wote sisi Watanzania. Muungano wetu huu umeleta upendo, amani na mawazo ya viongozi wetu walioipita ni mawazo sahihi kwamba Muungano wa Serikali mbili ndiyo Muungano sahihi kwa nchi yetu ya Tanzania na ndiyo maana tunatimiza miaka 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano huu ni wa vitendo, siyo wa maneno. Kuna Wizara ambazo hazihusiki na Muungano, mfano afya, kilimo, maji lakini tunaendelea kupata fursa hizi za Muungano kwa sababu Wizara ya Kilimo ya Zanzibar na Wizara ya Muungano zinashirikiana, Uvuvi, maji hali kadhalika. Kuna miradi ya India Zanzibar tumepewa sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza miaka 56 ya Muungano, tumetoka mbali sana lakini napenda niongeze kitu kidogo. Katika Muungano huu tuna jina letu Tanzania, jina zuri sana na lenye haiba. Kuna bendera ya Tanzania na kuna wimbo wa Taifa. Napenda kuishauri Wiza ya Muungano, aliyetunga jina la Tanzania, aliyechora bendera ya Taifa pamoja na aliyetunga wimbo wa Taifa na kuweka naomba watu hao watafutwe na waenziwe kwa sababu historia itapotea kwa vizazi vijavyo. Leo hii tukiulizana ni nani katunga jina Tanzania, wengi wetu hatujui.

Mheshimiwa Naibu Spika, navipongeza vyombo vya habari kwa kuibua mambo yaliyopita. Niliona kwenye gazeti moja waliandika aliyetunga jina la Tanzania lakini nani anamjua aliyetunga jina Tanzania, suala hili nataka Wizara ya Muungano iweke kumbukumbu hiyo. Kama walivyowatafuta wale waliochanganya udongo, wale vijana wanne wakajulikana na kutambuliwa na siku za sherehe za

16 APRILI, 2020

Muungano wanaalikwa na hawa waliotunga jina hili la Tanzania, jina lenye haiba linalotupa sifa duniani, bendera yetu, wimbo wa Taifa, watafutwe, wajulikane na iwe inatolewa kila baada ya muda ili vizazi vyetu viweze kufahamu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, dakika tatu, atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, dakika tatu na Mheshimiwa Musa Sima ajjandae.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Muungano na Mazingira imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya Muungano na Mazingira hasa kushughulikia kero za Muungano na pia masuala ya mazingira hasa kipindi hiki cha kupambana na changamoto za kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, napendekeza kuongezwa kwa juhudi za

kupambana na uharibifu wa mazingira unaopelekea kupotea kwa misitu na uoto wa asili. Misitu ya Mbeya inaharibiwa kwa uchomaji moto holela unaohatarisha upungufu wa mvua, kukauka kwa vyanzo vya maji na maporomoko ya udongo unaohatarisha uharibifu wa Ziwa Rukwa.

Napendekeza kuwepo kwa mkakati wa kunusuru mito na hata vyanzo vyake mito mikubwa inayopeleka maji Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Mto Ruaha na Mto Rufiji inayolisha mabwawa ya Mtera na Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wakuu kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani. Nawapongeza sana kwa kufanikiwa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki. Naomba muendelee kufanya ufuatiliaji ili isije ikarudishwa kupitia milango ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunapitia kipindi kigumu cha mafuriko katika sehemu nyingi hapa nchini. Mojawapo ya sababu ya mafuriko haya ni mvua nyingi na wananchi wengi waliojenga ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji kama mito, ujenzi huu umesababisha mmomonyoko wa ardhi, udongo mwingi kuingia kwenye mito na kupunguza kina cha mito, pia ujenzi huu umefanya maji yakose njia zake za kupita za kawaida na hivyo kusambaa na kusababisha mafuriko. Pamoja na kuwa viongozi wapo kila mahali, wanaona watu waovamia kujenga kwenye vyanzo vya maji, lakini hawakatazwi, wanaendelea kujenga kwenye vyanzo. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaondoa watu hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuendelea kuhamasisha upandaji wa miti. Tatizo ni kuwa miti inapandwa lakini haitunzwi. Napendekeza kuwe na utaratibu wa kulea na kuendelea kuhudumia miti inayopandwa hapa nchini.

16 APRILI, 2020

Mwisho, mabadiliko ya tabia nchi ni janga lingine la kidunia. Je, Wizara inahakikishaje kuwa Watanzania wanaelewa vizuri athari za mabadiliko ya tabia nchi, namna ya kuyathibiti na namna ya kukabiliana nayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, kumpongeza Waziri Azzan Zungu, na Naibu wake Mheshimiwa Sima pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri ya kulinda mazingira ya nchini kote Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi nina mambo machache ya kuchangia katika Wizara hii; kwanza tunazo Wilaya ambazo ziko kwenye kandokando ya Maziwa na Mito, tatizo kubwa wananchi waliopo kwenye maeneo hayo hawatambui kwa mujibu wa sheria wanatakiwa wafanye shughuli umbali wa mita ngapi na pia kwenye kujenga nyumba wanatakiwa kujenga umbali wa mita ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusiana na suala la vibali vya uchomaji mikaa. Kuna maeneo hayana athari ya uharibifu lakini wananchi wanapoomba vibali vya kuchoma mkaa hunyimwa, sasa nafikiri ni vyema kanuni na sheria za uharibifu wa mazingira ziwe zinatafsiriwa kwa lugha yepesi ili wale wananchi waliopo huko chini waweze kuzielewa na kuzitekeleza kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la limekuwa na usumbufu sana wakati wawekezaji wanapotaka kuanzisha viwanda vikubwa na hata wazawa wanapotaka kuanzisha viwanda vidogo inachukua miaka kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kuwapitishia taarifa zao na lingine yake iangaliwe kwani ni kubwa haiendani na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niombe kanuni na sheria za mazingira ziangaliwe upya ili kutoa urasimu kwa wafanyabiashara wa ndani na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kutoa maoni yangu katika Wizara ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili miradi iliyopangwa itekelezwe kwa wakati. Pia naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi hususan katika dhana ya kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ili kuondokana na ukataji miti hovyoy kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa, Serikali ifanye jitihada za makusudi isambaze gesi ya bei nafuu majumbani kama ilivyofanya kwenye maeneo ya Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu kwa viongozi wa Halmashuri nchini kote kuzingatia sheria za mazingira, kuna maeneo ambayo hayapaswi kupewa vibali kwa ajili ya ujenzi, mfano Morogoro Mjini wananchi wamejenga juu ya milima ambako kuna vyanzo vya maji, hii inaleta uharibifu mkubwa na Halmashuri inatoa vibali vya ujenzi, hivyo imeleta athari kubwa kwa kusababisha uharibifu wa mazingira, hivyo elimu kwa watendaji wa Serikali itolewe.

Pia naishauri Serikali kampeni ya upandaji miti katika Halmashauri zetu ione haja ya kupanda miti mchanganyiko ikiwemo na miti ya matunda, hii itasaidia kutokata miti hovyoy sababu ni vigumu kwa mwananchi kukata mti wenye matunda, hivyo ukataji utapungua kwa kiasi kikubwa.

Pia naishauri Serikali iongeze fedha za ndani za kutosha kuliko asilimia kubwa ya fedha za mazingira inategemea wadau kutoka nje kutunza mazingira yetu ambayo pia haifiki kwa wakati.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza mchango wangu kwenye Wizara hii, kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha leo kutoa mchango wangu katika hotuba hii. Pia nitumie fursa hii kuendelea kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulliongoza Taifa letu kwa umahiri mkubwa na kuendelea kudumisha Muungano wetu kwa amani na utulivu mkubwa.

Lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa namna anavyoendelea kulliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa na kwa njia za kisasa zaidi, unajitahidi kulifanya Bunge letu liwe Bunge la kisasa zaidi, hasa kulifanya liwe Bunge mtandao.

Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii ya Muungano na Mazingira sambamba na Naibu wake, pia nimpongeze Katibu Mkuu na Naibu wake. Wote hao kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kufikia malengo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze mchango wangu kwa kuishauri Serikali kuhusu uharibifu wa mazingira nchini. Uharibifu wa mazingira hapa nchini bado ni mkubwa hasa kwa upande wa kilimo cha kuhama hama, kwa kuwa bado tunao wakulima wanaolima kilimo cha kutumia jembe la mkono na cha kizamani. Wakulima hawa ulazimika kuhama mara kwa mara, hivyo husabibisha ukataji mkubwa wa miti na kuharibu uoto wa asili. Kwa mfano katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kumeibuka uhitaji mkubwa sana wa mashamba ya ufuta. Mashamba haya hudumu si zaidi ya miaka mitatu, hivyo mkulima hulazimika kutafuta shamba jipya na hivyo kuendelea kukata miti bila kujali athari za mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika kuelimisha wananchi juu ya kilimo cha kisasa na matumizi sahihi za kilimo bora na matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo. Kilimo cha ufuta na korosho kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kisipoangaliwa kwa

upana wake ndicho chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira kwa mikoa hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchomaji moto na matumizi ya kemikali katika kuchoma miti na kuangamiza misitu imekuwa ni jambo la kawaida kwenye mikoa hiyo. Sehemu nyingine yenye uharibifu mkubwa wa mazingira ni ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya ufugaji wa kisasa. Wafugaji wetu wengi kwa sasa wamekuwa wakisambaa nchi mzima bila ya kuwa na mipango madhubuti ya utunzaji wa mazingira kule ambako wafugaji hao wanakohamia, ni bora Serikali ikatoa mwongozo utakaoonesha idadi ya mifungo na ukubwa wa eneo husika. Kwani kwa sasa kuna mlundikano mkubwa wa mifugo katika sehemu mbalimbali nchini kunakosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Idara za Mazingira au wataalam wa mazingira katika Halmashauri zetu ni changamoto kubwa sana kwani Halmashauri nyingi nchini hazina wataalam wa kada, hii jambo linalo zifanya halmashauri zetu nyingi kutekeleza miradi mingi bila kuzingatia athari za mazingira, na pengine kusababisha migongano ya kwenye idara mbalimbali, mfano miradi ya barabara inayo husisha uchimbaji wa kokoto na vifusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishuri Wizara kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za Muungano ili kuendelea kudumisha Muungano wetu, Muungano ambao ni wa kupigiwa mfano duniani kote. Muungano ambao ni moja ya tunu ya Taifa letu, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kwa mujibu wa nafasi yake anawajibu wa kuenzi Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa Muungano wetu. Aidha, napenda

16 APRILI, 2020

kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuiwasilisha kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu mazingira; nchi yetu inakabiliwa na matatizo makubwa ya uharibifu misitu. Hii inatokana na matumizi mabaya ya kuni kwa ajili ya matumizi ya kupikia. Hii inafanywa na watu wa aina zote, masikini na watu wa kipato cha kati. Ushauri wangu katika suala hili kwa Serikali ni kutafuta njia mbadala. Kwa kuwa Serikali yetu inaendelea na zoezi la kupeleka umeme vijijini Serikali itengeneze mikakati maalum ya kuwawezesha wananchi namna ya kutumia umeme kwa shughuli za mapishi. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya ukataji wa miti kwa ajili ya kuni.

Pili ni kuhusu Muungano; Muungano wetu ni Muungano wa kihistoria ulimwenguni kote. Huu ni Muungano imara unaohitaji kuenziwa kwa nguvu zetu zote. Ushauri wangu katika suala hili kwa viongozi wetu kuwa wastahamilivu na wasikivu kwa wananchi wanapoleta changamoto za Muungano ili kuzitatua kwa maslahi ya p zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu wa maandishi kwenye hoja iliyoko mezani, hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nitamke kwamba naunga mkono hoja na ninamp ongeza Waziri Musa Azzan Zungu na Naibu wake Mheshimiwa Ramadhan Sima kwa kazi nzuri wanayoifanya katika masuala ya Muungano wetu na uhifadhi wa mazingira yetu. Pia nampongeza Rais

wetu Dkt. John Pombe Magufuli na Makamu wake Mama Samia Suluhu kwa uongozi wao makini na hamasa yao katika kudumisha Muungano na kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia katika maeneo machache kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Musa Zungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kampeni ya upandaji miti; mradi huu hautaweza kufanikiwa katika Wilaya kame kama Longido, Serikali isipowekeza kwanza katika miradi ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingi vyenye ardhi ya kutosha na ambayo ingefaa kupanda miti haina maji kwenye Wilaya kame za nchi yetu na njia ya kuondoa changamoto hii ni Serikali kuchimba visima virefu na kuchimba mabwawa ya kukinga maji ya mvua ili wananchi waweze kuhamasishwa kupanda na kutunza miti kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile baada ya kutatua changamoto ya maji katika maeneo kame ya nchi yetu, ili tufanikiwe kunusuru mazingira yetu kutokana na tishio la mabadiliko ya tabia nchi, kuna haja ya Wizara kuanzisha kampeni pana ya kitaifa ya kuagiza kila mtu na taasisi katika nchi yetu kupanda japo mti mmoja hadi 10 kwa mwaka na kuitunza ili tufanikiwe kuifanya Tanzania kuwa ya kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa moja ya machimbuko ya uharibifu wa mazingira ni utegemezi mkubwa wa Watanzania kwenye nishati ya kuni na mkaa, Wizara ihamasishwe uanzishwaji wa kwenye kaya na taasisi zote zinazotegemea kuni na mkaa kama nishati ya kupikia ili watumiaji wawe wanavuna mazao ya miti waliyojipandia badala ya kuiharibu misitu tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili bei ya gesi ishushwe na Watanzania wahamasishwe kutumia gesi badala ya kuni na mkaa.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine na muhimu zaidi kwa sababu ni rafiki kwa mazingira, ni Serikali kuwekeza kwenye miradi ya matumizi ya nishati jadidifu kama vile nishati ya jua na upepo. Uwekezaji katika rasilimali ya jua na upepo utatusaidia sana kunusuru mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mimea vamizi, ninaishauri Serikali iwekeze katika tafiti za kubaini aina ya mimea vamizi zilizovamia katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kuanzishwe miradi inayoshirikisha jamii kwa mfumo wa nguvu kazi na ama ambapo vijana na watu wasio na ajira wanapewa vibarua ya kuondoa na kuteketeza mimea hiyo. Ipo mimea ya aina mbalimbali katika maeneo ya malisho vijijini, mashambani na pembezoni mwa barabara zetu ambazo tusipokuja na mkakati kabambe wa kupambana nazo kuziondoa zitakuja kutuharibia ekolojia ya asili ya maeneo yetu na mingine ina sumu na huaribu mazingira, kwa mfano gugu karoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, mosi nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika.

Suala moja tu muhimu ambalo ningependa kufahamu kuhusu mradi wa kuwezesha ardhi zilizoharibika na upatikanaji wa usalama wa chakula katika maeneo kame ambao upo mwaka wa pili wa utekelezaji wake katika Wilaya tano za Magu, Mkalama, Nzega, Kondo na Michewen Zanzibar. Tatizo fedha hazijatolewa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Tunashauri fedha zitolewe ili mradi huu muhimu utekelezwe ikiwemo Mkalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wa Taifa letu,

16 APRILI, 2020

Wabunge wenzangu, wananachi wote kwa ujumla, kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu amani, ulinzi, mshikamano, upendo na mafanikio makubwa sana katika kipindi cha miaka hii mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Watanzania kuungana wote kumwomba sana Mwenyezi Mungu atuondoshee janga hili la corona katika Taifa letu na dunia nzima. Watanzania tuzingatie maelekezo ya kitaalam kupambana na virusi vya corona kwa jinsi inavyotikisa dunia nzima kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa kwa jinsi alivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015 - 2020 kwa miaka mitano sasa aliyotuongoza, kwa kweli yapo mambo mengi sana yanayoifanya nchi yetu kuwa kielelezo Barani Afrika na dunia kwa ujumla, binafsi mimi nasema nchi yetu imechelewa kumpata katika kuongoza nchi.

Nawapongeza Mheshimiwa Makamu ya Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wote Waandamizi na watendaji wote kwa jinsi walivyolitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali mpango kabambe wa upandaji miti kitaifa kwa ngazi ya Kaya, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa kufanya mashindano yasiyo na gharama kwa kutoa cheti, ngao, miche na tuzo. Kila shule, chuo na taasisi kama hizo kupewa maeneo ya wazi kama milima, mabonde na vyanzo vya maji ili wapewe miche ya miti rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Halmashauri nchini iwe na mpango wa vitalu vya miche kwenye shule za kata kwa kuzipatia mbegu na vifaa vya kukuzia miche hatimaye kuzigawia shule za kata kwa ajili ya shule za msingi, sekondari na taasisi zingine.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kwa sasa Wakala wa Misitu Tanzania hajaweza kukabiliana na uharibifu wa misitu nchini kwa baadhi ya maeneo nchini, hivyo basi kufanyike tathimini ya kina kuhusu chombo hiki kwa kupitia sheria, kanuni na utendaji wake ili kuleta ufanisi zaidi na mafanikio makubwa kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na kwa namna ya pekee naipongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji wake mzuri katika kuiongoza Tanzania. Nampongeza pia kwa uamuzi wake wa makusudi wa kuamua kusitisha sherehe za Muungano na kuagiza fedha hiyo ipelekwe Zanzibar ifikishwe Wizara ya Afya zikatumike kwenye suala la tiba ya kuzuia maambukizi ya Corona Zanzibar. Hongera sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa juhudi zako za kujali wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kutokana na utendaji wake kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanazozifanya kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa utendaji wake kupitia miradi yote ya maendeleo iliyopo Zanzibar.

Naomba Serikali iendelee kutoa elimu kuhusu ili wananchi kuwa na uelewa zaidi wa kudhibiti maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa homa kali ya corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu makazi ya Makamu wa Rais Kisiwani Pemba yaliyopo Wete, Pemba ambapo mwaka 2008/2009 jengo la Ikulu Ndogo ya Jamhuri lilitengewa bajeti kwa ajili ya kufanyiwa ukaravati

wa jengo na ununuzi wa _____ za jengo hilo. Katika bajeti hiyo haikuweza kukidhi haja na kubaki maeneo kadhaa kwa ajili ya kusubiri bajeti nyingine. La kusikitisha hadi sasa jengo hilo halijaweza kutengewa bajeti ingawa nimeweza kusemea jambo hili siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kwa vile jengo hili kwa sasa lipo katika hali ngumu sana linavuja, limekuwa gofu na kupoteza hadhi yake kama makazi makuu ya viongozi wa Kitaifa, Serikali itenge muda muafaka kufanya ukaguzi maalum na kuona namna ya kulikarabati ili lisiendelee kupotea kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niunge mkono hoja ingawa ndiyo naanza kuchangia kwa dakika tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja moja tu ambayo imezungumzwa kwa upana sana katika masuala ya bei za umeme Zanzibar. Kwanza, nianze kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano kwa jinsi ambavyo wamelifanyia kazi jambo hili kwa upana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mambo mawili ya msingi katika jambo hili. Jambo la kwanza ilikuwa ni gharama ya kodi ya _____ kwenye mauzo ya umeme kwenda Zanzibar ambalo mwaka jana lilizungumzwa sana na kwa busara kubwa sana ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifuta gharama hiyo ya _____ ya shilingi bilioni 22.9. Kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo. Lilikuwa ni jambo lilichukua muda mrefu lakini baadaye lilifikia muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali ya Muungano wa Tanzania inawauzia umeme Zanzibar, kwa upande wa Unguja _____ 70 na Pemba _____ 8 na kwa ujumla wake ilifikia takriban shilingi bilioni 149. Jambo la msingi hapa ni gharama za kununua umeme. Zanzibar kupitia

16 APRILI, 2020

na Bara kupitia wanazo bei walizokubaliana lakini kwa busara ya Serikali hizi mbili ziliona jambo hili lifanyiwe kazi kwa umakini ili wenzetu wa Zanzibar ikibidi wapate unafuu wa gharama hiyo na ndiyo jambo linalofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa kutoa taarifa tu, kazi inayofanyika kwa sasa ni kama ifuatavyo. Wataalam walishakutana kutoka Novemba, 2019 na Makatibu Wakuu wa Serikali zote mbili kwa maana ya Zanzibar na ya Muungano walikutana mwezi uliopita na suala hili sasa linaletwa kwa Mawaziri. Jana Makatibu Wakuu walikuwa wanakamilisha taarifa hiyo ili Mawaziri wa Serikali zote mbili nao wakae na sisi tumejipanga ikiwezekana Makatibu wakimaliza tu tutakutana ili kushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naloweza kutoa taarifa hapa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa pande zote mbili wanaotumia umeme wawe na imani na Serikali, hili jambo litashughulikiwa kama ilivyofanyiwa kazi. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba jambo hili hatma yake itafikiwa muda si mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Musa Sima ajiandae.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi najielekeza tu katika kutoa ufafanuzi kwenye hoja aliyobua Mheshimiwa Kubenea inayoeleza kuwa kuna mkanganyiko au mgongano kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar na hasa kuhusiana na neno nchi au sifa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mambo ya msingi. Jambo la kwanza, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaitambua Katiba ya Zanzibar na kwa hiyo hizi zinaweza kutafsiriwa pamoja. Panapotokea mgongano kuna

msingi wa Kunapotokea mgongano wowote
katika Katiba, mojawapo ya msingi inayotumika ni msingi wa

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme mwenye mamlaka hasa ya kuizungumzia Katiba ya Zanzibar ni Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Ndiyo maana hata linapozuka suala la tafsiri ya Kikatiba kwa Katiba ya Zanzibar, kesi ile huishia katika Mahakama Kuu ya Zanzibar, haiendi katika Mahakama ya Rufaa ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea misingi hiyo, sasa moja kwa moja nijielekeze kwenye hicho kinachoitwa ni mgongano. Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 1 inasema Zanzibar ni nchi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 1 inasema Tanzania ni nchi moja na kwa hiyo hapa changamoto iko kwenye tafsiri ya neno nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno hili lina changamoto zake kwa sababu tumelitoa katika neno la Kiingereza, Sasa unapozungumzia neno _____ ya katika Sheria za Kimataifa, _____ zipo za aina nyingi na kuna _____ mbalimbali za _____ Kwa hiyo, unaweza kuwa unatumia neno _____ lakini unamaanisha nchi ya aina tofauti. Ndio maana Vatican ni

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja kidogo. Vatican inaitwa _____ na nyingine zote _____ lakini zina mbalimbali au zina mazingira mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukienda kwenye Katiba yetu au Katiba zetu pamoja na tahadhari niliyoitoa mwanzoni, Katiba ya Zanzibar inasema Zanzibar ni nchi na inakomea hapo. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema Tanzania ni nchi na ni Jamhuri ya

16 APRILI, 2020

Muungano. Hata tafsiri ile ya Kiingereza ninayo hapa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema:

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo kusema, tofauti kubwa iliyopo kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ile sifa ya Ujamhuri au Ndiyo maana Katiba ya Zanzibar inasema tu Zanzibar ni nchi lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema Tanzania ni nchi na ni Jamhuri ya Muungano kama ilivyoelezwa kwenye Kiingereza:
"

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti kubwa kati ya matumizi ya neno "nchi" kwa Zanzibar ni kwamba siyo Jamhuri; haina sifa ya ujamhuri na kwenye Muungano, ina sifa ya Jamhuri. Hii ndiyo tofauti kubwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunakushukuru kwa ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Mussa Sima, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na mtoa hoja atakuwa akijiandaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye pia ametuwezesha, leo tupo katika mjadala huu mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana na ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein. Nampongeza pia Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa maelekezo yao ambayo wamekuwa wakiyatoa na tumekuwa tukiyafanyia kazi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kuishukuru Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kweli imekuwa na maono mapana sana. Nimejaribu kufuatilia namna ilivyokuwa inatoa ushauri mambo; mawili tu niyataje ambayo imetuelekeza kwamba kuna haja sasa badala ya kuwa na tuwe na badala ya Baraza sasa tuwe na Hili ni jambo la kufanyia kazi, naishukuru sana Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imeona kuna haja ya wale Maafisa Mazingira walopo kule chini wawe chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Nawahsukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetoka hoja mbalimbali, nitagusa chache. Nianze na Mheshimiwa Dkt. Sware ambaye anataka kuwaaminisha Watanzania kwamba Serikali hii haijaweka kipaumbele suala la mazingira. Siyo kweli! Nataka tu nilieleze kwa mapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira umuhimu wake ulipowekwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, hiki ndiyo kipaumbele cha kwanza. Sasa kama imewekwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, maana yake jambo hili limepewa kipaumbele na sisi ndiyo Tunapozungumza Mifuko ya Mazingira Duniani ndani na nje, Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo inahusika. Kwa hiyo, imepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amezungumzia suala la ufinyu wa bajeti na vitu vingine. Sisi wajibu wetu ni kuratibu. Zipo Wizara za Kisekta, zipo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Maliasili na Utalii. Hizi zote zinashughulika na mazingira na bajeti zao zipo kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ally Saleh...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

16 APRILI, 2020

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Zainab Bakari ni kweli wamezungumza habari ya makazi ya Makamu wa Rais pale Tunguu, Zanzibar. Kweli wanatakiwa kulipwa fidia. Niwape tu wakazi wa pale kwamba sasa suala hili lilifanyiwa tathmini na lipo Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha imeunda Kamati. Wakati wowote Kamati ile itaenda ku-tathmini ambayo imefanywa watu wale waweze kulipwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bonnah Kamoli amezungumza suala la Mto Msimbazi. Nataka pia nimpe Tuliwakabidhi wenzetu wa ili waweze kuangalia gharama halisi na miundombinu ili iweze kuanza kujengwa kwenye eneo hilo la Mto Msimbazi. Pia Amegusia madampo, nataka niliseme hili kwa Halmashauri zote na nchi nzima, tunazungumzia taka ngumu lakini pia taka hatarishi pamoja na

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zinapaswa kuanzisha miradi zenyewe wala zisisubiri Serikali Kuu iwapelekee miradi. Zinapaswa kuibua miradi ya kuhakikisha kwamba inakuwa na mradi wa kuteketeza taka ngumu lakini na Halmashauri alizozitaja hata kama Iringa na Halmashauri nyingine ukienda Mwanza, miradi ile siyo ya Serikali Kuu, wameibua wenyewe kupitia mahitaji mingine ya

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Bonnah kwenye Halmashauri yake na Halmashauri nyingine waweze kuandika hiyo miradi, waweze kupata fedha na kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya dampo yanaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Masoud Nchambi amezungumzia habari ya wataalam elekezi. Nataka pia nimweleze kwamba tupo kwenye hatua za mwisho za marekebishao ya Kanuni yetu ya Wataalam elekezi

ambayo itakuwa na bei elekezi, hakutakuwa na bei kama ambavyo walikuwa wanajipangia mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni yetu hii ambayo tunatarajiwa wakati wowote itakuwa imeshakamilika na hao wataalam elekezi watakuwa wameelekezwa kama ambavyo sisi tumetoa. Ni kanuni ambayo inatuelekeza moja kwa moja, mwekezaji wa eneo fulani na eneo hilo, kwa mfano nichukulie suala la kituo cha mafuta (a) gharama yake labda ni shilingi bilioni nne; sasa tunamwelekeza na yule mtaalam mwelekezi, gharama yake haiwezi kuzidi pale, maana yake itakuwa chini ya shilingi milioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimwombe Mheshimiwa Nchambi kwamba wakati wowote kwa hoja yake hii ya msingi ambayo amelekeza sisi tumeshaitungia Kanuni na Kanuni zitakuwa tayari sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uhifadhi ya mazingira limeelekezwa katika Ibara ya 6 ya Sheria yetu ya mwaka 2004 kwamba ni jukumu la kila Mtanzania na kila anayeishi Tanzania katika suala la uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Sasa siyo jukumu tu la Serikali peke yake. Kwa hiyo, nataka niwaombe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kwamba ufike wakati sasa tuwe na jukumu hili la kutunza vyanzo vya maji na kuhakikisha kwamba hatukati miti ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Yussuf ameeleza vizuri, nami nataka nikubaliane naye na nimwambie tu Mheshimiwa Yussuf, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Makamu wa Rais mwenyewe katika kampeni yake ya kuhakikisha kila Halmashauri tunapanda miti 1,500,000, leo hii tumefanikiwa kwa asilimia 75. Namshukuru sana Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nitumie fursa hii kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

16 APRILI, 2020

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimuite sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi tena kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi na maelekezo aliyotupa na namna tunavyotekeleza maelekezo na maagizo kutoka kwake, kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Shein, kutoka kwa Makamu wa Rais, kutoka kwa Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Pili wa Rais. Hii ndiyo _____ ya Tanzania, timu ambayo inatuvusha na itatuvusha. Wanapiga mambo kama Simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi kumpongeza Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Mheshimiwa Najma, yeye ametoa pongezi nyingi sana kwetu, tunazipokea pongezi zake na ni kweli Serikali kupitia Hazina; anampongeza Waziri wa Fedha kwa namna walivyoweza kutekeleza bajeti ya Fungu 26 kwa asilimia 74 na hii ni Aprili mwaka huu, 2020; bado tuna miezi mingine miwili tunategemea tutafika mpaka asilimia 85. Hii yote inatokana na usimamizi mzuri wa Serikali kwenye makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti Kamati ya Biashara kwa pongezi zao. Vilevile Kamati ilipata fursa ya kwenda kutembelea miradi miwili ya Kinyerezi na Mradi wa _____ nampongeza sana Serikali. Mradi wa _____ na mradi wa Kinyerezi imeendana na ni rafiki kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye _____
masharti ya _____

ya _____
tuna-

16 APRILI, 2020

kupata misaada, kupata fedha kutokana na mchango wa Serikali kuanzisha miradi ambayo ni rafiki kwa mazingira. Kwa hiyo, napongeza sana Wizara na Serikali kwa namna mnavyoweza kuweka miradi kama hii ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya utekelezaji wa fedha za maendeleo kutoka kwa wafadhili

Hizi pesa zinatoka kwa wafadhili. Wafadhili wanapotoa hizi pesa hawatoi pesa kama tunavyotoa sisi katika Serikali yetu. Mradi unakuwa zaidi ya miaka minne. Kwa hiyo, pesa ikitoka haitoki asilimia mia, kila mwaka inapangiwa yake ya kutoka. Kwa hiyo, 23 kwa miaka minne inatimiza kabisa kukamilisha huo mradi. Kwa hiyo, msiwe na hofu kuona kwamba pesa hazitoshi, pesa...

MBUNGE FULANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Kaa kimya wewe!

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mfuko wa Mazingira. Mfuko huu sasa hivi uko katika maandalizi ya Makatibu Wakuu na karibuni tutakuwa na matokeo mazuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, suala la misitu amejibu Naibu na sasa hivi tuna kampeni siyo tu kupanda miti, bali kuitunza. Kupanda na kutunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fakharia ametoa pongezi, nasi tunamshukuru Mheshimiwa Rais. Shilingi milioni 500 siyo pesa ndogo, ni pesa nyingi sana, inahitaji ujasiri na upenzi. Pesa hii imetoka sababu ya upenzi, ujasiri na undugu kupeleka kwa wenzetu Wazanzibar ili nao wapate kunusurika na gonjwa hili.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tauhida yeye ametaka mimi niwe karibu, niwe katikati. Nitakuwa katikati, nitakuwa mbele na nitakuwa nyuma kuhakikisha akina mama wa Zanzibar wanapata matibabu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Sware ni mtaalam wa mazingira na kwa kweli bajeti sisi hatu- pesa za mazingira za nchi nzima. Kila Kilimo, Maji, Ardhi, Utalii na Maliasili wana mgao wao wa pesa za mazingira, hazitoki katika mfuko wetu, zinatoka kwenye mfuko ambao tayari wanapelekewa katika utaratibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Sware alitaka kujua kuhusu Kamati ya Kitaifa ya Mazingira. Kamati hii ipo na Mwenyekiti wa Kamati hii ni Katibu Mkuu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na ilishafanya kazi vizuri na ninampongeza sana Katibu Mkuu na timu yake. Wajumbe wa Kamati hii wameainishwa kwenye sheria na sheria ninayo ipo hapa, sina haja ya kukusomea kwa sababu muda utakuwa hautoshi, lakini nitakujibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati hiyo kazi iliyoifanya kwanza ilitoa ushauri kuhusu mita 60 kwenye vyanzo vya maji. Sasa hivi nasubiri wataalam wa Wizara yangu wanipe mrejesho ili sasa tutoe mwongozo kuwapelekea wananchi ni namna gani mita 60 zitaweza kufanya kazi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili walitoka kuhusu na ushauri umefuatwa na Serikali na imepigwa marufuku nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu ulikuwa wawe kwenye Mfuko wa Mfuko wa ni na tayari tumeshafanya mazungumzo na wame- kuwa Wakiingia humu kuna pesa sio chini ya Dola milioni 300 ambazo zitakuja Tanzania na zitakuwa zinasimamiwa na taasisi ambayo Serikali inaiona ni na ina

16 APRILI, 2020

ya kutunza na kulinda pesa hizi. Kwa hiyo, hongereni kwa mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za maendeleo zinachelewa, wakati mwingine kulikuwa na matatizo kama ya Italy. Kwa hiyo, hata pesa za maendeleo za mfuko lakini bahati mbaya kulikuwa na mabadiliko ya uongozi. Kwenye mabadiliko ya uongozi, kwa hiyo, aliyeingia hakuweza kuziidhinisha mpaka naye ajiridhishe. Kwa bahati mbaya sasa baada ya kujiridhisha imetoka Kwa hiyo, sasa tunasubiri tena Mungu atuondolee suala la

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimwa Saada ametoa pongezi kwa shilingi milioni 500. Muungano ni tunu ni lazima tuenzi, asiyeuthamini Muungano sio binadamu. Yeyote asiyeuthamini Muungano huu sio binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda kujitambulisha kwa Mheshimiwa Dkt. Shein, Rais wa Zanzibar alinionesha chumba ambacho Mwalimu Nyerere na Hayati Abeid Karume walikutana wakakubaliana kuweka Muungano. Karume akamwambia Mwalimu, haina haja ya mjadala, mimi ni Makamu na wewe ni Rais. Hii ndiyo ya Kiafrika, undugu, kupendana na umoja. Daima Muungano huu utadumu, yule asiyeutaka mwenye wivu akajinyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bonnah kazungumzia kuhusu suala la Mto Msimbazi. Ni kweli mimi na Mheshimiwa Bonnah tumeshafanya ziara Mto Msimbazi na changamoto ipo nimeshamwagiza Mkurugenzi Mkuu wa akakae na Mamlaka ya Mkoa wa Dar es Salaam kutizama namna gani tutaweza kuutoa ule mchanga. Mchanga huu ukitoka una ya kushuka chini na kujaa katika maeneo mbalimbali. Mchanga huu vilevile unaathiri mikoko katika Bahari ya Hindi maeneo ya Mikoko hii chakula chake ni maji chumvi. Mchanga ukijaa katika mikoko, maji chumvi hayaingii kwenye mikoko, mikoko inakufa.

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilishamwagiza Mkurugenzi wa akae na Mamlaka ya Mkoa wa Dar es Salaam kutafuta mbinu ya kutoa mchanga huu kwa kutumia utaalam. Kuna ya watu kuchimba ovyo ovyo wanaweka mashimo, yale mashimo ndiyo yanafanya ya maji kwenda kwa nguvu kupiga katika kingo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa Jangwani; mazungumzo kati ya Serikali na bado yanaendelea, tunategemea karibuni watakapomaliza watatueleza wamefikia hatua ipi? Serikali nayo vilevile lazima iwe makini, siyo kila mradi na kila mazungumzo wakubali tu, kuna masharti mengine ambayo Serikali ikiona hayafai, lazima wayajengee hoja na wakiyajengea hoja yanachukua muda kuweza kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi wa Msimbazi, Segerea na wote wanaokumbwa na Mto Msimbazi na Mto Ng'ombe hata mimi linanigusa nikiwa ni Mbunge wa Jimbo la Ilala ambapo mafuriko haya kwa kweli yanatuathiri kwa kiwango kikubwa sana. Hata hivyo, tunategemea hivi karibuni mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la dampo, hatua za mwisho zimefika, tumeshapata pesa za Uholanzi shilingi bilioni 85. Kimebaki kipengele kidogo tu Ubalozi wa Uholanzi wakirekebisha ili sasa pesa hizi zitoke na zianze kufanya kazi na dampo jipya liweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Yussuf kazungumzia kuhusu mazingira. Katika maeneo 148 ya Zanzibar na Pemba, maeneo 123 yanaathirika Pemba peke yake kutokana na mazingira. Mimi nilipata nafasi kwenda Pwese kwa Mgogo katika Kisiwa cha Pemba. Nampongeza Mkurugenzi wa Mazingira Zanzibar kwa namna alivyoweza ku- kwa muda wa wiki mbili tu ameniletea ripoti kamili ya madhara na tunakaa na timu yetu kutazama ni mfuko upi tuweze kuwapatia ili waweze ku...

16 APRILI, 2020

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimwa Nchambi mambo yako yamejibiwa na Naibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Zainab; Mheshimiwa mrembo, mzuri lakini unakuwa na roho kama ya jitu sijui la wapi! Kwa hiyo, nikuhakikishie mfuko wa pamoja uko katika hatua ya mazungumzo katika Ofisi ya Waziri wa Fedha wa SMT na SMZ

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini 4.5% ambazo kila mwaka zinakwenda Zanzibar zinakwenda na kuna akaunti maalum ambazo zinapelekwa na pesa zinazokwenda siyo kidogo sina haja ya kuzitaja sababu sidhani kama kuna umuhimu wa kuzitaja. Kwa hiyo pesa 4.5% zinakwenda na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa bandari, mradi wa bandari umekwama sababu masharti ya mtu ambaye alitaka kutukopesha hayakuwa rafiki walitaka mpaka mali za Serikali na majeshi yawekwe dhamana Serikali isingeweza kukubali kitu kama hicho. Kwa hiyo, ya Zanzibar mradi huu ulisimama lakini sasa hivi Serikali ya Zanzibar wanaujenga wenyewe tunajenga kwa pesa za ndani nampongeza sana Rais Dkt. Shein ameweza na anakusanya 93% ya mahitaji ya Zanzibar na hii inatokana na juhudi za pamoja za Rais Dkt. Magufuli na Rais Dkt. Shein Zanzibar wanakusanya Bara tunakusanya haya ndiyo mambo yanavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nahodha nakupongeza sana kwa maneno yako mazuri ya Muungano, usajili wa vyombo Mheshimiwa Mussa Hassan ni kweli kero ya miaka mingi na mimi nimesema tutaivalia njuga haya mazungumzo yako katika hatua za mwisho katika Mawaziri wa SMT na SMZ. Mheshimiwa Mbogo umezungumzia habari ya Mbweni haya ni mambo ya halmashauri lakini mradi umeyasema tutayafuatilia na kwenda kuyatembelea maeneo hayo. Suala la gesi kwenye matumizi ya mkaa Dar es Salaam ni muhimu sana, na toka nichukue Wizara hii tushakutana na wadau wa Taifa gesi, Oryx, gesi

16 APRILI, 2020

kutizama namna gani gesi iwe na bei nafuu ili wananchi waweze kunufaika.

Mwaka 2011 peke yake Mkoa wa Dar es Salaam ulitumia mkaa tani 1,000,000 wakati Dar es Salaam ilikuwa na watu wa 3,500,000 leo Dar es Salaam ina takriban watu zaidi ya 7,000,000 kwa hiyo tunajua mazingira yanavyoharibiwa. Nampongeza Mheshimiwa Kubenea kwa kuwa na msimamo mzuri wa Serikali kupambana na suala la ugonjwa wa corona. Suala la Katiba limejibiwa vizuri tu na Mwanasheria Mkuu, Ali King amezungumzia Muungano amesifia Hazina ni kweli ni Hazina. Mheshimiwa Khadija amezungumzia ambayo tushayatolea maelezo kikubwa ni kulinda muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya wale ambao hatujajibu tutayajibu kwa maandishi na tutayajibu kabla ya Bunge kwisha. Baada ya maelezo haya naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana sasa kwa ule utaratibu wetu, kuna Wabunge mbalimbali ambao wameomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri halafu tutamaliza, tutaanza na Mheshimiwa Dkt Saada Mkuya Salum, halafu tukimaliza naye tutaendelea na majina mengine niliyonayo hapa.

HOJA ZA KISERA

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nilikuwa nataka ufafanuzi juu ya sheria ya mikopo, misaada na dhamana ya mwaka 1974 kama

ilivyorekebishwa mwaka 2003 na yakaja marekebisho mengine makubwa zaidi mwaka 2017. Mwaka jana wakati tunachangia Bajeti Kuu ya Serikali, tulitoa hisa hizo na majibu yaliyotoka ni kwamba jambo hilo siyo jipya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshalileta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nilitaka kujua sasa iko katika hatua gani katika kuona kwamba yale marekebisho ambayo pengine yameiminya sana Zanzibar katika sheria hiyo hatua gani imefikia ili kuona kwamba tunaweka uwiano katika sheria hii, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saada nisaidie jambo moja hii sheria inamtaja Waziri huyu kwamba ndiyo Waziri mhusika ama Waziri tofauti na huyu ili nijue kama swali hili anaweza yeye kulijibu au hapana kabla sijamuita, anayetajwa mle kama Waziri msimamizi ni Waziri yupi?

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, anayetajwa katika sheria ni Waziri wa Fedha lakini niliongea hili kwasababu lilikuwa katika hisa ya Muungano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saada nadhani hilo tutaweza kulipeleka mbele kwasababu huyu Waziri wa Muungano kama siyo yeye anayehusika moja kwa moja anaweza asiwe na majibu hapa halafu tutakuwa tumemuweka kwenye kikaango. Mheshimiwa Ali Hassan King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kiufupi hoja yangu ilikuwa inahusiana na masuala yale ya bei ya umeme lakini Waziri amenipa hapa kwamba tayari suala linashughulikiwa kwa hiyo naiondoa hoja yangu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante hoja yangu Mheshimiwa Waziri ameigusia lakini sijaridhika vya kutosha kuhusu kwasababu hili ni takwa la kikatiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Tume ya pamoja ya kaunti kwa hivyo nikitaka ufafanuzi zaidi hili takwa hili la kikatiba litakamilika lini kwasababu sasa hivi tuna nusu karne na miaka sita juu, naomba ufafanuzi akaunti ya pamoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nawaza kama ni la Wizara ya Fedha hili, ama ni la Muungano kwasababu wakati mwingine tunaweza kumpa mtu maswali ambayo yeye hayamuhusu yeye.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la Muungano akaunti ya fedha ya pamoja.

NAIBU SPIKA: Msimamizi ni nani Mheshimiwa, msimamizi ni nani?

WABUNGE FULANI: Wizara ya Fedha.

NAIBU SPIKA: Basi Wizara ya Fedha bajeti yake itakapofika ili tupate majibu mahususi kwa maswali yetu kwasababu tukimpa Waziri ambaye hasimamii hicho kitu hatutapata majibu yale ambayo tunataka kama Bunge. Mheshimiwa Ally Saleh kutokea Msekwa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Mheshimiwa Waziri niliuliza nilichangia juu ya hoja ya wale watu ambao wanataka fidia yao na akasema tu kwamba hili suala hili liko njiani na atajibiwa lakini sasa ni mwaka wa tano watu wale hawajajibiwa nataka nipate maelezo ya kutosha kwamba watu wale kweli watapewa fidia yao kwasababu mwaka wa tano nawashaandika barua zinafika laki moja hawajajibiwa napenda kupata maelezo ya Waziri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh sijui ni Mwanasheria wao anajua hadi barua ziko ngapi, laki moja Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mussa Sima ufafanuzi

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nilijaribu kueleza nadhani Mheshimiwa Ally Saleh hajanielewa ama hajaridhika nimesema nakubaliana na kwasababu makazi ya Makamu wa Rais tunataka kuweka uzio na kama alivyoeleza wako watu wanaishi mule tayari imeshafanyika tathmini kilichofuata hatua baada ya ile tathmini ya kwanza ni kupeleka Wizara ya Fedha na nikasema Wizara ya Fedha wamekwishaunda kamati na hiyo kamati nikasema nawapa watu wale kwamba jambo hili kamati inaenda kujiridhisha kama haya madai ama hiyo iliyofanyika ni sahihi ikishajiridhisha wanalipwa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cosato David Chumi.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika na jawabu na...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cosato Chumi ngoja tumsikilize Mheshimiwa Ally Saleh

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, hii miaka mitano na ahadi kama hii wamekwishaambiwa mara nyingi sasa ni lazima tupate ya Kibunge hili jambo lijadiliwe na Bunge kwamba kwanini wanawaweka watu 50 katika kuwaning'iniza kwa miaka mitano na kama sikupata jawabu la kutosha nitatoa shilingi lijadiliwe namna gani kwasababu kesi kama hizi zishakuwa nyingi mwaka jana kuna watu walihamishwa kupisha Jeshi la Ulinzi matokeo yake wakakaa muda mwingi hawajahamishwa mpaka mwaka jana ikajadiliwa na hatukuambiwa taarifa mpaka leo kwamba wale watu wale baada ya kujadiliwa

16 APRILI, 2020

wamehamishwa hawajahamishwa kama sitapata jawabu la kutosha nitatoa shilingi ili tuwatetee wananchi wetu kwasababu wamekuwa wakining'inizwa sana na Serikali wanapotaka maeneo yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh hata hivyo tulitoa tu fursa Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu kwasababu hilo suala ni mahususi siyo suala la kisera kimsingi na tunajua unapohoji mshahara wa Waziri ni kuhusu mambo yale ya jumla na ya kisera sasa hili ni jambo mahususi hata hivyo niliona Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kusimama kutoa ufafanuzi zaidi.

NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufuatilia kwa undani kabla hata hatujaja hapa kamati hii ilikuwa iende mwezi huu lakini kulingana na hali iliyoko Zanzibar na sisi tunataka kuendelea kuomba rehema za mwenyezi na mapenzi yake mema jambo hili la ugonjwa huu wa Corona walau liishe ama lipungue baada ya hapo wale watu watapata fursa ya kwenda ya Serikali ni kwamba watu wako tayari ni wakati tu unasubiriwa kwenda na Serikali iko tayari kulipa sijajua Mheshimiwa Ally Saleh anataka kitu gani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Masuala ya fidia ni ya kisheria na licha kuwa imechukua muda mwingi kuna watu wamefariki kuna masuala ya mirathi. Kwa hiyo, ile timu ya tathimini lazima iridhike nani anayempa pesa na nani anayepokea pesa kuepusha migogoro ya kifamilia ambayo inaweza kutokea kwa hiyo Mheshimiwa Ally Saleh yeye aendelee kufutulia tu lini hawa watu watakwenda nafikiri karibuni watakwenda na watayamaliza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cosato David Chumi ufafanuzi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa kuokoa muda kati ya masuala ambayo kamati ilikuwa imeshauri ni pamoja na kuhakikisha kwamba mfuko wa mazingira unawezeshwa na kuanza. Lakini pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 35 na 36 imeeleza jinsi ambavyo na kusisitiza umuhimu wa taasisi za umma na binafsi kuweza ku- na kupata ithibati ili ziweze ku- kutoka mifuko mbalimbali ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba ufafanuzi Serikali katika jambo hili imejipangaje kuzijengea uwezo taasisi za umma na binafsi ili ziweze ku- na kupata hizo kama ilivyofanya kuweza ku- hizo ili tukabiliane na masuala mazima ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Chumi kwa hoja yake ya msingi, kama vile walivyoingia CRDB, Wizara ime- hii kwa mashirika yote, sasa wizara haiwezi kumfundisha mtu kuja ku- hizi inatakiwa taasisi za zenyewe ziwe na watalaam wa kuweza kuingia katika mfumo unaotakiwa ili na wao waweze ku- kwa hiyo ushauri wangu ni kuwa watafute wazuri mkae nao na fedha hizi zipo kama walivyofanya

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimwa Wabunge hoja ililetwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira akiomba Bunge liridhie fedha ambazo amezitaja kwenye hotuba yake na kamati

16 APRILI, 2020

yetu imetusaidia imepitia ikaleta taarifa yake hapa kamati zote mbili kwa niaba yetu sisi sote na kwa utaratibu wetu ilipaswa wakati huu Waheshimiwa Wabunge mhojiwe kwa sababu hoja ilishaungwa mkono sasa kwasababu wote tumeingia kwenye huu mtandao ambao ametuwezesha Mheshimiwa Spika ninazo taarifa hapa za kura, kura zimepigwa jumla ya 326 na Wabunge wengi kati ya hizo wamesema ndiyo.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 26 – Makamu wa Rais.....Sh.8,759,191,000/=
Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais.....Sh.11,581,534,000/=

NAIBU SPIKA: Kwa hivyo makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ambayo hoja yake imeletwa na Mheshimiwa Waziri ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 imepitishwa na Bunge.

Kwa maana hiyo nichukue fursa hii kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge wote kuwashukuru sana Wabunge ambao wameshiriki ngazi ya kamati lakini pia humu Bungeni kuchangia hata wale wenzetu ambao wameshirikiana nasi kutokea Msekwa na kumbi zingine, tunawashukuru sana kwa mawazo yenu mliyoyatoa.

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri walikuwa wakiandika hapa na wataalam wao wapo wameyachukua mawazo yenu na naamini yataboresha utendaji kazi wao ukizingatia hii bajeti waliyoiomba na ninyi mmeipitisha kwa kuamini kwamba wataendeleza utendaji kazi wao mzuri ambao wengi wenu hapa mlikuwa mkipongeza.

Nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Wizara hii kwasababu mambo yote ambayo mnayasimamia ni ya

muhimu sana na hata hizi zinazoitwa changamoto ama kero naamini kwa sababu mmeshafanya kwa asilimia kubwa sana hata hizo zilizosalia basi mtaweza kuzifanyia kazi. Na michango mingi naamini watalaam wenu wameichukua na wataboresha namna ya utendaji kazi wenu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nilite kwenu taarifa ama mwongozo wa Mheshimiwa Spika kuhusu tahadhari zaidi katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona tangu kutangazwa kwa ugonjwa wa corona COVID 19 tarehe 16 Machi, 2020 hatua mbalimbali zimechuliwa kitaifa na kitaasisi ili kujikinga na mambukizi ya ugonjwa huo.

Kwa kuzingatia ongezeko la wagonjwa hapa nchini sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaowajibu wa kuchukua taadhari zaidi katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona ili kukamilisha jukumu muhimu kwa sasa la kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kutunga sheria. Kwa sababu hiyo Mheshimiwa Spika analeta kwenu waraka huu unaotoa msisitizo zaidi katika kujikinga na ugonjwa wa Corona.

(a) Taarifa ya Waziri wa Afya ya tarehe 15 Aprili, 2020 imeonesha kuongezeka maambukizi katika Jiji la Dar es Salaam na Zanzibar na maambukizi mapya katika maeneo ya Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na Kagera. Hivyo ni muhimu sana kupunguza safari za Dar es Salaam na maeneo mengine kwa ujumla na hii inasaidia kupunguza hatari ya maambukizi katika taasisi yetu.

(b) Kuzingatia umbali kati ya mtu na mtu kwa maana ya na kupunguza mizunguko ndani ya jiji ya Dodoma. Mheshimiwa Spika anawashauri na kuwasisitiza kwamba mtindo wa nyumbani Bungeni, Bungeni nyumbani iwe ndio mwenendo wa maisha kwa wakati huu. Hata mahitaji ya nyumbani kutoka sokoni kuwe na siku maalum ikiwezekana mara moja kwa wiki

(c) Kulingana na taarifa za Wataalam wa Afya ugonjwa huu wa corana umeonekana kuwa na maadhara zaidi kwa

16 APRILI, 2020

wazee na watu wenye magonjwa sugu kama kisukari, shinikizo la moyo, pumu, kifua kikuu, saratani, figo na mengine. Hivyo basi ni vyema wenye maradhi hayo wakachukua tahadhari zaidi na kujikinga na maambukizi na hivi virus vya corona.

(d) Kuendelea kufuata ushauri wa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji na sabuni pamoja na matumizi ya vitakasa mikono yaani ili kuendelea kuepukana na maambukizi ya virus hivi. Pamoja na hayo yote ni muhimu tuzingatie lishe bora, maji ya kunywa ya kutosha, mazoezi mepesi na kupata muda wa kupumzika kwani haya ni mambo muhimu katika kuimarisha afya zetu.

Aidha, tuepuke kufuatilia na kutazama habari za kuogofya na kujenga hofu kwani hofu inaweza kuongeza msongo wa mawazo na kuzorotesha afya zetu. Mwongozo huu umetumwa kwa Wabunge wote kwa hiyo mnao kwenye zetu mtaupata, mtakapoangalia kwenye taarifa za kiofisi.

Waheshimiwa Wabunge maelekezo haya yaliyotolwa na Mheshimiwa Spika wote tuyatilie maanani na wale ambao pengine tunayo haya maradhi yaliyotajwa siyo tu maradhi kwa sababu pia kuna umri ni muhimu sana kufuatilia afya zetu kipindi hiki. Lakini pia hata sisi wenyewe kukaa mbali na hawa wengine ambao wanaweza kutuletea sisi madhara makubwa. ()

Waraka huu umetolewa na Mheshimiwa Spika siku ya leo tarehe 16 Aprili, 2020 naamini wote tutazingatia maelekezo haya aliyotoa Mheshimiwa Spika ikiwa ni pamoja na kupunguza safari zetu za kwenda sehemu zenye maambukizi ambazo ni Dar es Salaam na Zanzibar.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 17 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana.